
# MAISHA *ni* Kutafuta *Siyo* Kutafutana



Denis Mpagaze

# MAISHA NI KUTAFUTA
# SI
# KUTAFUTANA

**Denis Mpagaze**

# Yaliyomo

***Sura ya 1***
Subiri Viatu Vya Marehemu Utatembee Peku Muda Mrefu! ... 5
***Sura ya 2***
Tafuta Pesa Uepuke Dharau ... 11
***Sura ya 3***
Chukua Siri za Kupata Mtaji Uache Kulaumu Watu ... 15
***Sura ya 4***
Imani Pasipo Kuhoji ni Ushirikina! ... 21
***Sura ya 5***
Wekeza Ovyo Uwe Msema Ovyo ... 26
***Sura ya 6***
Chuki ni Sawa na Kunywa Sumu Afe Usiyempenda! ... 30
***Sura ya 7***
Ulimi Unang'ata Zaidi ya Meno ... 34
***Sura ya 8***
Kauli 10 Hatari Katika Ujasiriamali ... 42
***Sura ya 9***
Matatizo Hayaondoki Kwa Kulialia ... 51
***Sura ya 10***
Jina Lako Laweza Kuwa Sababu ya Balaa Unazopitia ... 57
***Sura ya 11***
Maskini Hana Hoja, Maskini Ana Haja ... 64
***Sura ya 12***
Ushirikina ni Nini? ... 72
***Sura ya 13***
Maisha ni Kitendawili, Kitegue Uteguke! ... 79
***Sura ya 14***
Siri ya Jogoo Katika Maisha ... 83
***Sura ya 15***
Mambo Kumi Kuhusu Mikopo ... 91
***Sura ya 16***
Aina za Tatu Marafiki ... 96
***Sura ya 17***

Mbona Tunazidi Kuwa Wajinga? ........................................ 100
***Sura ya 18***
Ngoja Niwakeree! ............................................................... 103
***Sura ya 19***
Tunaishi Katika Dunia ya Namna Gani? .............................. 108
***Sura ya 20***
Ukishukuru Mungu Anatenda, Ukiacha Shetani Anatenda .. 114
***Sura ya 21***
Mambo Haya Yanakugharimu ............................................. 120
***Sura ya 22***
Tukosoane, Tusitetane ........................................................ 125
***Sura ya 23***
Hasara Katika Biashara ni Giza la Kuona Nyota ................. 127
***Sura ya 24***
Amri Kumi za Kunasa Wateja ............................................. 131
***Sura ya 25***
Dhambi Saba Takatifu ........................................................ 135

**Sura ya 1**

# Subiri Viatu Vya Marehemu Utatembee Peku Muda Mrefu!

Mtegemea vya nduguye hufa maskini na vya kupewa hulemaza akili ni methali zinazotukumbusha kwamba utegeaji katika maisha haufai; ni sawa na kupumua kwa kutumia pua ya mwenzako. Haiwezekani. Kufanya hivyo ni sawa na kusubiri viatu vya marehemu. Utatembea peku hadi miguu iote tende. Maisha yamebadilika sana. Unatakiwa ujue hilo. Tunaishi katika nyakati za ukizubaa unalala njaa hata kama kaka zako wana pesa! Habari za kabla bro hajaoa alikuwa mtu freshi, utazisikia kwa watu wajinga. Kusubili kulishwa ni sawa na kucheza Makirikiri wakati linapigwa Sebene!

Acha utoto mwanangu, kaka yako naye anajenga familia yake kama alivyojenga baba yenu. Zama za kuhamia kwa mjomba na wadogo zako kwa shemeji yenu zimeisha. Uncle yuko busy na watoto wake, bro yuko busy na mke wake, shemeji busy na nyumba yake, huoni kama unawatafuta ubaya?

Michael Bassey Johnson aliwahi kusema kama unataka ndugu na marafiki wakuheshimu wathibitishie kwanza kama unaweza kujilisha. Hata huyo mke wa kaka yako unayemponda kila siku atakuheshimu mpaka utashangaa. Kwanza ukienda kumtembelea atakukupokea kwa heshima na hatokuliza utaondoka lini. Lakini kama ni kabwela sasa, hata begi ulilobeba utaingia nalo ndani mwenyewe bila kupokelewa na mtu ili upate cha kusema siku ukirudi kwenu. Utakalia lawama ati mke wa kaka yako ni mbaya

utadhani kaka alikuoa wewe. Kijana anayeendesha magari ya baba yake hana jeuri kwenye kikao cha vijana wanaomiliki baiskeli walisema wahenga.

Ukimudu kujilisha pamoja na umaskini wako utaheshimika kuliko msomi anayetegemea kulishwa. Utaitwa maskini jeuri. Miaka 30 bado unazengea msosi kwa kaka yako, shemeji yako akikutuma ufue nguo za mtoto unaruka juu, akikushitaki kwa kaka yako ukatimuliwa unasema kaka amelishwa limbwata kumbe wewe ndo limbwata mwenyewe! Kama umeamua kukaa kwa ndugu yako basi kubali kutumika kwelikweli maana wazungu wanasema, **"He who pays the piper calls the tune"** kwamba shemeji anayekulisha ndo hukupangia nguo za kufua kwa ajili ya watoto wake. Vya bure viko mtoni, siyo bombani. Vya bombani vinalipiwa ndiyo maana mwenye bomba hapangi foleni!

Vya bure vinapatikana kwa wazazi wako tu siyo kwa kaka yako. Ni wazazi tu ndo huwa hawawachoki watoto wao hata kama ni maskini, ingawa wengi mkiyapatia maisha huwa mnawasahau kwa sababu shukurani ya punda ni mateke. Watoto 12 mnashindwa kuwatunza wazazi wenu wawili na wakati wao wawili waliweza kuwatunza nyote 12 hadi mkasoma.

Mwanangu kama bado unapumua komaa tu mwenyewe otherwise kuendelea kumtegemea mwanadamu yanaweza kukukuta yaliyomkuta Wambura wa Mitandaoni. Wambura alivyotupwa gerezani alikula dili na mlinzi wa gereza amtoroshe. Mlinzi akamwambia, siku mfungwa akifa na jeneza kuletwa gerezani jitahidi ikifika usiku uingiemo halafu ujifunike na marehemu. Asubuhi wakati wa kwenda kuzika tutakubeba na tukifika makaburini baada ya kuzika nitarudi kukufukua haraka halafu unasepa zako. Baada ya muda kweli mfungwa akafa na jeneza likaletwa gerezani. Ilipofika usiku Wambura akaingia kwenye

jeneza akatulia ndani yake. Asubuhi wazikaji wakabeba jeneza mpaka kaburini. Wakazika. Wambura akasubiri mfukuaji aje lakini hola, joto linazidi kumkaanga, masaa yanakwenda. Alipoangalia kwa makini akagundua kumbe aliyekufa ni mlinzi aliyekuwa akimsubiri aje kufukua kaburi.

Wambura ndo akapotea hivihivi! Sasa sitaki na wewe upotelee kaburini ukiwa hai kama Wambura. Asante sana Mwl. Wa Kiswahili kwa utunzi murua wa kutukumbusha tusiwe kama Wambura. Ni bora ukomae tu kwa sababu mtafutaji halali njaa. Anayemtegemea mjomba ndo rahisi sana kulala njaa. Ukitia bidii maishani lazima utoke mwanangu maana jembe halidanganyi, unaweza usiwe tajiri lakini bado ukaonekana mtu mbele za watu. Kwanza utajiri ni mgumu ndo maana sipendi kuujadili ingawa nautaka. Tatizo utajiri ni kuinyima roho. Sasa naanzaje kuinyima roho na wakati maisha yenyewe kama maua tu, asubuhi limechanua jioni limenyauka.

Cha msingi komaa kumiliki vyako hata kama ni vibaya kama gari la fundi pikipiki. Gari la fundi pikipiki nyuma limeandikwa BABA YAKO ANALO?

Ondoa kwenye akili yako kwamba ndugu ni lazima akusaidie na ingiza fikra za kujisaidia. Tengeneza kesho yako. Kesho yako inahitaji mengi kutoka kwako zaidi alisema Frank Tyger. Acha kutolea macho mali za baba yako, tafuta zako wasikutoe roho. Vya urithi masimango, hayaishi. Kujitegemea ndo njia pekee ya kuelekea kwenye uhuru kamili alisema Patricia Sampson.

Kwanza Mungu amekupa miguu miwili ili uweze kusimama bila kushikwa sasa kulilia kubebwa na umri umekwenda ni huzuni kubwa kwa waliokuzaa. **The strongest man in the world is he who stands alone** alisema Henrik Ibsen mwandishi wa Kitabu

cha An Enemy of the People ulichokisoma high school ukatoka kapa.

Kutegemea vya watu huumiza moyo hasa pale wasipokutumizia hitaji lako. Utaishia kutukana watu moyoni kila siku. Ili usife kwa presha jenga tabia ya kujitegemea mwenyewe kama Shakespeare. Shakespeare anasema, 'I always feel happy. You know why? Because I don't expect anything from anyone" Akimaanisha kwamba siku zote yeye ni mwenye furaha kwa sababu hategemei chochote kutoka kwa mtu.

**Expectations always hurt** walisema wahenga wa Uingereza. Ukiwategemea sana watu utakuwa mtu wa kulalamika ati wamekukwamisha kumbe ulijikwamisha mwenyewe kuwategemea. Kama kivuli chako mwenyewe ikifika usiku kinakuacha sembuse mwanadamu mliyekutana barabarani? Amebarikiwa mtu yule asiyetegemea lolote kutoka kwa watu kwa sababu kamwe hatavunjika moyo alisema Alexander Pope.

Kwanza kumbuka Duniani ulikuja peke yako, hivyo uko peke yako. Mungu aliumba watu kwa ajili ya kutegemeana na siyo kutegeana. Afrika tunasema **I am because you are!** Yaani nipo kwa sababu upo. Kumtegemea mtu ni unyonyaji ndo maana watu wa Pwani wanasema, “Mgeni siku ya kwanza, mpe mchele na panza, siku ya pili, ya tatu na ya nne, mpe jembe akalime, akirudi muagane, aende zake mgeni.” Kumuonea aibu mgeni ni kutiana umasikini kwa jina la ukarimu ni jadi yetu. Kumbe ukarimu ukizidi ni uwenda wazimu, nimewahi andika maneno haya kwenye kitabu changu cha Ukombozi wa Fikra, mjomba wangu alipokisoma alinigombeza kweli. “Wewe Denis kwa nini unafundisha uchoyo?” Ukarimu wa mjomba wangu akifika kilabuni ulinishangaza,maana aliamrisha lete kama tulivyo ndo maana nikawaandikia wenye fikra kama za mjomba wangu.

Kutegemea vya watu ni sawa na kupima kina cha maji kwa miguu yote. Kama ni parefu unapimwa jumla. Watoto wa mjini wanasema pima upimwe! Ukiwekeza maisha yako juu ya mtu siku akikuacha utajiua. Biblia iliposema amelaaniwa amtegemeaye mwanadamu na kumwacha Mungu ililenga kutukumbusha kwamba mtu anakufa mara moja lakini Mungu ni wa milele. Ni bora tumtegemee Mungu tusiyemuona lakini yupo milele kuliko kumtegemea mtu tunayemuona lakini hana uhakika wa kuwepo milele.

Huwezi kupata maendeleo kwa asante. Fimbo ya mbali haiui nyoka. Kufanya hivyo ni sawa na kusubiri viatu vya marehemu, lazima miguu ionte sugu. Kumbuka nguo ya kuazima haisitiri matako. Kashone nguo yako ili usiwe kituko mtaani. Fanya kazi kama mtumwa ili uishi kama King Mswati lakini usile mabinti za watu kama Mswati. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu ni methali tuliyokaririshwa shuleni ili kufaulu mitihani pasipokujua maana. Ngoja nikwambie. Maana ya Mgaagaa na upwa hali wali mkavu ni kwamba jembe halimtupi mkulima, riziki ya mbwa iko miguuni, mtembea bure si mkaa bure, mtafutaji hawezi kula wali wa bila mboga. Asante kwa kunielewa kirahisi.

Kusubiri vya watu unaweza kufa hujavipata ukajikuta motoni ingawa tumeanza kuaminishana kwamba hakuna motoni. Mungu alikuumba katika ukamilifu. Nguvu ya kushinda na kushindwa iko ndani yako. Ukisubiri nguvu kutoka nje inaweza kukuua. Hata yai likipasuliwa na nguvu kutoka nje kifaranga kinakufa, lakini nguvu ya kupasua yai ikitoka ndani kifaranga kinaishi. Mambo makubwa huanzia ndani mwako. Acha kulialia kwa kuachwa na uncle, shemeji, mjomba na marafiki. Usipoteze muda kuwashambulia ndugu zako eti hawakusaidii. Hii haitakusaidia kitu zaidi ya kupanda hila kwa mavuno ya ufukara. Macho ya mbwa hayamzuii shemeji yako kula nyama. Kelele zako mbele ya uncle ni sawa na macho ya mbwa. Kelele za chura hazimzuii

ng'ombe kunywa maji. Acha kupoteza muda wako kufix blames badala ya kufix problems. Kufanya hivyo ni sawa na kukata tawi la mti ulilokalia kwani utaumia wewe.

Ukisubiri vya kupewa utaambulia mifupa kama mbwa. Usidhani mbwa wanapenda kula mifupa, ni kwa sababu hakuna anayewapa nyama. Maisha ya kutegemea vya watu hayana uhakika sana fanya kuachana nayo. Ni sawa na fimbo ya mbali, haiui nyoka.Vya bure vinafedhehesha viogope kama chakubimbi. Kuna gari lilikuwa linasafirisha vichaa, walipofika porini walisimama kuchimba dawa, vichaa wote wakakimbia. Hilo likawa balaa kwa dereva na konda maana kibarua kinaweza kuota. Dereva kuona hivyo akamwambia konda tutafanyaje sasa? Konda akajibu **niachie mimi nitaliweka sawa hilo, we kanyaga mafuta tu**.

Wakandelea na safari hadi stendi, wakakuta abiria kibao. Wakatangaza msaada kwa anayehitaji, abiria wakajazana maana vya bure hushambuliwa hata kama vinasumu. Dereva akawasha gari. Konda akamwambia dereva haina kituo hiyo, moja kwa moja mpaka hospitali. Gari likafika hospitali, abiria wote wakaingizwa wodi ya vichaa na kupigwa sindano za usingizi. Vya bure vikawagharimu. Kutegemea vya watu ni sawa na kupiga sarakasi umevaa taulo. Utafedheheka.

Tujenge jamii ya kushikamana na siyo kushikwana, jamii ya kubebana na siyo kubebwana, jamii ya kupendana na siyo kupendwana, jamii ya kutafuta si kutafutana. Kiswahili kitamu!

## Sura ya 2

# Tafuta Pesa Uepuke Dharau

Tafuta pesa mwanangu upunguze kumuita kila mtu, **mkuu, kiongozi, mkurugenzi, bosi!** Unajiabisha sana mwanangu. Pesa hainunui furaha lakini ni lini umaskini ulinunua furaha? Bora pesa kuna uhuru itakupa!

Tafuta pesa kijana wangu ili hata Polisi wakikukuta umetulia sehemu wakuulize **mkuu kuna shida yoyote?** Pesa haidanganyi mwanangu, ukiwa nazo utaitwa mfalme, usipokuwa nazo utaitwa mhenga. Enzi zetu muhenga alikuwa mzee mwenye akili, siku hizi muhenga ni mwanaume asiyekuwa na pesa hata kama bado hajazeeka!

Tafuta pesa binti yangu hata siku unapopewa appointment ukafika kabla ya honey wako uwe na ubavu wa kuagiza hata soda ya kopo kuliko kusimama nje ukitoa macho utadhani mwewe unazengea kifaranga kumbe ni binti mrembo aliyefulia. Wanaweza kukuitia mwizi ukapigwa bure. Ohooooh!

Tafuta pesa kijana wangu ili eupuke usumbufu wa kujitambulisha kwa kujieleza sanaaa. Unajua mimi ni mtoto wa binamu yake na Donald Trump. Mara nilisoma na mtoto wa Jakaya Kikwete. Mateso yote hayo ya nini? Ukiwa nazo watakutambulisha tu. Utasikia **kutana na cousin yangu Mkurugenzi wa CRDB Dar**, **kutana na kaka yetu Mkurugenzi wa viwanja vya ndege. Haya wewe jitambulishe!**

Tafuta pesa kijana wangu uepuke kunyanyaswa na mapepo kwenye mikutano ya injili. Ndiyo kwani nani huwa wanaangushwa na mapepo. Umewahi kuona tajiri kagaragazwa na mapepo hadharani? Thubutu. Pesa ina mamlaka ya kuamrisha hadi mapepo yanyamanze na yakanyamanza. Kama natania acha kusaka pesa utaniambia!

Tafuta pesa kijana wangu usionekana mkorofi. Siku zote kama huna pesa hata kwenye vikao vya familia ukinyoosha mkono kuchangia hoja wanasema unataka kuleta fujo, kumbe unabonge la point! Yaani kama huna pesa utasikilizwa na mama yako tu. Hata yeye ipo siku atakuchoka!

Tafute pesa uepuke kulala kwenye guest zenye ndala za miguu tofauti na rangi tofauti ili usije kuiba. Maskini haaminiki kuanzia kwao hadi guest! Inatia huruma lakini ndo hivyo hakuna jinsi! Halafu hawa watu wa guest wangejua maskini siyo mwizi kabisa, wasingemfanyia hivyo!

Tafuta pesa makonda wa daladala wasikutukane kama yule babu aliyesema **konda, ongeza sauti tumsikilize baba wa taifa**. Konda akamjibu vibaya kweli. U**ngemsikiliza baba wa taifa ungekuwa na gari lako**! Jamani. Umri siku hizi siyo kitu bila pesa.

Tafuta pesa kijana wangu upunguze hasira za haraka. Kama huna pesa ukiguswa kidogo unalipuka. **Baby nahamu na kuku leo.** Sikiliza majibu. **Una hamu ya kuku umekuwa mwewe?** Mtu asiyekuwa na pesa ndugu zake wenye pesa wakimgusa kidogo utasikia, **niueni, nasema niueni!** Sasa wakuue mara ngapi mwanangu na wakati uliishajifia? Tafuta pesa mwanangu, mimi

naongea kupitia uzoefu! Yasije kukuta ukasema baba hakuniambia.

Tafuta pesa hata ukiendaa ukweni ukifika wasemee shemeji amekujaa na siyo mume wa dada amekuja! Huna pesa mama mkwe atakuomba umsaidie kupasua kuni. Yanachekesha lakini ndo ukweli mwanangu! Tafuta pesa siku ukitua ukweni wasikuulize unaondoka lini!

Lakini ukipata pesa mwanangu usiende kupiga nazo picha na kuzisambaza mitandaoni, utawaumiza wasiokuwa nazo! Wengine watasema unajidai maana watu wengi wanapenda kuona unapost ujinga tu. Ukipost ujinga kila mtu atakupongeza!

Tafuta pesa mwanangu usijekujinyonga siku wenye pesa wakikunyang'anya mpenzi wako unayemuita malaika. Hivi uliona wapi malaika anaisha motoni? Malaika anaishi peponi. Tafuta pesa mpenzi asikukimbie. Kuna kijana alimwambia mke wake, bebi siamini kama nimekupata. Mke akajibu. Amini tu mume wangu, mie ni wako, omba Mungu tu usiishiwe!

Ukikosa pesa kila jambo litakuwa gumu kwako hasa yanayohitaji pesa. Ukikosa pesa waweza kufa kwa mafua huku ndugu wenye pesa wapo wakisubiri kutoa pesa siku ya msiba wako.

Tafuta pesa mwanangu ndugu wakutembelee. Kama huna pesa utatembelewa na ndugu zako siku ya kuzikwa. Ndio, watasafiri umbali mrefu kuja kuzika. Wakifika msibani watauliza kwani aliugua? Hawajui hata kama uliugua kumbe mwenzao ulikaa wodini mwezi mzima. Hakuna anayejua kama uliugua kwa sababu maskini hatembelewi, maskini hapigiwi simu, yeye ndo anapiga. Mwenye pesa akiugua hata mafua ukoo mzima

wanatumiana taarifa. Kila mtu atakupigia simu **unaendeleaje kaka?** Kama huna pesa taarifa zako zitawafikia ndugu zako ukifa.

Ukikosa pesa na ukawa na bidii ya kwenda kanisani watasema shida ndo zinakupeleka huko. Hakuna ugonjwa mbaya kama kukosa pesa. Huna pesa utashindwa kutoa hata sadaka na kupishana na heri maana imeandikwa **heri kutoa kuliko kupokea**. Mtumikie Mungu kwa mali zako. Sasa utatoa nini na wakati huna cha kutoa?

Pesa ni sabuni yenye uwezo wa kusafisha na kuondoa takataka zote akilini na rohoni, pesa ni tamu kama mlio wa ATM wakati inahesabu hela, hakuna meseji tamu kama ya meseji ya muamala simuni. Tafuta pesa usijenyang'anywa watoto wako uzeeni. Utaambiwa wewe siyo baba yao. Ohooo!

Najua nikikwambia utafute pesa utaniambia huna mtaji mwanangu. Fungua sura inayofuata nimekupa mbinu za kutafuta mtaji. Ukizifuata kwa uaminifu na kumaanisha lazima upate mtaji huo.

# *Sura ya* 3

# Chukua Siri za Kupata Mtaji Uache Kulaumu Watu

Kelele za sina mtaji ni nyingi! Unakutana na mtu kijana katupia pamba za bei mbaya, mkononi anasimu ya bei mbaya isiyoishiwa bando la kupost kila anachokifanya kuwarusha roho wanaomchukia na wasiompenda. Ukimkadilia thamani yake kuanzia kichwani hadi mguuni ni mshahara wa mtu, halafu mtu huyu anakwambia ana bonge la idea ya biashara lakini amekosa mtaji na wakati simu yake tu ni mtaji tosha. Hapa tatizo siyo mtaji, tatizo liko kichwani. Anaumwa akili, akipona atajishangaa jinsi anavyochezea mtaji. Mtaji hukusanywa kwa kudunduliza, Wazungu wanaita kusevu. Unaweza kujiuliza cha kusevu chenyewe kiko wapi? Hiki hapa siri ya kuseve!

1. **Acha manunuzi yasiyo ya lazima.**Siyo lazima unywe vitamu na vikali kila siku kwa sababu usipofanya hivyo hufi. Kama unabishi jaribu uone! Utapata mfadhaiko wa akili kwa muda mfupi tu lakini utazoea! Jaribu brother uone kama utakufa! Ukifa utakuwa umefail, usipokufa basi umetoboa. Fanya hivyo uone kama hujapata za kusevu. Ndani ya mwaka mmoja lazima utakuwa na mtaji. Unashangaa mwaka mmoja kwamba ni mrefu. Dangote amefika hapo alipo baada ya kusota kwa miaka 30.

2. **Punguza ukarimu wa kutoa ofa kwa sababu ukarimu ukizidi ni uwenda wazimu**. Wewe siyo Yesu hadi umnyweshe kila uliyemkuta baa, umlishe kila uliyemkuta kantini, umlipie nauli kila uliyemkuta kwenye daladala. Mtu mpaka kwenda baa lazima ana pesa yake. Acha maonyesha ya kitoto uokoe pesa upate mtaji. Halafu usipende kutembea usiku wewe siyo bundi. Kumbuka lolote linaweza likatokea likakugharimu pesa, ukakosa za kusevu!
3. **Siyo lazima kununua chai unapokwenda kazini na wakati unaweza kutengeneza chai yako mwenyewe**. Nunua hata birika la kuchemshia maji kama ofisi yako ina umeme na kama haina umeme basi nunua chupa ya kubebea chai kutoka nyumbani. Fanya hivyo uone kama hujaokoa shilingi za kutosha mwisho wa mwezi, ukapata cha kusevu, ukafungua biashara ukaachana na ajira! Utamu wa ajira usisubiri kustaafu! Wazungu wanasema retrire young and rich. Mimi tu ndo nilistaafu young and poor!
4. **Acha tabia ya kulakula ovyo kila unachokiona barabarani maana vinakugharimu**. Umeona karanga unataka kutafuna, umeona ndizi unataka kumeza, umeona miwa twende, umekutana na ice cream unataka unyonye mzee baba, siyo kwamba vitakugharimu pesa tu, vitakugharimu na afya yako na kumalizia pesa famasi na dispensari! Badili tabia uone kama hujapata cha kusevu ukafungua biashara ukatoboa hivi hivi halafu wajinga wakasema ni Freemanson!
5. **Hauna sababu ya kununua maji ya kunywa na wakati unaweza kuchemsha na kwenda nayo kazini.** Tumia mkoba wako kubeba maji ya kunywa kama unavyotumia mkoba huo kubeba kanga za kubadilisha njiani na viatu vya ziada. Beba kichupa cha maji kwenye begi lako la laptop, mbona K-Vant

inakaa? Ukifanya hivyo utapunguza matumizi na kupata cha kusevu, ukajipatia mtaji.

6. **Punguza matumizi ya umeme nyumbani kwako**. Usiache redio au televisheni vinawaka siku nzima hata kama hakuna wa kuvitumia. Viwashe pale unapovihitaji tu. Wageni wanapokutembelea msiendelee na mazungumzo huku redio na televisheni vinaongea. Vizime! Usiache laptop kwenye chaji na wakati huitumii. Lakini pia marufuku watu kuchaji simu zao wanapofika nyumbani kwako. Hii itakupunguzia gharama za umeme na kupata cha kusevu ukaanzishe biashara uache kulalamika. Fanya haya tu kama unataka mtaji!
7. **Acha kufungulia maji kwa kasi kubwa kwa sababu mengi yanapotea na lazima uyalipie**. Usiruhusu mabomba kuvujisha hata tone kwa sasa kidogokidogo huongeza bili ya maji. Kwa wale wanaotumia bombamvua kuoga jifunze kuoga fasta. Hakikisha wakati unapaka sabuni na kujisugua bomba limefungwa. Hakikisha hakuna maji yanayopotea ili bili ipungue upate za kusevu kwa ajili ya mtaji.
8. **Tumia kwa uangalifu sabuni za kufulia na kuogea pia**. Usiache sabuni kwenye maji muda mrefu itaisha bure na kuingia gharama ya kununua nyingine kwa hela ambayo ungesevu kudunduliza mtaji. Sijui unanielewa?
9. **Acha kupiga simu zisizokuwa na ulazima**. Usitumie simu kupiga stori. Hata unapojiunga na vifurushi vya siku, wiki na hata mwezi fanya hivyo pale tu utakapoona kuna ulazima. Kujiunga na vifurushi usivyovihitaji utajikuta kufanya mawasiliano usiyoyahitaji na kuwapotezea watu muda. Bando za ofa ndo huwapa jeuri watu kupiga majungu. Haya ni matumizi mabaya ya rasilimali ambayo mwisho wa siku yanakugharimu fedha na kujikuta hauna cha kusevu.

10. **Acha mizunguko yote isiyokuwa ya lazima kwa wale wanaotumia magari**. Tumia hata daladala kwenda sehemu inayofikika ili ile pesa ya mafuta usevu kwa ajili ya mtaji. Acha kupanda bodaboda, taxi au bajaji kwa umbali unaoweza kutembea kwa mguu ili upate cha kusevu. Halafu mbali na kusevu, kutembea kwa mguu ni sehemu ya mazoezi ya mwili. Mazoezi yatakuepusha na magonjwa ambayo yangekugharimu pesa kwa ajili ya tiba.
11. **Siyo lazima uwe na aina 10 za pafyumu, aina saba za losheni**, aina sabini za lipsticks, pea 1,000 za viatu na mikoba ya rangi zote. Huu ni ufahari wa bongo movie ambao mwisho wa siku unakugharimu wewe! Ikikupendeza acha ili upate za kusevu upate mtaji!
12. **Kabla ya kulipa bili yoyote jiridhishe, ukiona mahesabu hayaji vizuri, uliza.** Usilipie kitu ambacho hujatumia kwa uhalali. Jenga tabia ya ubishi kama waha linapokuja suala la kulipia kitu. Usisite kuomba punguzo la bei hata kama ni supermarket na fixed bei zao, kuwa mbishi. Usiache chenji hata senti tano. Kidogo kidogo hujaza ndoo! Lakini pia badala ya kulipia channels 150 kwenye king'amuzi lipia channels unazoangalia tu.
13. **Acha kabisa tabia ya keep change popote pale unategemea kusifiwa kwa sababu sifa inaua!** Dai chenji hata kama ni buku! Milioni moja bila buku inapoteza hadhi ya kuwa milioni moja! Hakuna pesa ndogo chini ya jua, mie ndo maana vitabu vyangu nauza buku jero tu!
14. Unapoamua kumtoa mchumba wako dina akaja na shost zake usijifanye kidume ukaumia kwa sababu ya ufahari, badala yake waulize wamekuja kula kwa bill ya nani! Wakisema ni yao waambie **samahani sina huo uwezo**. **Mie siyo Yesu! Nina bajeti ya mtu mmoja.** Be open kuliko kuwatukana

kimoyomoyo! Ukitoka out na mtu mwambie kuwa kila mtu atajilipia bili yake. Hapo lazima upate za kusevu ufungue biashara uitakayo.

15. **Usihonge wala kununua machangudoa!** Wahongwaji hawana shukurani brother. Halafu huko kwenye kuhonga risk ni nyingi sana. Kuna magonjwa ambayo yatavuruga bajeti yako. Lakini pia kuna kugonganishwa na kufedheheka mjini bure! Sibora uachane na hiyo business upate za kuanzisha biashara?
16. **Usitupe vyakula vinavyobaki badala yake kadiria chakula cha kuwatosha**. Asiyemaliza chakula wakati mwingine apewe kidogo. Ukifanya hivyo walahi lazima upate cha kusevu na kufungua biashara upunguze kelele!
17. **Kwa nini ukanywe bia ya shilingi 10,000 na wakati bia hiyohiyo inauzwa kwa shilingi 2,500 pale Tupendane Baa?** Ufahari utakunyonga! Ni kweli unapokwenda kunywea au kula sehemu zenye hadhi unakutana na watu wenye hadhi mkabadilisha mawazo ukatoka kimaisha. Nakushauri fanya hivyo kama una hadhi ili uongeze hadhi!
18. **Punguza idadi ya sherehe za kuchangia kwa mwaka**. Usijifanye wewe ni mwema na tajiri wa kuchangia kila kadi ya harusi unayoletewa na wakati unaishi kwenye nyumba ya kupanga. Ukizoea ufahari utajikuta ukikopa ili kupata ufahari na kumlilia Mungu kwamba maisha ni magumu. Maisha siyo magumu wewe ndo mgumu. Acha hayo uone kama hujapata mtaji!
19. **Kama hujajenga nyumba yako na unahitaji kupanga**, basi panga karibu na unakofanyia kazi au kibarua chako, hii itakusaidia ili ukate gharama za usafiri. Usitake kuishi kwenye nyumba yenye vigezo unavyovitaka ukaumia kwenye nauli!  Life is how you make it wanasemaga wazungu.

20. **Usipende kuazima kitu cha mtu kikipata tatizo huna namna zaidi ya kulipa wakati ambao hauna hiyo bajeti**. Cha mtu mavi walisema wahuni wa mjini, wasiolala njaa lakini wanachelewa kula!
21. **Usisahau kuabudu na kumtolea Mungu Zaka na Sadaka kwa sababu imeandikwa heri kutoa kuliko kupokea**. Ukifanya hivyo Mungu atailinda mifuko yako hata ukiweka pesa zitadumu na mwisho wa siku utapata cha kusevu! Mpaka hapo hujapata mtaji tu? Labda kichwa ngumu!

**Sura ya 4**

# Imani Pasipo Kuhoji ni Ushirikina!

Imani ni kitu kizuri maana kwa imani unaweza kuhamisha milima, lakini imani inakuwa na maana ikitanguliwa na reasoning! Reasoning ni kuhoji kwa kutumia akili ya juu, Socrates anaita upper head! Ukianza kuamini kwanza halafu ndo ukahoji baadaye matokeo yake yatakushangaza kama watia nia wa CCM walivyoshangazwa na wajumbe kwenye kura za maoni. Wajumbe waliposema **tuko nyuma yenu**, **watia nia wakaamini** bila kuhoji, walivyogeuka nyuma hawapo, nikayakumbuka yale maneno ya Bw Yesu, "Si kila aniambiaye, 'Bwana, Bwana', ataingia katika ufalme wa Mbinguni." Faith without reason is superstition alisema Baba Mtakatifu wa Papa Leo XIII mwaka 1879 akimaanisha kwamba imani pasipo kuhoji ni ushirikina.

Amekwambia ukimzalia mtoto atakuoa, hoji kabla hujazaa ukaachwa solemba na mtoto wako ukaitwa single mother! Amekwambia ukimsomesha hatakuacha, hoji kabla hujamsomesha, akakuacha ukajinyonga. Wamekwambia limbwata inaweza kumtuliza mumeo nyumbani, akaacha kupoteza pesa kwa michepuko mkajenga, hoji kabla ya kumlisha limbwata akawa zuzu mkafa njaa! Umeambiwa kilimo cha matikiti kinalipa, kwamba ukiwekeza laki mbili utapata milioni kumi, hoji kabla hujalima matikiti ukaja kuyala mwenyewe! Umeambiwa ukilala na binti yako utapata utajiri, hoji kabla

hujaingiza laana kwenye ukoo wenu, mkawa watu wakuzaa wabakaji tu.

Ukienenda kwa imani pasipo kuhoji unaweza kula kinyesi cha mbuzi ili upone kisukari kwa sababu tu umeambiwa hivyo. Kenya kuna watu wanaamini kutembea na msichana bikra ni dawa ya ukimwi na wakati Afrika Kusini wanaamini kuoga mara baada ya tendo la ndoa ni kinga ya ukimwi, ndo maana Rais Jacob Zuma alipoulizwa kwa nini hakuwa na mashaka kubaka mwanamke mwenye virusi vya ukimwi, alijibu ati alikwenda kuoga baada ya kile kitendo." Imani pasipo kuhoji ni kipimo kizuri cha ujinga alionao mtu!

Amewambia mkimchagua kila mtu atakuwa huru kukosoa kila kitu, hoji kabla ya kumchagua isijekula kwenu kwa sababu Afrika mke hakosolewi sebuleni, anakosolewa chumbani, kama huamini jaribu! Ukitaka kujua hakuna mwanaume dhaifu mnase kibao mbele ya mke wake! Wahenga waliposema akili za kuambiwa changanya na za kwako walimaanisha tusikubali kuishi kwa imani tu badala yake tuishi kwa imani na reasoning. Tusiishi kwa fikra za Ndiyo Mzee!

Ukiingia kwenye imani yoyote ile na akili za kuku kukimbilia punje mahindi utanaswa na mrusha punje. Imani zingine ni sumu ya maendeleo tuwe makini nazo. Hoji kwanza, halafu amini. Galileo Galilei aliwahi kusema kama Mungu ndo alitupa uwezo wa kuhoji kwa nini tusiutumie? Galileo aliwauliza hivyo wakuu wa dini waliomtia ndani kwa kuhoji kwa nini Biblia inasema Jua linazunguka na wakati halizunguki, wakamwambia anapingana na neno la Mungu! Huna adabu. Kwenye reasoning hakuna cha adabu.

Ukiambiwa kumchinja mtu ni thawabu kwa Mungu, hoji kabla ya kuangukia kwenye dhambi ya mauaji. Ni Mungu gani anayewapokea wauaji? Yaani uingie Mbinguni kwa kuua? Kuna video nyingi huko mitandaoni huwa zinaonyesha jinsi watu wanavyochinjwa kwa jina la imani. Anavutwa mtoto wa watu, anapigishwa magoti, mikono inashika chini na kutengeneza umbo la mbuzi, au tuseme ng'ombe, then ana kuja mtu mwenye kisu kirefu na kikali sana, anapiga maramoja, fyaaa kichwa kinadondokea shimoni, damu inamwagika, mwili unavutwa na kulundikwa walipo wafu wanzake, muuaji anamshukuru Mungu kwa kuua. Loh! Hii ni imani haribufu!

Tuishi kwa imani baada ya kuhoji. Ukihoji utapata majibu mengi yatakayokuongoza kufanya maamuzi sahihi. Umeambiwa viungo vya binadamu ni dili kwenye biashara hoji kabla hujafanya mambo ya hovyo. Mwaka 2013 Mtandao wa Global Publisher uliwahi kutoa taarifa za watu waliofanya mambo ya hovyo kabisa. Soma mwenye, "Hivi karibuni mapaparazi makini walipata bahati ya kupokelewa na mfanyakazi wa mochwari ambapo baada ya salamu walijitambulisha kwa majina ya bandia. Walisema wao ni wafanyabiashara wa samaki tokea Mwanza na wanataka viungo vya wanadamu vilivyopo mochwari hapo. Waliambiwa kuna mikono na sehemu za siri za kiume, kama wako tayari wanaweza kuuziwa. Bei ni shilingi milioni moja mpaka laki mbili kutegemea na ukubwa wa kiungo chenyewe. Ili kudhihirisha hilo, mfanyakazi huyo alikwenda kutoa 'sampo' ya viungo hivyo na kuambiwa kama wapo tayari watoe mkwanja biashara ifanyike mara moja". Unaona hiyo michezo?

Katika Dunia ya leo matapeli ni wengi, ukienenda kwa imani utaibiwa kuanzia mitandaaoni hadi kwenye nyumba za ibada na ukicheza watakuua kabisa. Kibwetere wa Uganda aliua wafuasi wake kwa sababu aliwaambia mwisho wa dunia umefika na wao bila kuhoji wakaamini, wakaliwa kichwa. Issue yenyewe ilikuwa hivi. Huyu Kibwetere alikuwa na kanisa lake nchini Uganda, sasa mwaka 2000 aliwatangazia waumini wake kwamba ndo mwisho wa dunia hivyo wakaanza maandalizi ya kunyakuliwa. Waumini wake wakauza mali zao, wengine wakaacha kazi, wengine wakasalimisha hati za nyumba na mashamba, pesa za mauzo ya mifugo, mishahara ya mwisho wa mwezi kama sadaka, wakatubu dhambi zao tayari kwa safari ya Mbingu. Iliofika 1 Januari 2000 wakashangaa Dunia bado ipo. Akili ikawarudi kidogo. Baadhi yao walicharuka kudai fedha na mali zao walizokabidhi.

Baada ya Kibwetere kubanwa sana, ghafla alitangaza kuwa amepokea maono kuwa Machi 17, 2000 ndiyo mwisho wa dunia. Kanisa likaandaa bonge la pati ya kuagana kwenda Mbinguni. Watu waliserebuka pasipo kujua ya nyuma ya pazia. Siku ya tukio la mwisho wa Dunia, kanisa lilichomwa moto watu wakiwa ndani yake, madirisha na milango imefungwa hakuna mtu kutoka. Zaidi ya watu 500 waliteketea kwa moto. Kibwetere akapotelea kusiko julikana, wengine wakasema alichomeka na yeye, wengine wakasema alikimbilia Malawi.

Mungu alitupa akili ili zitusaidie kuishi vizuri, kutozitumia ni dhambi kwa Mungu baba na kama unavyojua mshahara wa dhambi ni mauti. Jamani tutumieni akili zetu vizuri, tuacheni kuenenda kwa imani tu pasipokuhoji tukaangamia kizembe.

Imani pasipo kuhoji huvuruga amani ya nchi, inavuruga utaratibu wa maisha ya watu, inavuruga kila kitu. Unamuuliza mswahili, wewe utamchagua nani? Badala ajibu swali na yeye anakuuliza swali. "Je. Unaweza kumkataa baba yako kwa sababu ya baba wa kambo? Hii ni imani. Wakati mwingine baba anaposhindwa kutekeleza majukumu yake kuna ubaya gani kuacha kumuita baba?

Kuna vijana hadi leo wanaamini Tanzania kikiwaka nchi itakuwa sawa, jamani kabla ya kukinukisha jipeni muda wa kuhoji. Ukijipa muda wa kuhoji utagundua vita vikianza haviishi. Kongo ni mfano mzuri, ni miaka zaidi 60 sasa tangu wakinukishe hakijazima. Sudani, Chad, Burundi, Uganda na nchi nyingine kama hizo bado watu wanaishi roho juu. Rwanda pamoja na kupiga maendeleo kishenzi bado wanaishi roho juu wakati Tanzania amani siyo ajenda kabisa. Ukijisumbua kuhoji utagundua vita ni mtaji wa nchi zinazouza silaha. Sasa watafanya kila wawezalo vita zisiishe. Usiombe vita. Ukihoji zaidi na zaidi utagundua vita hutafuna watu wa chini, wakubwa huwa wanakwenda kuishi vizuri uhamishoni.

Unaambiwa hirizi ni kinga ya biashara na mali zako, hoji kabla ya kuvaa hirizi mwili mzima ukidhani ni kinga. Siku ikidondoka mbele za watu utajiharibia sifa kama yule binti aliyekatikiwa na shanga zikasambaa wakati wa kusifu na kuabudu kanisani. Shanga siyo mbaya. Lakini na nyie waganga Mungu anawaona. Unakuta kwenye hirizi pengine kaweka karanga za kukaanga ambazo hazina uhusiano kabisa na maendeleo yako.

## Sura ya 5

# Wekeza Ovyo Uwe Msema Ovyo

Unachukua mkopo benki ili uanzishe biashara, unakwenda kuponda mali kufa kwaja lakini kufa hufi, Mungu anakupa afaya njema ili ukalipe kwanza vya watu, unashindwa kulipa mkopo, biashara huna, watu wa benki wanauza nyumba yako uliyoweka dhamana, unaanza kusema ovyo kuhusu benki kudai haki yao, "mabenki ya siku hizi hayana utu." Wewe ndo huna utu! Acha kuharibu biashara za watu, pambana na hali yako!

Wazazi wako wameuza shamba ili uende shule, badala ya kusoma unawaka tamaa ya mwili, unabeba mimba, boyfriend anakunyima pesa ya kutoa mimba, mwalimu wa nidhamu anabaini una ujauzito, unasomewa sheria za kufukuzwa shule, sheria ambazo uliapa kuzifuata wakati unaanza shule, unafukuzwa shule, unaanza kusema ovyo kwamba mwalimu wa nidhamu ana roho mbaya na wakati wewe ndio una roho mbaya.

Unaanzisha kilimo na ufugaji, unazalisha mazao kwa wingi, unakosa soko, unaanza kusema ovyo kuhusu serikali kushindwa kukutafutia soko. Kuanza shughuli ya kilimo bila kujua soko litatoka wapi ni kuwekeza ovyo. Sikiliza hata serikali nazo ziko busy kuhakikisha wenye mamlaka wanakula vizuri, wanalala pazuri, wanasafiri pazuri kwa jina la kuwasaidia walala hoi.

Unamsomesha mchumba, anapata kazi na kuolewa na watu wenye hadhi yake halafu unaanza kusema hovyo kuhusu wanawake wote kumbe wewe ndo hovyo kusomesha mchumba na wakati mchumba hasomeshwi! Unapoamua kusomesha mchumba hakikisha future yako inasoma na hiyo ndo maana ya kuendana. Hakuna mwanamke anayeingia kwenye ndoa bila kujihakikishia usalama wake, ukimkuta huko basi ujue yamemkuta safarini tu! Hawa watu wanaangalia future ya mwanaume! Ndo maana mwanamke hata kama ulikuwa jambazi huko nyuma, kama future yako inasoma yuko tayari kuambatana na wewe! Tafuta pesa malaika wako ainjoy kumbuka hakuna malaika anayeishi jehanamu!

Unaendesha gari, sheria za barabarani zimewekwa, hutakiwi kwenda zaidi ya spidi 50 kwa saa katika sehemu zenye makazi ya watu, hospitali na mbuga za wanyama, wewe unakwenda spidi 100, trafiki anakupita tochi, unaanza kusema ovyo kuhusu trafiki, yaani trafiki anakuwa mbaya kwa kutekeleza wajibu wake. Ama kweli akutukanaye hakuchagulii tusi.

Waandishi wa habari wamekufuata ofisini kwako, wanakuomba uongee chochote kuhusu tuhuma zako za kutoa ajira kwa kuwalala watoto wa watu, unawatimua kwamba hufanyi kazi na magazeti kwa sababu yanaandikwa na wavivu wa kufikiri, wakiyamwaga kwenye vyombo vya habari na dunia kukushangaa kwa ushenzi unaanza kusema ovyo kuhusu waandishi wa habari.
Kipindi cha uchaguzi wanakuja wagombe waungwana na washenzi, kwa hongo ya tisheti, kofia na pombe mnachagua viongozi washenzi, wanawatenda halafu mnaanza kusema hovyo ati siasa ni mchezo mchafu! Hivi hapa nani mchafu kati ya aliyechagua uchafu na uchafu wenyewe?

Serikali imekuheshimu, imekupa dhamana ya kuwahudumia wanyonge, unatumia cheo kuwaumiza wanyonge, unatumbuliwa ukafie mbele, ukifika huko ulikokwenda kufia unaanza kusema hovyo kuhusu serikali kwamba imekuonea, ni uvunjaji wa haki za binadamu! Yaani wewe kuwashughulikia wanyonge ni haki za binadamu, lakini serikali kukushughulikia wewe ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

Umeajiriwa kwa mbinde, badala ya kuchapa kazi unachagua kuchat na kila mtu, kazi zinalala, unaitia hasara taasisi, unafukuzwa kazi, unaanza kusema ovyo kuhusu mwajiri wako. Kosa siyo mwajiri. Kosa ni wewe kuwekeza hovyo kwenye chatting. Maneno yako ya hovyo hayatakusaidia. Umeyakoroga yanywe mwanangu!

Nchi yetu imejaa wasema ovyo. Vijana kwa wazee, wasomi kwa wasiosoma, wanawake kwa wanaume wanasema ovyo. Kusema ovyo ni matokeo ya kuwekeza ovyo.

Unaingia kwenye kinyang'anyiro cha ubunge kwa lengo la kuteuliwa kwenye nafasi nyingine badala ya kupambana upate ubunge halafu usipoteuliwa ukurugenzi, udc, na udas unaanza kusema hovyo kuhusu chama na serikali na wakati ni uwekezaji wako wa hovyo!

Maisha ni kupambana na siyo kuzengea, maisha ni kupatia na siyo kubahatisha. Kuchukua fomu ya ubunge kwa lengo la kuteuliwa ni sawa na kuishi kwa kupiga ramli, matokeo ya kija vibaya lazima uwe msema hovyo! Amka brother, heshima yako mtaani ni kubwa, wekeza vizuri ili usijekuwa msema hovyo!

Mke wako anapata ujauzito, inafika siku ya kujifungua, huna hata shilingi mfukoni unapiga simu kwa rafiki zako wakutoe pesa ya nauli umkimbize shemeji yao hospitali, rafiki zako wanakunyima, unaanza kusema ovyo kuhusu rafiki zako kana kwamba ujauzito ni tukio la ghafla. Hapa tatizo ni kuwekeza hovyo kwa sababu hakuna mimba ya ghafla!

Unaingia kwenye ndoa kichwa kichwa, ndoa inakubinua, unabinuka chali cha mende ndembendembe halafu unaanza kuongea ovyo kuhusu ndoa kwamba ndoa ni gereza unalolala kitanda kimoja na adui yako, ati ndoa ni jela tafuta mfungwa wa kufanana naye na wakati ndoa ni mpango wa Mungu kwa watu wote! Ona sasa kwa sababu yako msema hovyo kuhusu ndoa, vijana siku hizi wanaogopa kuingia kwenye ndoa na wale wanaojitoa muhanga kuingiemo, wanaingia kupambana badala ya kuenjoy!

Ukiingia kwenye ndoa na mawazo ya kuua utaua, ukiingia kwenye ndoa na mawazo ya kunyongwa utanyongwa, ukiingia kwenye ndoa na mawazo ya kuachika utaachika kwa sababu unavyowaza ndiyo unavyokuwa. Kwani hiyo nyumba unayojenga kwenu bila mumeo kujua si maandalizi ya kuachika? Hilo gari ulilomnunulia huyo mwanamke siku mkeo wako akijua akakufanyizia si ndo utaanza kuongea hovyo ati wanawake wote ni umbwa kumbe wewe ndo mbwa kwa sababu ya uwekezaji wako wa hovyo?

## *Sura ya* 6

# Chuki ni Sawa na Kunywa Sumu Afe Usiyempenda!

Mwalimu mmoja aliwaagiza wanafunzi wake kila mmoja aje na nyanya kulingana na idadi ya watu anaowachukia. **"Nyanya hizo mtazibeba kwenye mabegi yenu ya madaftari,"** alisisitiza mwalimu. Kweli kesho yake wanafunzi wakazibeba zile nyanya vizuri kabisa, wengine walibeba moja, wengine mbili na wengine nyingi sana. "**Kila mwanafunzi aandike majina ya watu anaowachukia kwenye nyanya alizobeba"** alisema Mwalimu. Baada ya kuzipa majina mwalimu aliwaambia kila mwanafunzi azirudishie nyanya zake kwenye begi lake halafu aziache humo humo ndani ya begi kila siku awe anakuja nazo shuleni na kurudi nazo nyumbani. Baada ya siku kadhaa wanafunzi wakaanza kulalamika hasa wale waliobeba nyanya nyingi kuwa nyanya ni nzito sana na zinatoa harufu mbaya na zinaharibu vitu vyao vizuri walivyoweka kwenye mabegi yao.

**Hivi ndivyo ilivyo mtu unapoubebesha moyo wake mzigo wa chuki.** Kitakachoumia siyo zile chuki bali ni moyo wake! Ndiyo maana Yesu anasisitiza sana msamaha maana anajua madhara ya kutosamehe, **"Kisha Petro akamwendea, Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba? Yesu akamwambia, Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini"** (MATHAYO 18:21-22). Wahenga walisema

ukilipatia tumbo lako chakula kibaya jiandae kucheza ngoma kutoka tumboni!

Safisha moyo kwa kusamehe wanaokukosea, maana msamaha ni moja ya virutubisho vya moyo wako.Kusamehe ni kujipenda. **Hata Mungu asingewasamehe wenye dhambi mbinguni pangekuwa wazi. Haijalishi meno yanaun'gata ulimi mara ngapi lakini bado vinanaishi pamoja**. Faida za kuishi pamoja ni nyingi kuliko kutengana. **Ulimi hauwezi kufurahia utamu wa nyama bila meno kutafuna.** Kumbe kabla ya kumchukia mtu na hata kumuona hafai jaribu kwanza kukumbuka utamu wake. **Wanasaikolojia wanasema unapochukizwa hesabu mpaka mara 15 kabla ya kufanya maamuzi, itakusaidia kuchelewesha hasira.** Ipo nguvu katika kusubiri. **Hii ni nukuu kutoka kwenye kitabu cha Maisha ni Kutafuta Si Kutafutana, uk 32, kama unakitaka changia 5,000 tu nikurushie kwa Mpesa 0753665484**

**Hata mti unapopitia katika msukosuko unapunguza matawi na siyo mizizi. Kosa moja haliachi mke** walisema wahenga. **La msingi tuvumiliane maana hata kwenye kiwanda cha sabuni kuna watu ni wachafu tu na kiwanda kinawavumilia. Siafu wakiingia ndani huchomi nyumba, unachoma siafu**. Kuna mfalme aliyekuwa akitumia mbwa kuwaadhibu watumwa wake wanapokosea. Siku moja mtumwa aliyemtumikia mfalme kwa miaka kumi alitoa wazo baya, mfalme akaamuru kutupwa katika banda la mbwa. Mtumwa alinung'unika na kusema, "**Nimekutumikia kwa miaka 10, na leo wanitenda hivi? Naomba unipe walau siku 10 kabla hujanitupa bandani!**" Mfalme akakubali. Katika siku hizo 10, mtumwa akamuomba mlinzi kuwahudumia mbwa hao wakali kwa kuwapa chakula,

kuwaogesha na kila aina ya faraja ambazo wanyama huhitaji. Siku 10 zilipokwisha, mfalme akaamuru mtumwa atupwe bandani kutumikia adhabu yake. Hilo likafanyika kwa haraka, lakini cha kushangaza mbwa walianza kulamba miguu ya mtumwa na si kumrarua kama ilivyotegemewa. Mfalme akastaajabu, akasema: **"Nini kimewasibu mbwa wangu?"** Mtumwa akajibu, **"Nimewahudumia mbwa hawa kwa siku 10 tu na hawajasahau fadhila zangu. Lakini wewe nimekutumikia miaka 10, umesahau yote kwa sababu ya kosa moja tu!"**Mfalme akatambua kosa lake na akaamuru mtumwa aachiwe huru.

Kamwe usiruhusu historia nzuri kufutika sababu ya jambo moja usilolipenda! Msamaha ni nguzo na msingi wa utulivu wa akili na uhai wa roho zetu. Moyo usiosamehe huuponza mwili. Binadamu asiyesamehe hana amani moyoni na wala hana urafiki na Mungu. Chuki ni sumu **inayodhuru na kuua**. Acha kujipa sumu, acha kujiumiza kwa kubeba mzigo wa chuki moyoni. Ndiyo maana Tony Robbins anasema, "**Msamaha ni zawadi unayojitunukia mwenyewe." "Unaposamehe ni kuonyesha kwamba unajipenda"** alisema Steve Maraboli. **"An eye for an eye will make the whole world blind"** alisema Mahatma Ghandi. Achezaye na tope humrukia.

Anayesamehe ndiye mshindi ni methali ya Kizulu. **Kufanya makosa ni jambo la kibinadamu, kusamahe ni jambo la kimungu.** William Shakespeare alisema, "**Tusitwishe mzigo mzito kumbukumbu zetu kwa jambo zito ambalo limepita."** Kununa kwetu hakubadili historia. Kukasirika kwetu hakubadili historia. Kulaani kwetu hakubadili historia. Kutukana kwetu hakubadili historia. Kusamehe kunabadili historia kwa sababu

hupunguza idadi ya watu wabaya. **Katika maisha yako usitafute kosa tafuta vema** alisema Henry Ford.

**Sura ya 7**

# Ulimi Unang'ata Zaidi ya Meno

Ulimi hauna mfupa lakini unaweza kuvunja moyo, ni bora kujikwaa kidole kuliko kujikwaa ulimi, ulimi ni kiungo legelege kinachoweza kuvunja ndoa imara, ulimi ni kama njiti ya kiberiti lakini unaweza kuteketeza msitu mnene ndio maana Mungu akatupa ulimi mmoja na masiko mawili ili tusikie sana na kuongea kidogo. Kasheshe ni pale mtu anaposikia sana ili ajibu badala ya kuelewa. Mtoto mmoja alimuuliza mjomba wake, "Eti Mjomba ukichanganya OMO na FOMA unaweza kupata povu?" Mjomba akajibu, "Ndio, lazima upate kwa kuwa zote ni sabuni za unga. Halafu mjomba akasema, "Siku nyingine usiwe unauliza maswali ya kipumbavu." Mtoto akamwambia mjomba majibu yako ndio yakipumbavu. Utapataje povu bila kuweka na maji? Ulimi ulimvua nguo mjomba mbele ya mtoto wa dada yake.

Msengenyaji mmoja alialikwa kwenye sherehe ya uimbaji. Bila kujua akamgeukia jamaa aliyekuwa karibu naye na kuanza kumsema mwanamke aliyekuwa anatumbuiza, "Ana sauti mbaya sana! Unamjua ni nani?" Yule jamaa akajibu, "Ndio namjua ni mke wangu." Msengenyaji akasema, "Sisemi juu ya sauti yake bali maneno anayoimba si mazuri. Nashangaa nani alitunga wimbo huo mbaya." Jamaa yule akajibu, "Ni mimi niliyetunga wimbo huo." Kuna watu walitakiwa kukatwa ndimi zao siku nyingi, sema watashindwa kula. Hebu tafuta kitabu cha Matatizo si Tatizo utakutana na visa kama hivi vya kutosha. Kimeandikwa na Padre Faustin Kaamugisha!

Mungu alijua ulimi ni soo ndo maana kauwekea vizuizi viwili. Kizuizi cha kwanza ni meno na cha pili ni lips ili usitoke kirahisi. Ulimi unaweza kulaani au kubariki, kuua au kuumba, kuharibu au kujenga. Wakati anateuliwa kuwa mwenyekiti wa chama Abeid Karume alitamka kwamba washenzi watamuua na kweli miaka minane baadaye wakamuua kama alivyobashiri kwa kinywa chake.

Kwa maana, Atakaye kupenda maisha, Na kuona siku njema, Auzuie ulimi wake usinene mabaya, Na midomo yake isiseme uongo imeandikwa katika 1: Peter 3:10. "Samaki anayefumbua mdomo wake hunaswa na ndoano ya mvuvi" alisema Nape Mnauye akaja kunaswa mwenyewe na kupoteza Uwaziri.  Jitahidi kufumba mdomo wako kwani kuna watu wana hamu ya kukutia ndoano wakunase. Ulimi ni kama wembe mkali, ukiushika vibaya unakuchana. Afadhali kuteleza sakafuni kuliko kuteleza kwa ulimi. Ulimi ni kiungo kinacho sababisha dhambi nyinyi zaidi ya kiungo chochote katika mwili wa binadamu. Unaweza kupokea simu ya "Honey I miss you" kutoka kwa demu wako akiwa juu ya kifua cha msela.

Anania na mke wake walipouza kiwanja walimdanganya Mungu wakaliwa vichwa. Petro akamwambia Anania, wewe hukumwambia uongo mwanadamu bali Mungu. Anania aliposikia maneno haya akaanguka chini na kufa vijana wakamzika fasta. Saa tatu baadaye mkewe Anania akaingia, naye hana habari ya mambo yaliyotokea. Petro akamwuliza, "Niambie, je, mliuza kiwanja kwa thamani hii?" Akajibu, "Ndiyo, tuliuza kwa thamani hiyo. Saa ile ile akaanguka chini miguuni mwake na kufa, wakamzika fasta kwa sababu dhambi haikupi muda, ukiikaribia tu inakulamba hapohapo. Isome Biblia hata kama huna mpango wa kwenda mbinguni, we isome tu. Inamafundisho mazuri!

Achungaye mdomo wake na ulimi wake, hujiepusha na matatizo mengi. Mwanamke mpumbavu alikuwa anapigwa kila siku na mumewe. Akaamua kwenda kuomba dawa kwa Padri. Padri akampatia chupa ya maji ya Baraka na kumwambia kila mumeo anapoingia, weka maji mdomoni. Mwanamke yule akafanya vile na hakupigwa tena. Maji yalipokwisha akaanza kutandikwa tena. Akarudi kwa Padri amuongezee dawa. Padri akamwambia ewe mwanamke mpumbavu ulimi wako ndo hukufanya utandikwe. Kuwa makini na ulimi wako. Mtu mpumbavu midomoni mwake uovu ni mtamu kama sukari, anauficha chini ya ulimi wake si maneno yangu ni maneno yake yeye aliye juu.

Watu wengi wameuawa kwa upanga, lakini ni wengi zaidi waliouawa kwa ulimi. Nani ataniwekea mlinzi mdomoni mwangu, na kuupiga mhuri wa busara, ili unizuie nisije nikakosa, ulimi wangu usije ukaniangamiza anauliza Sira mwana wa Mungu. Kitabu cha Sira kinapatikana katika Biblia ya Wakatoliki. Sijui kwa nini Biblia nyingine zinavitabu vichache na wakati imeandikwa usipunguze wala kuongeza neno. Haya mambo haya hayataki haraka maana unaweza kuharibu.

"Kama mtu akijiona kuwa ni mtu mwenye dini, lakini hawezi kuutawala ulimi wake, dini yake haifai kitu, na anajidanganya mwenyewe" yanasema maneno ya Mungu katika Yakobo 1:26. Haya sasa wale mnaowasengenya mpaka watumishi wa Mungu kisa umetangaziwa mchango wa kununua gari la mchungaji. Kama huna hela siuziue tu kuliko kujiongezea laana juu ya laana? Maana hapo ulipo umeishalaaniwa weee mpaka Mungu anakushangaa na shetani anakucheka.

Unasengenya watu kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi, halafu Jumapili unawahi ibadani na kiherehere chako hadi madhabahuni utadhani msaidizi wa Yesu! Acha kumchezea Mungu wewe, ataukata ulimi wako na kuwatupia ndege wautafunee, ohooo! Ulimi ni kama moto, kaa nao mbali usikubanike kama nyama ya

mbuzi. Ulimi hauna adabu,unaweza kukudhalilisha mbele za watu ukaonekana hopeless guy na wakati tulikuamini sana!

Jamaa mmoja kwenye daladala baada ya kuona binti mzuri aliwaka tamaa na kuanza harakati za kumpata binti yule mrembo. Akachukua simu yake na kuanza kupiga kwa uongo, "Hello Mr. Supervisor, nitachalewa kidogo kwa sababu kuna mahali nitapitia, so nipelekee tu hiyo Ferrari yangu nyumbani". Mrembo akamuangalia kijana yule kwa jicho la mwisho wa mwezi basi kijana akajua tayari kafanikisha lengo lake, kisha akaropoka , "Niaje mrembo", mrembo akamkazia macho kisha akamwambia," Shika beteri yako ya simu uliangusha wakati ukitoa simu mfukoni". Jamaa aliamua kushuka kwenye daladala kabla hajafika, halafu ni daladala za Mbagala kupata siti lazima utoke jasho.

Daktari alipigiwa simu aende hospitali. Alipofika hospitali alikuta baba wa mtoto amepaniki ,"Hivi kwa nini nyie madaktari hamkai kazini? Kwa nini umechelewa? Hufahamu kama maisha ya mtoto wangu yapo hatarini? Daktari alitabasamu na kusema, "Samahani sana, sikuwa karibu na hospitali na nimejitahidi kuja kwa haraka sana baada ya kupokea simu, nakuomba upunguze hasira ili nifanye shughuli yangu." "Unasemaje? Nipunguze hasira?" Baba aling'aka."Hivi angekuwa mwanao ungepunguza hasira? " Daktari akajibu,"Sisi madaktari tunatibu tu, uponyaji ni kazi ya Mungu, katulie umuombe Mungu wako Mzee." "Ushauri mwingine ni wa kijinga kweli, eti nikatulie" aliendelea kufoka mzee.

Upasuaji ulimalizika ,"Asante Mungu! Mtoto wako amepona!" Kama una swali lolote utamuuliza nesi" Daktari akaondoka zake mbioo!

Baba akamgemkia nesi, "Huyu daktari mkorofi kweli, yaani hawezi hata kusubiri kidogo nimuulize maendeleo ya

mwanangu?” Nesi akamjibu, huku akitokwa na machozi, “Mtoto wake alifariki jana kwa ajali ya gari, wakati tunampigia simu aje kumtibu mwanao alikuwa kwenye mazishi ya mtoto wake. Amefanikiwa kuyaokoa maisha ya mtoto wako, kwa hiyo ameenda kuendelea na mazishi ya mtoto wake.” Wahenga walisema ongea na akili yako kwanza kabla ya kuongea na ulimi wako! Ulimi unaumiza nyie, acheni tu.

Tumrudie Mungu vinginevyo ndimi zetu zitatumaliza. Mtoto aliuliza, "Hivi Mungu ni mkubwa kama nini? Baba akajibu, “Inua kichwa angani kisha niambie ile ndege ni kubwa kiasi. Mtoto akajibu ni kadogo sana. Kisha ndege ilipotua baba alisema, “Haya niambie hapa hii ndege inaukubwa gani? Mtoto akasema hapa ni kubwa mno, kuliko ilivyokuwa angani. Ndipo baba yake akasema ukubwa wa ndege uliyoiona angani na hii unayoiona hapa chini ni sawa isipokuwa umbali wa ndege uliyoiona angani ndoo umesababisha ionekane ni ndogo ukilinganisha na hii iliyopo karibu yako. Ndivyo ukubwa wa Mungu ulivyo. Mungu ni mdogo sana pale unapokuwa mbali naye, ila huwa ni mkubwa pale unapokuwa karibu naye sana.

Ulimi na ubongo vikikosa mashirikiano utajikuta ni mtu wa kuongea kila wakati, kujibu kila anachokisikia, kulalamikia kila jambo, kukisemea kila unachokiona na wakati imeandikwa kuna wakati wa kunyamaza na wakati wa kusema Mhubiri 3:7b. Yapo mambo ambayo tunapaswa kunyamaza kwa ajili ya usalama wetu na usalama wa wengine. Hata mjinga akinyamaza huhesabiwa maarifa anasema Mungu kupitia Mithali 17:28. Ndiyo maana inashauriwa:

1. Usiongee kuhusu utajiri wako mbele ya maskini kwa sababu wataona kama unawananga tu.

2. Usiongee kuhusu afya yako mbele ya wagonjwa kwa sababu wataona kama unajidaia afya uliyonayo.

3. Usiongee furaha yako mbele ya mwenye huzuni maana atajiskia vibaya.

4. Usiongee kuhusu wazazi wako mbele ya yatima maana utawatonesha vidonda vilivyoanza kupona.

5. Usiongee kuhusu mumeo mbele ya wajane maana wataomba nawe mumeo afe.

6. Usiongee kuhusu watoto wako mbele ya mtu tasa utasababisha ajione hana thamani mbele za watu.

Kumbuka ulimi huponza kichwa, usipotia neno hutopatwa na neno walisema Waswahili wa Pwani. Abigaili alipomuona mume wake amelewa alichagua kunyamaza, pengine angetandikwa makofi kama yule mama aliyepewa dawa na Padri. Soma 1 Samweli 25:36-38.

Ni kweli kuna wakati unasemwa vibaya, unasingiziwa mambo, unatukanwa, unaonewa, unachafuliwa lakini kumbuka uzushi huanzishwa na wenye chuki, kusambazwa na wajinga, na kukubaliwa na wapumbavu.

Muhubiri mmoja alitoa noti ya elfu kumi na kuuliza, "Noti hii inathamani gani?" Waumini wakajibu "elfu kumiiiii". Vema kabisa alisema Mtumishi. Akaichukua ile noti akaifinyangafinyanga na kuuliza tena noti hii inathamani ya shilingi ngapi? "Elfu kumiiiiiii" Vizuri sana. Akaitupa chini, akaikanyagakanyaga na kuuliza tena noti hii ina thamani gani? "Elfu kumiiiii" waumini walijibu vilevile.

Mtumishi akasema, katika maisha kuna kipindi utasalitiwa, utakanyagwa, utaonewa, utatukanwa, utachekwa, utapuuzwa lakini kumbuka thamani yako itabaki palepale labda uamue

mwenyewe kuiharibu; na unaweza kuiharibu kwa kujibu makombora kwa matusi. Usikubali ulimi wako ukaharibu thamani yako chagua kunyamaza.

Ukiwa na hasira katu usitegemee kuwa utajadiliana na mtu kwa hekima. Ukiongea utaongea kwa hasira, ukijibu utajibu kwa hasira, kwa ajili ya hayo mwenye busara atanyamaza kimya wakati kama huo; kwa kuwa ni wakati mbaya. Kumbuka hasira ni hasara. Soma Waefeso 4: 26. Wahenga wanasema, "The smarter you get the less you speak". Akushindaye kuongea, mshinde kunyamaza. Koini siku zote hupiga kelele, noti haipigi kelele, maana yake ni kwamba thamani yako inavyozidi kuwa kubwa ndivyo unavyotakiwa kuwa mkimya na mpole. Nasema uwe mpole na siyo mjinga.

Jifunze kuzuia ulimi wako usinene mabaya. Mtume Petro anasema kama unapenda maisha na kuona siku njema, uuzuie ulimi wako kunena mabaya, na midomo yako isiongee hila kabisa, soma mwenyewe 1:Petro 3:10. Jenga hoja usikike na siyo kupaza sauti. Chunga sana ulimi wako usinene mabaya juu ya wengine kwani kufanya hivyo ni sawa na kutema mate juu, lazima yakurudie. Katika Mithali 13:3 neno linasema 'Yeye alindaye kinywa chake hulinda nafsi yake, bali afunuaye midomo yake atapata uharibifu'. Katika Mithali 21:23 tunasoma hivi, 'Mtu azuiaye kinywa chake na ulimi wake, atajilinda nafsi yake na taabu'.

Jifunze kuwa mtu wa maneno machache maana katika wingi wa maneno hapakosi kuwa na maovu; bali yeye azuiaye midomo yake hufanya akili, na maneno ya hekima kutoka Mithali 10:19. Avoid too much talking. Iweni wepesi wa kusikia na si wepesi wa kusema Yakobo 1:19 ndo maana mmepewa mdomo mmoja na masikio mawili. Kuna watu wengi haki zao zimeibiwa, wengine wamefungwa, wamepoteza kazi zao, wapendwa wao kwa sababu ya matumizi mabaya ya ulimi.

Mungu kasema kweli kuhusu ulimi. Hebu cheki.

1. Mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi; na wao waupendao watakula matunda yake' Mithali 18:21.

2. Maana twajikwaa sisi sote katika mambo mengi. Mtu asiyejikwaa katika kunena, huyo ni mtu mkamilifu, awezaye kuuzuia na mwili wake wote kama kwa lijamu' (Yakobo 3:2).

3. Ulimi wako watunga madhara, kama wembe mkali, ewe mwenye hila umependa mabaya kuliko mema, na uongo kuliko kusema kweli. Umependa maneno yote ya kupoteza watu, Ewe ulimi wenye hila (Zaburi 52:2-4).

4. Koo lao ni kaburi wazi, kwa ndimi zao wametumia hila. Sumu ya fira i chini ya midomo yao. Vinywa vyao vimejaa laana na uchungu' Naam ole wako ulimi unaokazana kutunga hila, kuachilia laana, kusema uongo na kupoteza watu, maana mabaya yaliyopandwa yatakurudia (Warumi 3:13-14).

Wenye hekima wamejaaliwa midomo midogo na masikio makubwa ili wasikie sana na kusema kidogo! Hekima ni Mungu, upumbavu ni shetani!

# Sura ya 8

# Kauli 10 Hatari Katika Ujasiriamali

Tangu ajira zianze kuzingua, ujasiriamali ndo umekuwa swaga ya mujini kama asemavyo Pedeshee Ndama mtoto ya Nyau. Watu hawana mpango wa kuajiriwa kivileee. Hata walioajiriwa siku hizi wanaganga njaa kupitia ujasiriamali. Binafsi naposikia hivi nafurahi sana kwa sababu ujasiriamali na uwekezaji ni mpango wa Mungu mwenyewe aliofutundisha kupitia wale watumwa watatu na talanta. Kumbe afanyaye ujasiriamali ni mwenye akili mbele za Mungu. Yule mtumwa aliyepewa talanta na Bwana Yesu halafu akaiweka kwenye kibubu badala ya kuizungusha ili izae, Yesu alimuita mjinga, lakini wale waliozungusha talanta zao na kuzaa faida aliwaita majembe!

Pamoja na kwamba ujasiriamali umekuwa swaga ya mujini wengi bado wanachemka, wanaanzisha ujasiriamali na gia ya kushindwa. Lakini kwa kuwa akili ni nywele, nimezitumia kutafuta wapi tunakwama. Nikagundua midomo ndo issue. Tunatema sumu badala ya kutema cheche. Mgonjwa alimuuliza daktari, "Je, tangu uanze kufanya operasheni ya kichwa umeishaua wagonjwa wangapi?" Daktari akajibu "Mmoja." "Je, na mimi leo ni mgonjwa wa ngapi kufanyiwa oparesheni na wewe?" Aliuliza mgonjwa. "Wewe ni wa pili," alijibu Daktari. Mgonjwa akafa! Kilichomuua mgonjwa siyo oparesheni, ni kauli ya Daktari!

Kauli zinaweza kuumba au kuua, kubariki au kulaani, kuangusha au kuamsha. Mungu aliumba Mbingu na Nchi kwa kutamka tu. Na Iwe Nuru; Ikawa, na Liwe Anga Likawa, na Tumfanye mtu

kwa sura na mfano wetu, mtu mke na mume akawaumba kwa siku moja. Kwahiyo habari za kusema kati ya me na ke nani alianza kuumbwa, jibu ni kwamba waliumbwa wote siku moja. Zile habari za mwanamke kutoka ubavuni ni lugha ya picha ikimaanisha ndoa. Maana ukisema Eva aliumbwa baadaye ina maana Mungu alimsahau. Yaani Mungu akumbuke kuumba wanyama ke na me asahau kwa mwanadamu? Usipokuwa na utulivu wa akili usomapo Biblia utajikuta ukimkosoa Mungu na kulaaniwa hivihivi na wakati imeandikwa Mungu hachunguziki.

Sasa tuendelee na kauli hatari katika uwekezaji na ujasiriamali wako!

**Kauli ya Kwanza: Huwezi kuwa tajiri bila kutoa kafara.**

Wengi tunaamini hakuna utajiri bila kutoa kafara; hakuna mafanikio ya biashara bila ushirikina; huwezi kuchomoka kibiashara bila chuma ulete, full kutiana hofu tu. Yaani tajiri asipate msiba, akifiwa katoa kafara; gari la tajiri lisipate ajali watu wakafa, wakifa ametoa kafara; wateja wasipange foleni kwenye duka la tajiri, wakifanya hivyo basi kachimbia kiganja cha alubino mlangoni. Maskini wengi wameamua kubaki maskini ili wawe salama na wachache wamekwenda kwa waganga kutafuta utajiri wakadunda. Sikiliza. Ujasiriamali si uchawi. Ujasiriamali una kanuni. Mojawapo ni kuinyima roho kitu inapenda! Hii ni ngumu sana kwa maskini. Maskini akipata matako hulia mbwata, utasikia acha nile bata, maisha yenyewe mafupi, halafu atapiga picha na kuzisambaza mitandaoni dunia nzima ione anavyokula mtaji. Unajua ukiwa maskini halafu mshamba utateseka sana.

**Kauli ya Pili, huwezi kuwa tajiri bila kupiga, kwahiyo matajiri wote ni wezi tu.**

Kauli hii inaua hulka ya kufanya kazi kwa bidii na maarifa na hivyo watu kuishi kwa kuzengea nani wampige. Hawa ndo wanaamini kila mtu ni mwizi, tumetofautiana fursa za kuiba. Wakiona mtu kaajiriwa halafu asiibe wanamuita fala. Labda ni kwambie tu, wizi siyo dili, dili ni kutafuta watu watakaokupa changamoto za kimaendeleo na si za kimatumizi. Changamoto za kimatumizi zitakufanya uwe mwizi tu. Kuendelea kusambaza upuuzi kwamba kila tajiri ni mwizi haitakusadia kitu zaidi ya kuwanunia matajiri bure wakati tajiri hanuniwi. Acha ujinga upate kuishi, yanasema maneno ya Mungu katika Methali 9:6.

**Kauli ya Tatu, ogopa madeni maana yanaua.**

Hivi unajua kama Mungu mwenyewe anayakubali madeni? Kama Yesu aliwakopesha wale watumwa wakapige biashara watoke utumwani, wewe ni nani hadi useme mikopo haifai? Tatizo ulichukua mkopo ukaunywa badala ya kuuzungusha, ukashindwa kulipa, ukadhalilishwa ndo maana ukachagua kuwa msema hovyo ati mikopo haifai, kumbe wewe ndo hufai. Labda nikwambie tu hakuna tajiri asiyekopa. Tena anakopa hela za maskini. Maskini anaweka pesa ili imfae kwenye shida, halafu tajiri anazikopa, ananunua daladala ili maskini asafiri, anajenga nyumba ili maskini akapange, anajenga zahanati ili maskini akatibiwe, anafungua mgahawa ili maskini akanywe supu ya kongoro na chapatti mbili. Maskini bwana eti anaweka hakiba imfae wakati wa shida na wakati kuwa maskini tayari ni shida.

Anza kukopa sasa ewe mtumwa mwema. Kuchomoka maishani bila mikopo ni mziki mene. Halafu sifa ya mwanaume ni kudaiwa bana. Kwanza madeni yanaamsha akili. Madeni yanakufanya uwe mchacharikaji. Lakini pia madeni yatakupa akili ya kumshawishi anayekudai akukopeshe tena kabla hujamlipa. Halafu siri ya madeni ni kopa sana na kuwa mgumu kulipa deni, lakini mwiko kudhulumu maana dawa ya deni kulipa. Kikubwa hakikisha ukichukua mkopo, marejesho yatokane na faida na siyo kurejesha

tena zilezile ulizokopa. Ndiyo maana lazima uwe na mbinu kali za kumkwepa mdeni wako. Hili watu wa mabenki wanalijua, ndo maana wakati wa kudai huja na sura ya mbuzi, lakini wakati wa kushawishi uchukue mkopo kwao wanakuja na sura ya kondoo.

**Kauli ya Nne, walimwengu si watu, kaa nao mbali.**

Hivi unaanzaje kukaa mbali na watu na wakati ujasiriamali unahitaji watu? Hii ni sawa na kuwaponda wanawake na wakati huwezi kuishi bila mwanawake, labda uwe mgonjwa. Wenzako matajiri wakiona watu wanawaza cha kuuza ili watajirike zaidi kwa sababu watu ni fursa, wewe ukiona watu unajihami wasikuue kwa sababu watu ni hatari kwako, loh! Halafu mtu mwenyewe unayeogopa watu wasikuue hakuna unachomiliki zaidi ya simu ya kuchat na kutukana wenye akili kwa sababu una wivu wa kichawi.

Leo hii uchumi wa China ni tishio kwa sababu ya population. Kama unataka kutoboa kwenye ujasiriamali penda watu tu ndo maana Yesu akaongeza Amri mpya ya UPENDO. Soma Yohana 13:34. Narudia tena, soma Biblia hata kama huna mpango wa kwenda Mbinguni. Ina mafundisho mengi mazuri. Ukiiangalia Biblia kwa jicho la kitumwa utapishana na maarifa yaliyomo humo.

**Kauli ya Tano: pesa ni chanzo cha mabaya yote.**

Ukiwa mjinga sana utakubaliana na usemi huo kwamba pesa ni chanzo cha mabaya yote, ukiwa nazo utakosa amani, wenye pesa hawana furaha na wakati wahenga walisema pesa ni sabuni ya moyo. Kuona ubaya wa pesa tu na wakati kila kitu kina ubaya na uzuri ni maandalizi ya kufa lofa. Usafiri wa ndege ni mzuri sana lakini ukiwaza kuanguka huwezi kupanda ndege, bila kisu huwezi kufurahia nyama choma lakini unapokiona kisu ukawaza

kuchinjwa basi utakichukia kisu. Pesa hi hivyohivyo. Kama huna uwezo wa kuimudu pesa lazima ikuue.

Lakini kuichukia fedha ni kumchukia Mungu pia maana imeandikwa katika Hagai 2. 8 kwamba fedha na dhahabu ni mali ya Bwana. Halafu unavyochekesha huna hata cheni ya dhahabu, kwa sababu umeambiwa kujiremba ni dhambi. Loh! Nyumba ya Mfalme Suleiman, unayemuita baba yako wa imani ilipambwa kwa vito vya dhahabu.

Nakubaliana na wanaosema ukiwa na pesa unaweza kununua chakula; lakini si hamu ya kula; unaweza kununua dawa, lakini si uponyaji; unaweza kununua kitanda kizuri, lakini si usingizi, lakini waniambie ni lini umaskini ulinunua furaha? Kama hauna pesa ndo hatari zaidi, maana unaweza kuwa na hamu ya kula ukakosa kitu cha chakula,unaweza kuwa na usingizi ukakosa pa kulala, unaweza kuugua ukakosa ukafa. Kikubwa tafuta pesa uache jeuri!

Mimi nadhani pesa siyo mbaya ubaya ni kuwa mtumwa wa pesa kwani unaweza kutoa roho za watu ili uzipate. Wenzako wakiona fedha wanafikiria uwekezaji zaidi, utajiri zaidi, maisha mazuri zaidi, kuinua kazi ya Mungu zaidi, shule nzuri zaidi kwa watoto wao, wewe ukiona pesa unawaza kuongeza mademu zaidi, kuongeza ulevi zaidi, kuvuta bangi zaidi, kuongeza mauaji zaidi, kufanya usaliti zaidi, kuongeza uzinzi zaidi na kula bata zaidi ndiyo maana unamuomba Mungu akuepushe nazo. Hata mkeo anafunga na kuomba usipate hela maana huwa unarukwa na akili ukizipata. Kama ukipokea laki mbili tu ya mshahara hulali nyumbani, ukipata milioni?

Tafuta pesa ewe kondoo mwema usiye na lolote ujiongezee baraka duniani na mbinguni maana ukiwa na pesa hata kazi ya Mungu utaifanya kwa uaminifu. Ikitangazwa michango kanisani utakuwa wa kwanza kuchangia lakini kama hauna pesa utakuwa

wa kwanza kuwatukana kimyakimya viongozi kwa kutangaza michango. Kwani unadhani hizi kelele za kusema michango makanisani imezidi zinatoka kwa watu gani? Zinatoka kwa wasiokuwa na pesa! Saka pesa uepuke dhambi ya kuwatukana watumishi wa Mungu kimyakimya.

Halafu utakulaje mema ya nchi kama huna pesa? Hivi nani asiyependa kusafiri kwa ndege? Nani anayependa mwanaye asome katika shule zinazoandaa wapiga kura badala ya wapigiwa kura? Nani anayependa kulala chumba kimoja na gunia la mkaa, debe la unga na mbuzi? Au tuseme stoo? Hayupo. Pesa siyo jibu la kila kitu, lakini walau inaleta ahueni ya maisha, ukiwa nazo hautalala stoo, hautakula vyakula vya kuku na mbuzi, utakula kuku na mbuzi wenyewe, hautovaa tisheti za Jaza Ujazwe; tisheti za Tanzania bila kifaduro inawezekana, utavaa nguo zenye heshima, hautosafiri kwa mabasi ya abiria chunga mzigo wako, hautotibiwa kwenye hospitali zisizo na dawa lakini zinakondom, nakwambia ukiwa na pesa hata jamii itakuheshimu, utaitwa mzee katika umri mdogo. Wokovu ni akili kichwani, imani moyoni na pesa mfukoni alisema Bishop Augustine Mpemba.

**Kauli ya Sita: Dunia imeoza, dunia imekwisha, dunia ni takataka na wakati Mungu alitukabidhi Dunia tukaitawale.**

Kauli za kuiponda dunia ni hatari kwa sababu utatumia muda mwingi katika maandalizi ya kufa na kunyakuliwa badala ya kuwekeza kiuchumi. Hawa ndo wakifa historia ya marehemu inakuwa fupi sana. Marehemu alizaliwa, akakua, akazurula, akafa, apumzike kwa amani kwa kumaliza kazi yake hapa duniani. Hivi ni kazi gani amemaliza na wakati ameacha mke na watoto kwenye nyumba ya kupanga? Jamani tuacheni kudanganyana! Hii dunia ni ya kwetu, tuipende, dunia ni ya kwetu tuitunze, dunia ni ya kwetu, tuijenge, dunia ni ya kwetu tusiitelekeze tukidhani kuna dunia nyingine, maana imenadikwa

Mbingu ni za Mungu, nchi ni za wanadamu. Soma Zaburi 117: 16 uone kama nakutania. Sasa we nyea kambi tu! Piga kazi ewe kondoo mwema ili dunia iwe mahali pazuri kwa mwanadamu kuishi. Acha kuponda mali za Mungu.

**Kauli ya Saba: Ponda mali kufa kwaja na wakati kifo siyo nukta, kifo ni alama ya mkato.**

Kumbuka kuna maisha baada ya kufa ndo maana jina zuri la Mwl Julius Nyerere bado linaishi. Kauli hii imechangia watu wengi kushindwa kuwa na mipango inayozidi mwaka mmoja. Yaani tunaishi jana na leo, kesho itajijua. Wengi tukipata pesa hatutulii mpaka ziishe zote. Tutanunua mpaka vitu tusivyovihitaji ili kuwarusha roho wasiotupenda, tukitoka out tunataka tumlipie kila tuliyemkuta pale utadhani yeye alitoka out bila pesa. Hivi unajua kama ukarimu ukizidi ni uwenda wazimu mpendwa?

Wakati matajiri wanashindana katika uwekezaji, maskini wanashindana katika matumizi. Mlevi mmoja alisema yaani nitafute pesa kwa shida halafu niitumie kwa shida? Nikifa je? Ukipata tumia, ukikosa mshukuru Mungu. Kuponda mali kufa kwaja siyo issue sana, lakini ukifa utaacha nini? Mobutu Sese Seko Kuku wa Zabanga aliponda mali, akafa na kuacha jina baya. Usiache jina baya ewe kondoo mwema uliyekosa maono.

**Kauli ya Nane: Napotezapoteza muda walau masaa yaende na wakati imeandikwa ukomboeni wakati.**

Funua Waefeso 5:16 ingawa najua huna muda wa kufunua Biblia, lakini una muda wa kufunua vya gizani, loh! Ukipoteza muda, muda utakupoteza. Kila saa unayopoteza ni fursa ya kuwa na balaa baadaye. Ukichagua kuchezea muda huwezi kukwepa matokeo yake ambayo ni mabaya tu. Hata uwe na akili kiasi gani, ukishindwa kuyatawala masaa 24 ya kila siku utaishia kuwa msimulizi wa mafanikio ya wenzako., “Jamaa tulisoma naye,

darasani alikuwa chenga. Ati darasani alikuwa chenga na wakati leo ndo DC wako. Acha kukariri bro!

Wakati Wachina wanapunguza mpaka masaa ya kulala ili muda utoshe kujenga madaraja, wewe unalala mapema kama kuku na kuamka late kama mlinzi aliyekesha akilinda duka la muhindi kwa mshahara wa makongoro ya mbuzi na utumbo wa kuku. Full kulaliwa kama house girl wenu, mwaka wa pili sasa hamjamlipa vijisenti vyake, ati mnamtunzia. Wizi tu! We poteza muda tu lakini kumbuka muda haupotei, wanapotea watu!

**Kauli ya Tisa: Kupata ni majaliwa, aliyekupa wewe ndo kaninyima mimi.**

Hizi ni kauli zinazoua juhudi za kufanya kazi na hivyo mtu kubaki akiishi kwa kubahatisha na wakati maisha siyo kubahatisha, maisha ni kupatia. Kwanza kitendo cha kuzaliwa tu ni bahati, halafu unasubiri bahati nyingine. Erick Thomas, anasema unapokaribia kushindwa kabisa basi ndio inabidi usubiri hiyo bahati vinginevyo komaa mpaka kieleweke. Bahati huambatana na kuchacharika, ndo maana wahenga walisema bahati ya mbwa iko miguuni mwake. Bahati inatengenezwa, amka ukaitengeneze. Fungua hata genge la kuuza chakula uone kama bahati haijakukuta huko. Maskini ni wengi na wanapenda sana kula, tumia hiyo kama fursa. Linapokuja suala la kula maskini ni jasiri sana. Maskini anaweza kuwa na elfu kumi mfukoni akala yote kwa sababu yeye anaishi leo, hana kesho. Kesho itajijua.

**Kauli ya Kumi na ya mwisho: mimi ni wa hivihivi, siwezi kufanikiwa maana ukoo mzima tajiri alimiliki baskeli.**

Utasikia kwanza hata vidole havilingani sasa kwa nini nijisumbue kutafuta utajiri usiowezekana; wapo waliopangiwa sisi ni wasindikizaji tu. Mzee Mengi aliwahi kusema mafanikio ya mtu

hayahusiani na historia yake ndo maana yeye alijenga ghorofa na wakati baba yake alimiliki kuku. Hawa wenye fikra za vidole havilingani ndo hawakosi katika kila burudani walau wapoteze muda na mawazo. Yaani unapoteza mawazo na wakati wenzako wanauza mawazo kwa gharama kubwa sana! Labda nikwambie tu, mbele za Mungu watu wote ni wa thamani ndo maana imeandikwa nilikujua tangu u tumboni kwa mama yako. Safisha fikra zenye sumu akilini mwako na waza mambo makubwa. Kumbuka hata mbuyu ulianza kama mchicha. Shalom!

## Sura ya 9

# Matatizo Hayaondoki Kwa Kulialia

Dunia imejaa mambo ya kuhuzunisha kuliko kufurahisha. Au tuseme, imejaa matatizo. Matatizo yanavunja moyo, matatizo yanasononesha, matatizo yanaumiza, matatizo yanafedhesha, matatizo yanashusha hadhi ya mtu, matatizo yanaua.

Pamoja na kwamba uhai ni zawadi kutoka kwa Mungu, wengi tunajuta kuzaliwa kwa sababu ya matatizo. Tunafunga na kuomba na wengine kukesha kwa wachawi na waganga ili kupata ahueni ya maisha lakini bado hali inazidi kuwa mbaya, pesa mfukoni hakuna, ramani hazisomi, hata kula ni kwa manati, sasa tunakula vyakula vya mifugo badala ya kula mifugo yenyewe.

Shida hapa iko kichwani.Tunatumia nguvu nyingi kukemea na kuroga badala ya akili. Tumieni akili kama ipasavyo ni maagizo kutoka kwa kitabu kitakatifu. Soma 1: Wakorintho 15: 34. Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa siyo rasilimali ( Hosea 4:6). Katika hiki kipindi cha mitume na manabii kondoo wanateseka sana kwa sababu ya kutotumia akili. Yaani wanapokuwa nabii, kila utakalo waambia watafuata hata kama ni kula magome ya miti ili wapate utajiri. Kuna mchungaji huko Afrika Kusini anasema anaponya kwa kutumia ushuzi wake, na kondoo wanapanga mstari kwenda kunyampiwa. Jamani!

Hivi unafahamu kama kutumia akili kunalipa sana? Sikiliza, unajua ukitumia akili hata kidogo, utaelewa matatizo yote ni

sehemu ya maisha, kuyashinda ndio hufanya maisha yalete ladha, kuyazuia ni sawa na kuziba shimo la panya kwa mkate. Haiwezekani. Kuna methali ya Wayahudi inasema, Simuombi Mungu anipe mzigo mwepesi, namuomba anipe mabega makubwa kuweza kubeba mzigo wowote. Maana yake ni kwamba kuyakimbia matatizo ni kukimbia fursa. Hebu mlilie Mungu akupe akili kama alivyoahidi kupitia (Zaburi 119:169), "Kilio changu kikufikie, ee Mwenyezi-Mungu! Unijalie akili kama ulivyoahidi."

Wenye akili huona fursa katika kila tatizo na wajinga huo matatizo katika kila fursa! Sikiliza, matatizo ni kama giza la kukusaidia kuona nyota. Bila matatizo hakuna uvumbuzi. Tunasoma katika Isaya 9:2 kwamba "Watu waliotembea gizani wameona mwanga mkubwa". Maana ya mstari huu ni kwamba watu hao walifanya kitu baada ya kuchoka kukaa gizani.

Tatizo la ukame limewafanya Waisrael kuendesha kilimo cha matunda kwa kumwagilia kwenye mmea tu na sasa wanauza matunda duniani kote. Hizo ni akili. Waliona nyota katika giza. Sisi tuna mito, ardhi safi na majira rafiki lakini tunakula matunda kutoka Afrika ya Kusini kwa sababu hatuna akili.

Wenye akili walivyoona kutembea kwa miguu kunawachelewesha walitengeneza vyombo vya usafiri; wenye akili walipoona giza linasumbua walivumbua umeme; wenye akili walipoona barua ni nusu ya kuonana wakavumbua teknolojia ya mawasiliano sasa dunia ni kama kijiji; wewe unatumia akili kulia na kulaumu badala ya kufanya kitu. Ukiona tatizo unakimbilia kuombewa na wakati jamaa zako wanakimbilia kuchanjwa chale kwa Waganga. Njaa inaingia nyumbani kwako unaomba Mungu akupe chakula hata shambani

hujawahi kukanyaga. “Achana na ujinga upate kuishi; fuata njia ya akili” yameandikwa katika Mithali 9:6. Unaitwa mtumishi wa Mungu hata bustani ya mboga huna. Yesu mwenyewe mtoto wa Mfalme alikuwa fundi seremala, sembuse wewe mtoto wa asiyejulikana hata mtaa wa pili tu? Mtume Petro alikuwa mvuvi! Hufanyi kazi halafu unataka kula na wakati imeandikiwa asiyefanya kazi na asile ( 2 :Wathesalonike 33:10) siyo aombewe. Ina maana asiyefanya kazi afe. Mwenye busara hutenda kila kitu kwa akili, lakini mpumbavu hutembeza upumbavu wake (Methali 13:16).

Unapokutana na matatizo usikate tamaa. Kuwa kama nywele na kucha.Haijalishi unavikata mara ngapi lakini haviachi kuota. Vizuizi viko vingi lakini ni mwiko kukata tamaa. Ili punje ya ngano iote, lazima izikwe ardhini.

Ukitumia akili utagundua kwamba matatizo ni weusi ulioko nyuma, mbele ni kweupe, usikubali kurudi nyuma kwenye giza. Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo. Mke wa Ruthu aligeuka nyuma akawa jiwe la chumvi.

Ukitumia akili utalifanya tatizo lako kuwa fursa. Badili hasi kuwa chanya, badili sumu kuwa dawa, badili jangwa kuwa msitu, badili mlima kuwa tambarare, penye giza washa mshumaa, penye chuki panda upendo, penye mto weka daraja, kumbuka hata Yesu alibadili maji kuwa divai watu wakaenjoy pale Kana (Yohana 2:1-11). Hata mauzo ya Yosefu kule Misri yaligeuka kuwa fursa kwa familia yake. “Mimi ndiye ndugu yenu Yosefu, mliyemwuza Misri. Lakini sasa msifadhaike wala kujilaumu kwa kuniuza. Mungu ndiye aliyenileta huku niwatangulie, ili niyaokoe maisha ya watu (Mwanzo 45: 4-5). Kila tatizo lina makusudi yake, ni suala la kutuliza akili tu.

Ngugi wa Thiongo aliandika kitabu cha Shetani Msalabani akiwa gerezani akapiga hela mbaya. Wakati wengine wakiwa gerezani wanawaza mbinu mpya za kuiba, wenye akili wanawaza namna ya kufaidika kutokana na kifungo. Maana yake ni kwamba unaposongwa na matatizo usijinyonge.

Wakati mwingine matatizo ni ujumbe, usikilize, matatizo ni wimbo uimbe, matatizo ni maisha yaishi, matatizo ni kifo kicheleweshe, matatizo ni fursa inyakue. Siyo kwamba mambo ni magumu ndiyo maana hatuthubutu, ni kwa sababu hatuthubutu ndiyo maana mambo ni magumu.

Matatizo ni sumaku inayokuvuta uwe karibu na Mungu! Wakati mwingine Mungu hutumia matatizo ili utukufu wake uonekane. Mungu angeweza kabisa kuzuia Yohana kukaangwa kwenye mafuta yanayochemka na kutupwa kwenye kisiwa cha mateso cha Patmo, Mungu angeweza kuzuia Isaya kukatwa vipande vipande kwa msumeno wa kukatia mbao akiwa hai, Mungu angeweza kuzuia Stephano kupigwa mawe mpaka kufa, Mungu angeweza kuzuia Daniel kutumbukizwa kwenye tundu la simba, Mungu angeweza kuzuia Yusuph kutupwa gerezani, Mungu angeweza kuzuia Shedrack, Meshack na Abednego kutumbukizwa kwenye tanuru liwakalo moto, lakini hakufanya hivyo. Aliruhusu matatizo hayo kutokea ili wamsogelee yeye.

Bila matatizo kuna watu wasingekanyaga kanisani wala msikitini. Bila matatizo Mungu asingetukuzwa hospitalini na gerezani. Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyanifariji (Zaburi 23: 4).

Mungu kabla hajakuweka juu ya mnala, anaweza kukuweka shimoni, kabla ya kukupa furaha akakupa karaha, kabla ya kukupa baraka akakupa balaa, kabla ya kukupa matamu akakupa machungu. Mwiko kukimbia. La msingi hapa tuwe tayari kukamuliwa kama sponji yenye maji. Mvua ile ile inayosababisha mafuriko na kuua watu ndio inayostawisha mazao mwanadamu apate chakula. Moto unaoyeyusha mshumaa ndio huivisha tofali.

Haijalishi tatizo lako ni kubwa kiasi gani, cha msingi pambana kama Daudi. Daudi alipoona ukubwa wa Goliath, alijipa moyo na kusema, "Walau jiwe langu halitakosa pa kupiga." Kweli bwana alipojaribu kulipiga, siakaliua? Daudi alipambana. Hakumuachia Mungu! Matatizo yakukomaze kama maji yakomazavyo zege.

Kinacholeta baa la njaa ndicho kinakuonyesha chakula kilipo. Njaa ndiyo iliyomkumbusha yule mwana mpotevu kuwa kwa baba yake kuna chakula tele. Tunasoma hivi katika Luka 15:17, Alipoanza kupata akili, akafikiri: 'Mbona kuna wafanyakazi wengi kwa baba yangu wanaokula na kusaza, nami ninakufa njaa?" Kuruka ruka kwa maharage ndio kuiva kwake walisema wahenga.

Ufupi wa Zakayo ulisaidia wokovu ukaingia nyumbani kwake, akaacha kudhulumu. Ni baada ya kupanda juu ya mti na Yesu kumuona. "Zakayo, shuka upesi, maana leo ni lazima nishinde nyumbani mwako" (Luka Luka 19: 2-5, 8). Zakayo akawa amekutana na Yesu hivihivi kwa sababu ufupi si ugonjwa.

Maisha yanapokupa limao, tengeneza juisi ya limao, maadui wanapokutupia mawe, yakusanye ujenge ghorofa, matatizo yakikupa huzuni igeuze kuwa furaha kwa sababu huzuni haikusaidii lolote zaidi ya kuumiza moyo wako bure. Tumuige

Yesu aliyevumilia kifo msalabani na leo hii ameketi upande wa kulia wa kiti cha enzi cha Mungu (Waebrania 12:2). Kumbuka hakuna anayefurahia uchungu wa kung'olewa jino ila kila mtu anafurahia matokeo yake.

Ukiwa na akili utakubaliana na mimi kwamba matatizo ni mtizamo tu. Mvua inaponyesha kuna watu wanaona tope, wengine wanaona mazao yakistawi. Mtazamo ni jambo dogo sana linalofanya tofauti kubwa maishani. Hata jani la chai linapata nguvu ya kugeuza rangi ya maji likiwa kwenye maji ya moto. Matatizo yanaongeza nguvu. Kumbuka ni njaa ndio hukipatia chakula ladha, ni kiu ndio hufanya maji yawe matamu, ni jua kali ndio hufanya kivuli kiwe na thamani, ni upweke ndio huleta uhitaji wa urafiki,ni fujo za watoto ndio huleta uhai wa nyumba.

Matatizo ni mengi, jipeni moyo mtashinda alisema Yesu. Kuna mtu alimwambia mvuvi, wewe huogopi kwenda baharini kuvua samaki? Mjomba wako alifia baharini, baba yako alifia baharini, kaka yako alifia baharini, wewe mbona huogopi? Mvuvi akajibu, "watu wengi wanakufa wakiwa vitandani lakini watu hawaachi kulala vitandani".

Matatizo ni msalaba, ubebe ukubebe. Nelson Mandela aliubeba msalaba wake kwenda jela, msalaba ukambeba kwenda Ikulu. Huwezi kuukwepa msalaba, kila mahali utaukuta. Msalaba ni jirani yako mbebe, msalaba ni mke wako mebebe, msalaba ni watoto wako wabebe, msalaba ni wazazi wabebe, msalaba ni kazi yako ibebe, msalaba ni magonjwa yako yabebe, msalaba wako ni vishawishi, njaa, wajibu wako kwa Mungu, wajibu wako kwa umma na kwa kanisa vibebe. Mtu asiyechukua msalaba wake na kunifuata, hanistahili ( Mathayo 10:38).

# Sura ya 10

# Jina Lako Laweza Kuwa Sababu ya Balaa Unazopitia

Nani anaweza kumwita mwanaye Adolf Hitler? Vipi Idd Amin? Osama Bin Laden? Kaini? Shilawadu Je? Unafikiri ni kwa nini? Ni kwa sababu majina hubeba nguvu kubwa. Yaweza kuwa nguvu mbaya au nzuri, nguvu yenye neema au noma, baraka au balaa, ndo maana wenye maarifa wako makini sana na majina.

Kuna uwezekano mkubwa hilo jina lako ndo chanzo cha njaa uliyonayo pamoja na bidii yako katika kazi, chanzo cha magonjwa yanayokumalizia pesa, chanzo cha utasa wa muda mrefu, chanzo cha kufukuzwa kazi kila unapoajiriwa, chanzo cha ulevi unaokupelekesha, chanzo cha michepuko kukulia pesa zako, chanzo cha kuzaa nje hovyo kwa jina la kitanda hakizai haramu, dawa ni kulikataa hilo jina. Hata Ibrahimu na mke wake Sara walitoka kimaisha baada ya kubadilishiwa majina. Sarai akaitwa Sara na Abramu akaitwa Ibrahimu.

Jina lina nguvu asikwambie mtu,ndo maana huko kwenu mtoto akilia anapewa jina la babu yake na kunyamanza. Hii ni hatari kwani mtoto anaweza kunyamaza jumla katika biashara, ndoa, maisha na hata elimu. Huyu ndo akiwa shule utasikia kapewa mimba na mwalimu akiwa form 1, mara amekula ada, hamjakaa sawa kauza TV, yaani full kuhenyesha wazazi. Shida ni jina. Acha kuwasumbua watumishi wa Mungu bure!

Unahitaji kuomba kwa bidii ili kuvunja laana, maagano na matambiko yaliyofanywa dhidi ya majina uliyorith toka kwa bibi na babu zako, vinginevyo unaweza kukuta watoto wako wote ni wachawi kwa sababu uliwapa majina ya babu na bibi zao waliokuwa wachawi!

Unaweza kujipa moyo kwamba umeokoka shetani hakuwezi. Wokovu wenyewe wa kubeep! Kanisani unakwenda kusinzia wakati wote wa mahubiri na kuwa macho wakati wa kwaya, huna hofu ya Mungu, unawasengenya mpaka watumishi wa Mungu, huna adabu, halafu unasema una Yesu.

Kila unachofanya hakiendi, unaamua kwenda kutafuta ahueni kwa waganga, wanakushughulikia kweli kweli kumbe tatizo ni jina. Kuna mume mmoja alikwenda kutafuta utajiri kwa mchawi, mchawi akamwambia njoo na mkeo. Walipofika, mchawi akasema, “Ingia kwanza wewe,” Mume akaingia, mlango ukafungwa na kuanza kumchanja viwembe na kumpaka pilipili. Mume alipiga kelele balaa. "Haya toka nje na mkeo aingie." Mke alipoingia mchawi alifunga mlango na kuanza kumbaka, wacha mama apige kelele. "Vumilia mke wangu," Mume alimtia moyo mke akijua ni pilipili. Mke akajua mume alimtoa kafara kwa mganga ili wapate utajiri. Ndoa ikawa mashakani kwa sababu ya laana ya jina. Nukuu hii imetoka uk 59 wa kitabu cha Maisha ni Kutafuta Si Kutafutana, rusha Sh 5000 kwa 0753665484 kurushie sasa hivi!!

Unaweza kujikuta umewaumiza wanao kwa kuwapa majina usiyoyajua. Siku hizi kila mtoto anayezaliwa kama siyo Angel basi ni Junior.

Wewe ni tajiri lakini wanao wanamiliki umaskini wa kuwatosha kwa sababu uliwapa majina yenye vinasaba vya umaskini! Unang'ang'ania kumpa mtoto jina la babu yake na wakati hakuwahi kumiliki hata mkokoteni! Mtoto alizaliwa na baraka zake, wazazi wakazifunga kwa kumpa jina lililobeba umaskini, mtoto anakufa maskini na mbinguni haendi maana imeandikwa Mungu hafanyi maagano na maskini.

Maskini hana hoja, ana haja. Mpendwa anadondosha elfu 10 kanisani maskini unaikanyaga na kuondoka nayo ukanunue unga halafu unajiita shujaa wa Yesu. Jaribu la shilingi elfu 10 tu limekushinda, ukipewa vikubwa je?

Kitendo cha Mungu kuwabadilisha watu majina ni ujumbe kuwa makini na majina tunayowapatia watoto wetu. Usikubali kirahisirahisi ndugu kumpatia jina mwanao. Watambambika jina litakalomfanya mtoto wako awe mtu wa majanga.Unashangaa katoto kadogo kana na presha, sukari, kansa na magonjwa mengine mengi ya wakubwa. Kumbe kamerithi kutoka kwa wajina wake.

Kwanza hata Mungu hapendi ndo maana alimpiga ububu mume wa Elisabeti Mzee Zakaria ili asimpe mwanaye jina la ukoo, na baada ya jina tu mzee akapona ububu, mtoto huyu ni Yohana Mbatizaji!

**Hebu tusome habari ya kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji (**LUKA 1:57-64), *"Ikawa siku za kujifungua kwake Elizabeti zilipotimia, alizaa mtoto wa kiume . Habari zikawafikia majirani na jamaa jinsi Bwana alivyomfanyia rehema kuu. Nao wakafurahi pamoja naye. Mtoto alipokuwa na umri wa siku nane, watu wakaja kuhudhuria tohara yake. Wote wakataka wampe*

*yule mtoto jina la Zakaria, yaani jina la baba yake. Lakini mama yake akakataa na kusema, "La si hilo. Jina lake litakuwa Yohana." Wakamjibu, "Mbona hakuna mtu katika jamaa yako mwenye jina kama hilo?" Basi wakaamua kumwuliza Zakaria kwa ishara kwamba yeye angependa mtoto aitwe nani. Akaomba mahali pa kuandikia, naye akaandika: "Jina lake ni Yohana." Watu wote wakastaajabu. Papo hapo uwezo wa kusema ukamrudia Zakaria naye akaanza kumsifu Mungu. Watu wote walioshuhudia jambo hili wakastaajabu mno, na habari hii ikaenea sehemu zote za wilaya ile ya Yudea."*

Hivyo ndivyo alivyopatikana Yohana Mbatizaji. Katika hayo maandiko unaweza kujiuliza kwa nini Mungu aliamua kutoa jina kwa Yohana mbatizaji? Huku ndugu wakitaka jina la ukoo? Mungu alijua kabisa jina hilo la ukoo lisingeweza kutimiza kusudi lake. Kumbe kuna majina hayawezi kutimiza makusudi ya Mungu. Pengine Mungu amekuandaa kuwa mfanyabiashara mkubwa duniani kwa bahati mbaya unapewa jina la babu aliyechukia biashara enzi za uhai wake. Hapo unakuwa umepishana na baraka za Mungu.

Wazazi na wale ambao mtakuwa wazazi baadaye liangalieni sana jambo hili yaani jina ambalo mtampa mtoto wenu. Lakini pia tafakari jina lako umelipataje? Je jina lako linatokana na nini? Kwa nini unaitwa Shida, Mateso, Sikujua? Tafakari chukua hatua.

Lakini jambo la pili ni kuhusu mahali unapoishi na kufanyia kazi. Inawezekana umeng'ang'ana kuishi Dar es Salaam na kumbe mafanikio yako yapo Songea, au umeng'ang'ania kuishi Songea mafanikio yako yapo Bukoba. Ama unakomaa na shughuli za ulinzi kwenye maduka ya wahindi Mwanza kumbe

wewe ni mkurugenzi wa wilaya ya Sikonge. Kila kitu kinawezekana brother. Unaweza kuwa umekomaa na kazi ya mgambo wa jiji kumbe wewe ni mhasibu wa halmashauri ya Kibondo. Unaweza kuwa umekomalia kazi ya kufundisha kumbe wewe ni meneja wa benki.

Usipokuwa na eneo sahihi, utashangaa miaka inaenda, umri unakatika, unapambana kufa na kupona lakini maisha hayasomeki! Utapata mshahara kila mwezi, lakini hata nyumba ya kuishi unaweza usijenge. Au ikitokea umejenga basi unaijenga kwa taaabu kweli. Hujaskia mtu anashindwa kunywa hata soda kwamba anajenga? Utalima na kuvuna sana lakini soko hakuna. Yaani kwa ufupi utaendelea kupigika mpaka utakapopata eneo sahihi. Maisha hayana uchawi ni maujuzi tu!

Ibrahim alipohamia Kanaani kutoka kule Uru ya Ukaldayi mafanikio yalianza kujipa yenyewe. Akapata na mtoto. Alibarikiwa mpaka akashangaa. Yusufu aliukwaa uwaziri mkuu baada ya kuuzwa Misri. Alikuwa na hela mpaka akanunua nchi nzima na watu wake wote. Jeuri ya pesa! Soma (MWANZO 47:19-20).

Unaweza kuona uhamisho kama adhabu kumbe ni sawa na kumpiga chura teke. Tanzania tunaamini uhamisho ni adhabu! Unapokea barua ya uhamisho kutoka Dar kwenda Kibondo unastruggle kupangua uhamisho kumbe unapangua baraka zako. Hata Yakobo alipata utajiri mkubwa sana alipohamia kwa mjomba wake Laabani. Alipata wake na kondoo kibao.

Sasa mwanangu mtaa unaoishi unapishana na ng'ombe, mikokoteni, bodaboda na vibaka unategemea kutoka kweli? Huko huwezi kukutana na high profile people.

Mifugo yako haiongezeki, mke wako hazai, mazao yako yanaliwa na mifugo ya jirani na hauwezi kumshitaki jirani yako halafu bado umekomaa kuishi hapo utadhani ulitambikia. Tafuta sehemu sahihi uhame. Huwezi kufugia nguruwe karibu na msikiti! Kafugie mbali na msikiti. Hiyo nayo ni siri ya maendeleo. Kufugia nguruwe karibu na msikiti ni sawa na kufungua saluni ya kunyolea kwenye mtaa wa wenye vipara! Utamnyoa nani?

Hebu muulize Mungu vizuri, huenda mafanikio yako yatapatikana ukihamia mtaa wa saba, biashara yako itafanikiwa ukihamia huko, huenda mifugo yako itaongezeka ukihamia huko, yawezekana mke wako atazaa mapacha ukihamia huko.

Unalalamika huolewi na umeng'ang'ania kupanga mtaa wa fisi kumbe unatakiwa ukapange mitaa ya mapedeshee ili ukutane na mumeo anaefanyia kazi Benki Kuu. Angalia hata sehemu za kwenda kunywa soda. Huko kwenye soda za jero jero utakutana na wachumba wa jero jero. Jenga utamaduni wa kwenda kunywa soda za buku ten hata mara moja kwa wiki ukutane na wenye hadhi hiyo. Riziki ya mbwa iko miguuni bwana.

Unafanya kazi Morogoro unataka ukaoe Bukoba kwa sababu umeambiwa kuoa nje ya kabira lako ni kosa. Unaanzaje kuoa mke usiyemjua? Ulimchumbia lini? Hivi unaelewa maana ya urafiki, uchumba hadi ndoa? Ndoa za ghafla zitakupa maisha ya ghafla. Unauziwa mbuzi kwenye gunia unakwenda kuliwa kichwa. Unaweza kuoa mwanamke aliyenenewa mabaya na mababu zake, akikanyaga tu ndani ya nyumba yako mikosi inaanza. Kwanza anavunja vyombo vyote vya ndani. Furaha na amani vinatoweka. Unaanza kuona maluweluwe usingizini na kupiga kelele kama unachinjwa, kumbe ni mizimu imekuja kumsalimia mjukuu wao, yaani huyo mkeo.

Kadhalika unaweza kuangukia kwa mwanaume aliyezaa kila mtaa kama mbwa na baada ya ndoa unaanza kupambana watoto wake. Halafu ukiwaeleza wazazi wako wanakwambia **maisha ni kuvumiliana**. Nani kakudanganya kwamba maisha ni kuvumiliana. Maisha ni zawadi kutoka kwa Mungu huna budi kuyafurahia na si kuyavumilia.

Mke wako yuko mahali unapoishi na siyo ulipozaliwa. Mume wako yuko mahali unapoishi ongeza bidii ya kuomba upewe macho ya rohoni kuweza kuona yaliyojificha. Kuna koo ambazo wanawake hawaishi na wame zao. Unakwenda kuoa mahali unakuta dada wa kwanza mpaka wa tano wameachika, wana kaa kwa mama yao ambaye naye aliachika. Hayo huwezi kuyajua kwa sababu fimbo ya mbali haiui nyoka.

Mungu anaposema leteni hoja zenye nguvu ndo kama hizi. Hoja za kukuonyesha jina sahihi, mkoa sahihi, wilaya sahihi, mtaa sahihi au kijiji sahihi cha wewe kuishi na kufurahia uumbaji wake amina!

## Sura ya 11

# Maskini Hana Hoja, Maskini Ana Haja, Usimwamini Akakuliza!

Maskini hana hoja, maskini ana haja walisema wahenga wa kale. Muhenga ni mzee mwenye akili kwa sababu siyo kila mzee ana akili maana hata wajinga wanazeeka. Maskini haaminiki ndio maana Mungu hafanyi maagano naye. Hata kwenye vikao vya familia maskini akinyosha mkono kuchangia hoja ndugu watadhani anataka kufanya fujo. Ukiwa maskini unaweza kuumwa hata na umbwa yako alisema Man cush, mchekeshaji kutoka Kenya. Umaskini ni sawa na  kuadhibiwa kwa kosa ambalo hujatenda alisema.

Pamoja na balaa la umaskini bado kuna kondoo wanaamini kuwa maskini ni tiketi ya kwenda mbinguni kwa sababu imeandikwa, "Ni rahisi kwa ngamia kupenya kwenye tundu la sindano kuliko tajiri kuingia Mbinguni," kwahiyo wanafarijika sana kuwa maskini. Ngoja niseme ukweli tu, ukiishakuwa maskini hata akili inakuwa nzito kuelewa mambo katika uhalisia wake na kutawaliwa na fikra za kwamba fedha ndo chanzo cha mabaya yote na wakati unadaiwa kodi, unadaiwa ada, unadaiwa rejesho, unadaiwa mpaka zaka na sadaka, unahitaji matibabu full kuchanganyiwa.

Ukiwa na fikra za kimaskini utaogopa utajiri ili kujiepusha na maovu kwa sababu imeandikwa kupenda pesa ni chanzo cha

mabaya yote, lakini ukiwa na fikra za kitajiri utaogopa umaskini ili kuepuka upweke na kutawaliwa maana imeandikwa maskini hutengwa na rafiki yake na tajiri humtawala maskini, soma Mithali 19:4.Tafuta utajiri ewe mwana wa Mungu uishi salama.

Maskini ana fikra ya kufanikiwa bila kufanya kazi kwa sababu imeandikwa omba chochote kwa jina langu nawe utapokea, tajiri anafikr za kufanikiwa kwa kupiga kazi maana imeandikwa asiyefanya kazi na asile siyo aombe chochote. Kwa maskini kila kitu kwake ni maombi na wakati kwa tajiri kila kitu ni hapa kazi tu.

Maskini hudhani kila tajiri ni mwizi na anawadhulumu maskini lakini tajiri huamini kila maskini ni mvivu kwa sababu imeandikwa matakwa yake mtu mvivu humfisha, kwa maana mikono yake hukataa kufanya kazi, soma Mithali. 21:25 kwa muda wako halafu ukafanye kazi uepuke umaskini wa kukutosha.

Maskini hudhani ili kufanikiwa lazima usome sana kwa sababu imeandikwa mkamate sana elimu, usimwache aende zake; ndiyo maana maskini yuko tayari kulala njaa ili mwanaye asome na wakati tajiri anaamini kusoma sana siyo kufanikiwa badala yake mafanikio ni uwezo wa kutawala rasilimali zilizopo kwa sababu imeandikwa nendeni duniani mkatawale kila kitu.Kutomiliki mali ni kupingana na agizo la Mungu.

Kwa maskini kazi ni adhabu na wakati kwa tajiri kazi ni burudani. Maskini hutengeneza pesa kwa kufanya kazi asizozipenda, tajiri hutengeneza pesa kwa kufanya kazi anazozipenda.

Tajiri analala masaa machache akifanya kazi, maskini anawahi kulala kama kuku na kuchelewa kuamka na wakati imeandikwa amkeni asubuhi na mapema mkailime nchi.

Maskini anaamini matajiri wote ni washirikina na sehemu yao ni katika ziwa liwakalo moto na kiberiti, matajiri huamini maskini wote ni wavivu ndo maana wananyang'anywa hata vile vidogo walivyonavyo! Soma Mathayo 25: 29.

Lakini ni mapenzi ya Mungu tupate maana imeandikwa, Bwana, Mkombozi wako, Mtakatifu wa Israeli, asema hivi;Mimi ni Bwana, Mungu wako, nikufundishaye ili upate faida, nikuongozaye katika njia ikupasayo kuifuata" (Isaya 48:17).

Maskini anaamini hapa duniani tunapita kwa hiyo anatumia muda mwingi kujiandaa na safari ya kunyakuliwa, na wakati tajiri anaamini kilichoumbwa na Mungu hakifi ndo maana anachapa kazi as if ataishi milele. Wenye fikra za kitajiri hupanda miti ya mbao na wenye fikra za kimaskini hupanda mchicha na matembele wawahi kula kabla hawajafa.

Maskini anaamini binadamu ni wabaya na dunia yote imeoza, tajiri anaamini binadamu ni mtaji na dunia yote ni fursa. Maskini akikutana na binadamu anawaza kuliwa nyama, maana imeandikwa binadamu ni wala nyama, soma Zaburi 27:2), na wakati tajiri akiona watu anawaza namna ya kuongeza utajiri hata kama ni kwa kuanzisha biashara ya majeneza.

Maskini hufundisha watoto wake jinsi ya kupambana na maisha kwa sababu maisha ni mapambano, tajiri anafundisha watoto kuwekweza maana hakuna maisha bila uwekezaji. Maskini anapambana kuanzia kwenye maombi, kwenye chakula, kwenye

daladala hadi kufa maana dawa tu ya malaria inamtoa jasho, hana bima. Ukiwa maskini ni very funny yaani hata ukipata pesa unapambana kuzitumia, akiwa baa ni amri ya lete kama tulivyo, akipita mjini ananunua kila kitu, nyumbani kwake amejaza makorokoro, kununua vitu asivyovihitaji ili kuwarusha roho watu asiowapenda, yaani anailazimisha dunia ijue anazo. Kwake amejaza vitu mpaka hakuna sehemu za kukaa, mbaya zaidi vitu hivyo havitumiii kabisa.

Maskini ni mdogo kuliko matatizo yake ndiyo maana kila kitu anamuachia Mungu.Tajiri ni mkubwa kuliko matatizo yake ndo maana hutumia uwezo wa Mungu kukabiliana na matatizo. Mmisionari mmoja aliwashangaa waafrika wanaomba mvua wakati wamezungukwa na maziwa,mito na mabwawa mengi, waliomba awaponye magonjwa yanayowasumbua na wakati magonjwa mengi yanatokana na ujinga wa kutofuata kanuni za afya.

Tajiri humuomba Mungu amjalie mema zaidi katika juhudi na uwezo wake kama binadamu kwa sababu hakuna kitu ambacho binadamu hapewa na Mungu wakati anaumbwa maana tumeumbwa kwa mfano wake. Maskini anaomba Mungu amnyakue akafurahie maisha ya Mbinguni na wakati huko hakula kula wala kunywa, ni kusifu na kuabudu tu!

Amka ewe kondoo, tafuta utajiri uachane na umaskini uende Mbinguni salama. Kuukataa utajiri na kuukumbatia umaskini ni kumkana Yesu Kristo kwa sababu Yesu alikuwa maskini ili sisi tuwe matajiri, kama unadhani nakutania soma 2 Wakorintho 8:9. Ukiishakuwa maskini fahamu umepishana na Yesu live!

Kuukataa utajiri na kuukumbatia umaskini ni kupishana na Mungu kwa sababu Mungu mwenyewe ndo atoaye utajiri kama alivyosema kupitia Kumb. 8:18. Kuukataa utajiri ni kukataa upendo wa Mungu wa kututaka tufanikiwe katika mambo yetu kwa sababu imeandikwa, “Mpenzi, naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo” (3Yohana 1:2).

Kuukataa utajiri ni kukwepa majukumu tuliyopewa na Mungu ya kutawala mali zote zilizopo duniani maana imeandikwa, “Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana; dunia na wote wakaao ndani yake”.

Tatizo hatuisomi Biblia ili kuelewa, tunaisoma ili tukawatie wenzetu hofu ya Mungu. Kuna mahubiri mengine ukiyasikia usiku huwezi kulala. Unaweza kufikiri Mungu ni katili sana. Ndio maana zamani tuliamini ukisoma Biblia lazima uchanganyikiwe na watu waliamini hivyo. Kuna watu wanahubiri utadhani kweli wamechananyikiwa. Jamaa mmoja akaenda kuhubiri kwenye kilabu cha pombe kwamba, “Pombe ni mavi! Imeandikwa anayekunywa pombe anakula mavi” Sijui huo mstari uko sehemu gani katika Biblia. Ujinga bana!

Hakuna sehemu ambayo Yesu alisema wenye mali hawatauona ufalme wa Mungu isipokuwa yeye alisema kwamba itakuwa vigum kwa tajiri kuingia Mbinguni. Hebu tuusome vizuri mstari huu, (Marko 10: 25), Ni rahisi ngamia kupenya katika tundu la sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. Maana yake ni kwamba ni vigumu kwa tajiri kuingia mbinguni lakini siyo kwamba haiwezekani. Inawezekana kwa neema ya Mungu maana imeandikwa, Yasiyowezekana kwa wanadamu yawezekana kwa Mungu (Luka 18:26). Kumbe tajiri naye

anaokolewa kwa neema kama anavyookolewa maskisini pia. Sasa acha ujinga ewe mtu wa Mungu upate kuishi.

Unaogopa kuusaka utajiri kwamba hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili. Ingekuwa kumiliki mali ni dhambi unadhani Mungu angesema ukiacha vyote na kumfuata yeye atakupa mara mia? "Yesu akasema, Amini, nawaambieni, hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu, na kwa ajili ya injili, ila atapewa MARA MIA SASA WAKATI HUU, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele" (Marko 10:29-30).

Kuacha vyote hakuwa na maana kuuza ulivyo navyo, alikuwa na maana kutenga muda wa kuifanya kazi ya Mungu, tena kwa bidii. Yaani linapofikia suala la Mungu, simamisha kila kitu na uwe pale kimwili na kiakili, hata nzi akikugusa usimskie. Sasa mwenzangu uko ibadani lakini kila meseji inayokuja unaisoma. Katika hili waislamu wamefanikiwa sana. Ikifika muda wa swala hata umletee kiasi gani cha fedha lazima duka lifungwe akaswali kwanza halafu wajinga wanasema analinga. Hivyo ndo tafasiri halisi ya mstari huu. Mali ya dunia iliwekwa kwa ajili ya kumtumikia mtu, na siyo mtu kuitumikia mali! Mtu aliwekwa juu ya mali yote na aliagizwa kuitawala.

Kuukataa utajiri kwa sababu imeandikwa usisumbukie maisha yako ni ushindi mwingine kwa shetani. Sasa watu hawafanyi kazi kwa kisingizio cha kwamba Yesu Kristo alisema tusiyasumbukie maisha. Hivi Yesu angekuwa na maana hiyo Mtume Paulo angesema asiyefanya kazi na asile? Kufanya kazi siyo

kusumbuka na maisha. Kazi ni uhai alisema Nyerere. Yesu mwenyewe alikuwa fundi seremala sembuse wewe?.

Hoja ya msingi ni kwamba katika kila jambo tumshirikishe Mungu na kumtanguliza yeye. Kazi bila Yesu inaweza kukujeruhi, unaweza kupata kazi itakayokupeleka jela, unaweza kununua nguo zitakazosababisha kifo chako zikishika moto, unaweza kununua gari likakuua wewe na familia yako, unaweza kujenga nyumba ikakuua. Maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote" , ni maneno matakatifu kutoka Yohana 15:5b.

Wenye fikra za kitajiri wanatembea na maandiko haya, "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu" yanapatikana katika Wafilipi 4:13. Kwa hiyo Yesu anaposema msisumbukie maisha yenu alikuwa na maana ya …utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa...na kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi; Bali mkikataa na kuasi mtaangamizwa kwa upanga; maana kinywa cha bwana kimenena haya. Tunapigwa na umaskini kwa sababu ya uasi wa agizo la Mungu. Unasema umeokoka na kumpenda Bwana halafu hata nauli ya kurudi nyumbani baada ya ibada hauna. Unategemea kuomba nauli kwa wapendwa ili wakunyime uwakemee. Yaani na ulokole wako hujui lolote zaidi ya kukemea. Kuwa na fedha nyingi au kidogo siyo dhambi, kwa kuwa fedha ni mali ya Mungu (Hagai 2:8).

1. Ibrahimu alikuwa tajiri aliyebarikiwa katika vitu vyote (Mwanzo 13:2).

2. Ayubu kipenzi cha Mungu alikuwa tajiri (Ayubu 1:3).

3. Yusufu wa Arimathaya, mwanafunzi wa Yesu aliyelitoa kaburi lake jipya ili azikiwe Yesu, alikuwa ni tajiri (Mathayo 27:57-60).

Shetani anafahamu mkristo safi akiwa na fedha za kutosha, atammaliza kwa kuhubiri injili, kujenga makanisa na kununua vifaa vya muziki na hapo shetani hata pumua. Unadhani nani atajenga kanisa kama siyo mkristo? Kumbe furaha ya shetani ni kuzinyofoa akili za kondoo ili wafe maskini.

Jamani wokovu si kwenda tu Mbinguni; bali kutoka kwenye matatizo ukiwa hapa duniani. Yaani ule mema ya nchi. Sasa usipoyala hapa utayala wapi? Hata Petro aliposema Bwana niokoe pale baharini unafikiri alikuwa anataka kwenda Mbinguni? La hasha! Yeye alitaka aokoke asizame katika maji ili aendelee kula mema ya nchi.

Usiwe kama mbwa amka ukafanye jambo. Kuna mbwa aliyekuwa amelala chini, anabweka na kutoa mlio wa kulalamika. Mpita njia akamuuliza mwenye mbwa: mbona mbwa wako anatoa sauti ya kulalamika? Mwenye mbwa akajibu amelalia msumali. Mpita njia akauuliza kwa nini asiamke? Ndugu yangu kuendelea kulalamika kwa matatizo uliyonayo badala ya kuinuka na kufanya kitu haitakusaidia.

Amka kaitafute kweli.

## Sura ya 12

# Ushirikina ni Nini?

Ushirikina ni ile hali ya kutamani kufa kwa sababu ya mafanikio ya wenzako. Unawakunjia moyo kwa mafanikio ambayo hukuchangia hata senti tano. Badala uwaulize walifikaje huko na wewe ufike unaulizia jinsi ya kuwashusha ili mkose wote. Huo ni ushirikina. Yaani una roho mbaya hadi umekuwa mfupi! Mtu anajenga nyumba, wewe tumbo linauma, ajabu kweli! Hutaki wengine wapate kwa sababu na wewe huna. Ushirikina huu ndo hufanya matajiri kufa na utajiri wao. Hawaamini hata kuwarithisha watoto wao. Tajiri anakufa na utajiri wake wote na kuwaachia watoto historia ya utajiri wa baba. Utaskia dingi alikuwa na mawe achaa! Asingededi sijui tungekuwa wapi! Ushirikina siyo hadi kubeba matunguli na kwenda kuroga. Hata kutaka kuwa tajiri peke yako ukoo mzima ni ushirikina!

Ushirikina ni ile hali ya ndugu akipata atahakikisha ndugu zake maskini hawalali njaa. Anajiona ni wajibu wake kuwalisha badala ya kuwapa mbinu za kujilisha. Siyo wajibu wake kabisa kufundisha namna ya kuvua samaki kama yeye! Lengo lake waendelee kumpigie magoti na kumtukuza! Halafu hao ndugu zake wanapolishwa wanadhani wameukata kumbe wamekatwa. Huo siyo ukarimu ni ushirikina kwa sababu ukifa ndugu zako watakufa mara mbili. Kama unawapenda wafundishe kuvua samaki usiwape samaki.

Katika familia ya watu kumi anasonga ugali mtu mmoja, wanakula watu mia. Ukiuliza nani alileta unga, dagaa, mafuta ya kibaba na kuni utaambiwa ni baba mwenye nyumba. Hao wengine wanafanya nini? Bora mama amepika. Haya ni matumizi mabaya ya rasilimali watu. Tuwajengee watu wetu utamaduni wa kufanya kazi. Watu ni mali tusiwape ugali wa bure tu.

China wamesomesha vizuri watu wao na kuiuzia dunia, wanafanya kazi na kujena uchumi wao. Wachina wako kila kona ya dunia. Kama hawajengi barabara basi wanachezesha kamali. Tunaita kubeti. Sisi tunafuga kundi la watu wasiozalisha chochote, lakini wanakula tu. Kila mwafrika mwenye kibarua nyuma yake anamsururu wa watu anaowalisha. Mshahara ni wako lakini huufaidi, wanafaidi wengi.  Huu ni ushirikina!

Ushirikina ni ile hali ya kuchezea simu wakati wa ibada; ushirikina ni kukimbia nje kupokea simu wakati wa ibada; ushirikina ni kuchelewa ibadani na kutaka ukakae siti za mbele ili wakuone ulivyovaa vibaya; ushirikina ni kusinzia wakati wa ibada utadhani usiku ulikesha; ushirikina ni kunong'onezana wakati wa ibada hadi; ushirikina ni kukaa bila sababu za msingi wakati wa kusifu na kuabudu;ushirikina ni kuangaliaangalia saa wakati mahubiri yakiendelea; ushirikina ni kuondoka kabla ibada haijaisha; ushirikina ni kukusanyika nje wakati wa ibada kujadili maisha ya watu.

Ushirikina ni ile hali ya kuwapiga mizinga jamaa zako kila siku na wala hujawahi toa ofa, ukipata hela husemi uko kijiwe gani, ukiishiwa unawasumbua wezako wakunyweshe. Utaskia, "Wakuu! Wapi leo? Wakurugenzi leo sina maisha mjue?" Ushirikina ni ile hali ya kuwakwepa wanaokudai. Pesa yangu

halafu unaniambie nikukumbushe. Huu ni uchawi. Wachawi wana kiburi kama wewe.

Ushirikina ni ile hali ya kutongoza wachumba na wake za rafiki zako kwa sababu huna adabu. Leo hii kuna watu wamefunga ndoa na wachumba za marafiki zao. Ushirikina huu ndo unakufanya usiaminike. Sema hujui tu. Habari zako hadi boss wako anazijua! Vijana msifanye hayo bana!

Ushirikina ni ile hali ya kusubiri mkeo akupeleke ustawi wa jamii ndo utoe hela za kulisha watoto wako mwenyewe. Wanaume wa namna hii wanaamini kila mtoto huzaliwa na bahati yake, hivyo hawajishughulishi sana kuipanga kesho ya mtoto huyo. Wanachojua ni kuzaa hovyo kila mtaa na sio kulea. Atalea Mungu. Ushirikina wa namna hii ndo umefanya waafrika wengi kuwa na uoni hafifu kuhusu kesho. Wengi hatuangalii kesho na kesho kutwa. Tunaangalia leo. Ni nadra sana kumkuta mwafrika mwenye malengo ya namna mjukuu wake ataishi.

Ushirikina ni ile hali umezidishiwa chenji hakafu unaipangia bajeti hela ya watu badala ya kuirudisha. Huo ni wizi! Ushirikina ni ile hali ya ukipewa ofa unataka kunywa Saint Anna na wakati tunakujua kinywaji chako ni Balimi! Huku ni kuwakomoa wenzako!

Ushirikina ni ile hali ya kupambana na kila anayekukosoa ukidhani anakutafuta. Kama hutaki kukosolewa usifanye lolote, usiseme lolote ili ufe si chochote, ingawa hata ukifa tutasema marehemu ameacha historia fupi sana, alizaliwa, akazurula, akafa Amina! Kumchukia anayekukosoa ni sawa na kuvunja kioo kwa kukuonyesha tongotongo machoni. Watu wakigundua hupenzi

kukosolewa, watakusifu hadharani na kukuteta mafichoni. Utasikia, “ana sura nzuri tatizo miguu!! Tukosoane tusitetane. Sikiliza, kuwa na kasoro ni sehemu ya ubinadamu, kukubali kuwa una kasoro ni uungwana, kujirekebisha kutokana na kasoro ni ushujaa na kuelimisha watu kwa ulichojirekebisha ni ukarimu.

Ushirikina ni kuponda ndoa za mitaala na mpango wa kando ndo habari ya mujini. Watanzania wanaita nyumba ndogo! Huwa najiuliza mzungu aliwezaje kutukamata katika hili la kwamba ndoa za mitala ni dhambi? Mzee wa Upako anasema ndoa za kikristo hazidumu kwa sababu ya kiburi cha kuoa mke mmoja.

Ushirikina ni ile hali ya kuona maovu na kuyafumbia macho kwa kuogopa kupoteza ugali. Wewe ni sawa Graduate anayesema anaogopa kuoa mwanamke msomi halafu anajiita mwanaume. We are trapped in stupidity prison. Kwa uoga huu tunakwepaje kuzalisha maskini wa kutisha?

Ushirikina ni ile hali ya kuamini kila tajiri ni mwizi hivyo lazima ashughulikiwe. Tabia hii hufanya watu waogope kusaka utajiri. Hapa uchumi utainukaje? Maana ukichapa kazi kwa bidii tegemea kurogwa na ukinusurika kurogwa basi tegemea kupambana na watoza kodi. Kodi Afrika hazilipiki. Ni rahisi kulipa rushwa kuliko kodi Afrika. Kodi imekuwa kero badala ya kuwa nyenzo ya maendeleo. Ukisema ulipe kodi kama inavyotakiwa utaumia sana. Kodi zimekuwa kubwa kuliko faida. Kwa hali hii afadhali kulima mahindi unywe uji na wanao siku zisonge mbele mkafe salama bila ugonjwa wa moyo.

Ushirikina ni ile hali ya kuamini kingonzi bora lazima awe maskini. Ukiwa tajiri unaambiwa wewe hufai ni fisadi. Katika

ushirikina wa namna hii watu watapambana kuwa maskini ili wawe viongozi. Utakuaje na mabilionea wengi? Waafrika imefikia sehemu tunafurahia umaskini na kuchukia utajiri. Umaskini siyo sifa. Maana kila mtu akianza kuelezea historia yake utasikia, “Msinione hivi! Nimepitia shida mimi acheni. Tumelala njaa sana home” Sasa sikiliza mwenzake. “Hunishindi mimi. Mimi nimekula ugali pilipili. Nimekwenda shule kwa mguu halafu peku. Sasa hiyo ni sifa? Tajiri akibanwa tunafurahi kweli. Eti wote mkiwa maskini mtaheshimiana. Huu kama siyo ushirikina ni nini? Acha niendelee kuuza vitabu ili watoto wangi wasije kuupa heshima umaskini.

Ushirikina ni ile hali ya kutaka kuishi maisha ya wengine na wakati ya kwako tunayajua. Unalazimisha kuzaa mapacha na wakati mimba ni moja. Bure kabisa! Unamuigizia nani sasa? Umeona tajiri anapeleka watoto wake shule kwa taxi na wewe unaamua kuwapeleka kwa watoto wako shule kwa bodaboda ili walingane na watoto wa tajiri na wakati huwezi kumlisha wala kumtibu vizuri. Hizo pesa za boda si bora ungemtengenezea lishe nzuri mwanao? Tunawaua watoto kwa nimonia kisa tuonekana tunazo! Eti medium school! Kweli ujinga na ujuaji pasipokujua ni watoto pacha uzao wa pili wa shetani!

Ushirikina ni ile hali ya kusema tuko nyuma yako lakini akigeuka hakukuti. Huu ni usaliti! Mtu anakuletea kadi ya mchango wa harusi ya mwanaye unampa mahope kwa kusema tuko pamoja lakini hadi harusi inapita hukutoa mchango!

Ushirikina ni ile hali ya kutoa majibu mepesi kwa maswali magumu. Utasikia kila anayemuunga mkono Rais anatafuta

uteuzi. Sasa Rais atateua watu wangapi? Huu nao ni ushirikina wa akili.

Ushirikina ni ile hali ya kutaka kujibu kila ulilolisikia na kuishia kuwapa umaarufu wajinga, na wakati mengine yalihitaji ukimya tu. Akushindae kuongea, mshinde kunyamaza. Kumtupia mawe kila mbwa anayekubwekea njiani utachelewa kufika unakokwenda. Kubweka ni tabia ya mbwa. Kuna watu wanatabia ya mbwa. Wanabweka muda wote.

Ni sawa unaenda ugenini halafu unasikia wanasema hapa hatujawahi kuibiwa kitu. Ukisikia hivyo ndo utaelewa kwa nini Biblia inasema kuna wakati wa kunyamaza na wakati wa kusema. Hapo ukisema tu siyo mimi basi watajua ni wewe.

Ushirikina ni ile hali ya kukazana kufuga ndegu na wakati wenzako wanafuga kuku, halafu ukienda likizo unataka wakuchinjie kuku! Umekuwa watu wa Dar? Watu wa Dar wakisikia unatoka Mwanza wanakwambia uje na samaki utadhani samaki wanaokotwa njiani! Wasisikie uko Mbeya sasa mwe! Utasikia bro, usisahau kutuletea mchele wa Mbeya, unanukia vizuri. Yaani wanadhani ukifika Mbeya ni kuzoa mchele tu kama mchanga! Watu wa Dar bwana!

Ushirikina ni ile hali ya kutengeza six parks na wakati wenzao wanatengeneza six cars, wanatajirika!

Ushirikina ni ile umekazana kukuza shape na wakati wenzako wanakuza kipato.

Ushirikina ni ile hali ya kudhani usomi ni kuzungumza Kingereza kwa mbwembwe kama Wakenya. Kuna wazazi wanawakomalia watoto wao wazungumze Kingereza nyumbani wao hadi unajiuliza ni nini hasa wanataka kukuonyesha: kwamba mtoto hajui Kiswahili? Tumekuwa wajinga wa kupindukia. Hivi sasa tunazo shule nyingi kote nchini ambazo zimekazana kuwafundisha wanafunzi kwa kutumia lugha ambayo walimu na wanafunzi hawaielewi, na wala haitatokea siku wakaielewa.

Ushirikina ni pale unapokutana na msomi kaipora nchi. Wazungu wakwambia njia nzuri na rahisi kula vya Afrika ni kuwatumia Wasomi wa Afrika. Yaani Mwafrika kila anavyozidi kupata elimu, ndivyo anavyozidi kuwa mbinafsi na mwizi. Nchi nyingi za Afrika zinalalamikia mikataba mibovu iliyosainiwa na wasomi.

Wafrika wanaweza kukwambia fungua biashara tutakuunga mkono lakini ukiishafungua huwaoni. Hawa dawa yako ni kuwafanya kama Msumkumaa alivyowafanyia wale mabahiri. Msukuma alifungua Zoo ya wanyama kwa kiingilio sha Sh 10,000, hakuna aliyeingia. Akashusha hadi Sh 5,000 pia hakuna aliyeingia. Akashusha tena hadi Sh 2,000, hakuna aliyeingia. Akashusha hadi Sh 1,000 pia hakuna aliyeingia. Akafanya bure, watu wakajaa hadi walikosa pa kukanyaga. Akafungulia simba mmoja na kutangaza bei ya kutoka nje ni Sh 20,000. Wote walilipa, msukuma akatajirika zake kwa kutumia akili. Akili inalipa! Tuacheni ushirikina ili tupate tuishi!

**Sura ya 13**

# Maisha ni Kitendawili, Kitegue Uteguke!

Katika mapenzi na ndoa tunawaacha wanaostahili kuvumiliwa na tunawavumilia waliostahili kuachwa matokeo yake ndoa zimekuwa ndoano na mapenzi yamekosa utamu! Binti yangu siku hizi meno huna, moyo unavuja damu, nuru usoni iliishatoweka, makalio yameshuka, mashavu yamelegea, ukivaa hupendezi tena kama za mani, umeharibika kwa sababu ya ndoa. Umeshindwa kutoka kwa sababu umeambiwa ndoa ni uvumilivu na kweli umeamua kuvumilia visivyovumilika! Hakika ndoa ni kitendawili kigumu kitegue uteguke.

Katika kufa na kupona, wanakufa waliostahili kuishi na wanaishi waliostahili kufa kitambo! Wezi, majambazi, vibaka na wahuni wanaofanya maisha yakose maana wanaishi miaka mingi na heri duniani. Imagine, umejinyima hadi ukanunua simu ya tachi ili na wewe ukachat majanga mitandaoni, unaamka asubuhi kibaka kapita nayo, huyo unadhani alistahili kuishi? Huyo alitakiwa kufa. Unaitesa familia yako hadi watoto wanaulizana hivi baba naye atakufa lini? Unakuja kushangaa wanakufa wanaotunza familia zao vizuri, wanabaki washenzi. Hiki ni kitendawili siyo kitendawili? Kama ni kitendawili kitegue!

Katika kazi na utumishi wanapandishwa vyeo waliostahili kufukuzwa kazi na wanafukuzwa kazi waliostahili kupandishwa vyeo. Kuna watu kazini wanaiba kweli lakini wanahamishwa na

kupata promotion, wengine ni wachelewaji, ufanisi sifuri lakini kwenye teuzi wamo na wale wachapakazi wakikomaa na nafasi zilezile utadhani walichanjia. Hii imekaaje? Kuna watu kila ukitembelea ofisi fulani wapo, ukisafiri ukirudi wapo, ukienda masomoni ukirudi wapo, wamekaa ofisini hadi mabosi wanapanga namna ya kuwatimua kazi au kwenda kuwaficha vijijini kabisa. Promotion hupati, likizo huendi, kituo cha kazi huhami pamoja na uchapakazi kwa bidii hadi umeamua kumuachia Mungu! Hiki kama siyo kitendawili ni nini?

Katika lishe na matunzo tunawalisha waliostahili kujilisha na kuwacha waliostahili kulishwa kwa sababu imeandikwa aliyenacho huongezewa na asiyekuwa nacho hunyang'anywa hata kile kidogo alichokuwa nacho. Yaani mbuzi wa maskini hazai, akizaa anazaa dume. Ukiishakuwa Rais wa nchi, waziri mkuu, na vyeo vingine vyenye mishahara na marupurupu manono jiandae kulishwa hadi kufa kwako, tena unalishwa kwa kodi ya maskini! Hawa unaanzaje kuwalisha na wakati vyeo vyao ni utajiri tosha? Maisha bana! Tunawabeba wasiobebeka na kuwaacha wanaostahili kubebwa.

Katika shule na mitihani wanafaulu waliostahili kufeli na wanafeli waliostahili kufaulu. Kuna wakati matokeo yakitoka hadi mnajiuliza hadi cha pombe kafauli? Yaani Braza K amezungusha pamoja na kukesha anasoma kama bundi? Yaani na Zuhuru Mlala Club amepita! Maisha bro yaache kama yalivyo, ukiendelea kuyafuatilia utaumia.

Katika ndoa na uzazi; wanabeba mimba waliostahili kunyimwa uzazi, wanakosa uzazi waliostahili kuzaa. Kuna watu hawahitaji ujauzito kabisa lakini kila akijaribu ana nasa na kwenda kutoa

mimba, kesi za utoaji mimba ni nyingi, wengine wanajifungua na kutupa vitoto chooni na wakati kuna wangine wamehamia hospitali kabisa kwa bed rest ili mimba isiharibike, wanarest miezi tisa, anazaliwa mtoto anakufa siku kesho! Hii nayo unaidefine vipi?

Katika umaskini na utajiri, wanatajirika waliostahili kufa maskini na wanakufa maskini waliostahili kutajirika! Mtu anakesha akipiga kazi lakini bado anaishi kama digidigi, wahenga wakasema hard workers die poor, smart workers die rich, wengine wakasema aliyekupa wewe ndo kaninyima mimi, jamani! Hakika maisha ni kitendawili, tenda unavyoweza usijekufa kwa presha bure!

Katika kuoa na kuolewa wanaolewa wasiostahili kuolewa, waliostahili kuolewa hawaolewi kabisa kwa sababu maisha hayana adabu. Kuna watu wanachezea ndoa na kuishia kusema kweli penye miti mingi hapana wajenzi. Umepewa kila kitu lakini miguu haitulii nyumbani, unawashwa! Ungejua wenzako wanavyoitamani ndoa hiyo.

Katika sifa na utukufu wanasifiwa waliostahili kuadhibiwa, wanaadhibiwa waliostahili kusifiwa; wanapendwa waliostahili kuchukiwa na wanachukiwa waliostahili kupendwa. Unaweza kusema ni kwa sababu wanajipendekeza kumbe watu na bahati zao! Utaskia msichana mrembo ila kwa kuomba hela unawashinda hadi walemavu. Jamani! Shida ni nini hadi wasikupende na urembo wako?

Katika siasa na uongozi; wanachaguliwa wasiostahili kuongoza, wanaostahili kuongoza hawachaguliwi. Kuna viongozi

wakisimama na kuanza kujenga hoja mtatamani kuingia chini ya viti, ukija kwenye utendaji ndo balaa kabisa utadhani wametoka ukoo wa shetani!

Maish Bwana! Kuna jamaa aliniambia maisha yakikuzingua achana nayo! Nikamwambia huna akili, yaani nife? Kuachana na maisha si kufa?

# Sura ya 14

# Siri ya Jogoo Katika Maisha

Dunia ina mengi, zembea kuyajua maisha ya kumudu! Uamuzi ni wako! Hata Mungu alivyotupa akili alituachia uamuzi wa kuzitumia. Ukiamua kuzitumia akili zako kulala, sawa yeye atakulinda usingizini ili uvune umaskini wa kukutosha, ukizitumia akili zako kuchapa kazi atakubariki hukohuko kazini hadi ushangae mwenyewe!

Hebu tushirikishane mengi ya huyu kuku dume, yaani jogoo kwa lugha tamu ya Kiswahili na rooster kwa lugha chungu ya mkoloni, lugha ambayo ukiizungumza vibaya watumwa wanakucheka! Bure kabisa.

Kwanza kabisa kuna mtu akisikia neno jogoo anawaza supu, mwingine anawaza chips kuku. Lakini mtu huyohuyo ukimwambia jogoo anatoa nuksi, jogoo ni mlinzi wa nyumba, jogoo huleta bahati, jogoo hutibu nguvu za kiume, atakwambia ushindwe na ulegee kwa Jina la Yesu na wakati Yesu mwenyewe alimtumia Jogoo kuthibitisha usaliti wa Petro. “Kabla jogoo hajawika leo, utanikana mara tatu!” na kweli Petro akamkana mara tatu!

Unaita ushirikina na wakati makanisa ya kale yalitumia nembo na minara ya jogoo kabla Emperor Constantine hajaja na msalaba wa Mungu wake Tamus kwa sababu waliijua siri ndani ya jogoo.

Wewe ukiona jogoo unawaza chips kuku na wakati wachina wana hadi mwaka wa jogoo kwa sababu wanazijua baraka zake, wewe unawaza nyama na wakati wajapani wanamuona jogoo kama messanger wa Mungu.

Jogoo ni hazina ya wachawi kwani humtumia kurogea watu, jogoo ni nguzo ya wafaransa ndo maana hadi kwenye geti la Ikulu yao Élysée Palace ina chata ya jogoo, timu ya Tottenham inafahamu siri ya jogoo hadi kuifanya kuwa nembo yao, kule Irani jogoo ni mjumbe wa Mungu, Bendera ya KANU inapicha ya jogoo pengine ndo maana Moi aliwika kama jogoo maisha yake yote, klabu ya michezo ya Uturuki ya Denizlispor inachata ya jogoo.

Orodha ni ndefu tuikatishe ili tuangalie mambo kumi kuhusu jogoo! Nazungumzia jogoo wenyewe acha haya machotara yanayokua kwa sindano na madawa kama binadamu sidhani kama yana akili. Uliona wapi kuku anaota moto na kutandikiwa pa kulala kabisa? Hayo tuachane nayo! Tudili na jogoo asilia!

**Moja: Jogoo huondoa nuksi!**

Wazungu, wahindi, wachina na wajapani wanasema jogoo anapowika hufukuza, wachawi mapepo, mikosi, nuksi balaa na mashetani yaliyotawala usiku ndo maana ni hatari kuamka kabla jogoo hajawika. Nadhani knowledge hiyo hata babu zetu

walikuwa nayo ndo maana kila familia ilifuga kuku, siku hizi kila familia inafuga ndevu na nywele! Bure kabisa!

Warus wanakwambia kabla ya kuingia kwenye nyumba mpya au nyumba ya kupanga hakikisha jogoo analala humo kwanza ili akiwika aondoe nuksi, vinginevyo ndoto za ajabu zitawasumbua, utakuwa kama yule bwana aliyeota anajifungua, kuamka asubuhi akakuta kajisaidia kitandani, mke akamnasa kibao, ndoa ikaishia pale.

Lakini pia kuna nyumba ndo ilikuwa ya kufanyia ufuska na watoto wa shule na wake za watu, ukihamia bila kufukuza nuksi mambo yako lazima yaende hovyo, ulikuwa na pesa inapotea, mlipendani mnaanza kutwangana, magonjwa ndo kila siku, kila kitu kinasimama, kuibiwa ndo usiseme, full nuksi utadhani guest za uswahilini, ukilalemo lazima uliwe kichwa.

Waislamu wanashauriwa kufuga jogoo mweupe nyumbani ili shetani na wachawi wasifike kwenye nyumba zao. Soma, Mu’jam Awsaṭ, Uk. 1201, vol. 1 na pia Ḥadīš 677. Lakini pia ni mwiko kwa muislamu kumdharau jogoo kwa sababu ndo huwaamsha kwenda kuswali alfajiri na mapema. Wanaamini kwamba ukisikia jogoo anawika kamuona malaika, ukisikia anakoroma kaona shetani, muombe Allah akulinde.

**Mbili: Jogoo huleta bahati katika biashara na kazi**

Huko Ujerumani, Slovakia na Bulgaria kabla ya kuanza kilimo wanachinja jogoo ili wapate mazao mengi. Hii ni kafara ya wazungu, ukiifanya Afrika wanasema ni chukizo mbele za Mungu, tumefundishwa hivyo. Lakini kafara ya uchinjaji ndo

sadaka kubwa kuliko sadaka zote. Hata wana wa Israel walipochinja walitoka utumwani. Kama mambo yako yanagoma jaribu na sadaka ya kuteketeza uone!

Wazungu, wahindi na wachina huweka alama ya jogoo kila wanapoanza kazi mpya ili waifanye kwa ufanisi. Ukiamka asubuhi unakuta madaraja yamesimama. How? Sisi tunakwama wapi? Mbona tuna majogoo mengi tu Afrika? Kwa nini tuendelee kuwaachia wachawi kutumia majogoo hayo kurogea? Afrika ukimuona kuku kwa mganga, jua rangi yake ndo imemponza. Waganga wetu wanatufundisha kutumia jogoo kuwaona wachawi live sijui ili iweje sasa?

Wazungu na wachina hadi leo wanaamini jogoo akiingia jikoni ujue ni mwaka wa neema, wewe jogoo akiingia jikoni unamtimua kwa mawe na viboko. Wanasema jitahidi basi jikoni usikose hata kifaa kimoja chenye chata ua picha ya jogoo. Yapo masufuria, visu, na majiko yenye chapa za jogoo. Lakini pia wanaamini ukitumia vifaa vyenye chata ya jogoo unajiongezea neema. Wajapani, Wafaransa na Wareno hutumia alama ya jogoo katika vitu vyao vingi kama mabati, majembe, pasi za mkaa, masufuria na panga. Hakuna nyumba inayoweza kuwa na baraka bila jogoo, wanaamini hivyo Wayahudi.

**Tatu: Jogoo ni ishara ya umaarufu, ujasiri, upendo na heshima**

Jogoo ni mdogo lakini akiwika kijiji kizima kinajua. Maana yake ni kwamba jogoo anaweza kukupa umaarufu kijiji kizima na duniani pote. Kama unahitaji cheo na jina lako livume kama anavyo vuma jogoo kwa kazi yako jogoo ndo jibu. Jogoo

anaweza kukufanya jasiri kutoka na ujasiri wake wa kupigana bila kuchoka. Jogoo anaweza kumua chatu. Wakorea wengi wanatumia tattoo ya jogoo kwa sababu ya uwezo wake wa kupigana hadi kufa bila kukata tamaa.

Jagoo anaweza kumfanya mtu mbaya kuwa mwema kutokana na hulka yake ya kuacha kuku wengine wale kwanza na yeye kuwa wa mwisho kula. Afrika mtu akikuheshimu anakuchinjia jogoo. Ukienda kutembea kwa mtu na jogoo mkononi hakuulizi utaondoka lini! Habari za mgeni siku ya kwanza, siku ya tatu mpe jembe akalime hazitokei kwa mgeni aliyefika na jogoo!

**Nne: Jogoo huzuia watu kuzama majini**

Mabaharia wa kizungu na kichina wanaweka tattoo za jogoo kwenye miguu yao ili wasizame. Kama jogoo anavyoelewa kwenye maji na wao wanaelea tu.

**Tano: Dini zote zinamkubali Jogoo!**

Jogoo katika ukristo ni ishara ya msamaha na kufufuka kwa Yesu Kristo ndo maana makanisa ya zamani yaliweka alama ya jogoo juu kama tunavyotumia misalaba leo hii. Wayahudi wanamuheshimu sana jogoo kwa sababu ndo humsifu Mungu kila siku kwa siku mpya. Huko Bolivia, wanaamini jogoo ndo alitangaza kuzaliwa kwa Yesu ndo maana wana ibada ya jogoo. Siku ya krismas jogoo huletwa kanisa kushiriki ibada.

Huko Bolvia Jogoo anapowika usiku wa manane anatukumbusha kuzaliwa kwa Yesu, sisi akiwika muda huo, kesho ni kisu. Lakini pia jogoo anawika ili kutukumbusha tutubu dhambi zetu. Biblia

inamtaja jogoo kama kiumbe mwenye akili sana. Soma Ayubu 38,36 katika International Bible.

Baada ya jogoo kuwika, Petro alijutia matendo yake! Kwa wakatoliki jogoo ni alama ya mwanzilishi wa kanisa! Jogoo ni Petro aliyemkana Yesu, akajuta na kusamehewa dhambi zake akaja kuwa Papa wa kwanza wa kanisa ndo maana pale Vatican kuna kanisa la ST. PETER'S BASILICA. Na kanisa hilo limejengwa juu ya kaburi lake na hiyo ndo chanzo cha maaskofu wakuu kuzikwa kanisani. Lakini pia sehemu hiyo ya kaburi la Peter ndo sehemu kuu ya wakatoliki kuhiji kote duniani. Kanisa lenyewe lilijengwa na Papa Julius II mwaka 500 na kitu nadhani. Papa Gregory I ndo alitangaza jogoo kuwa ishara ya ukristo na alama ya Mt. Petro.

**Sita: Jogoo hutoa ishara ya hatari ili watu wachukue tahadhari**

Katika nchi za Babylon, Irael, Misri, Iran, India, China, Amerika, na nchi zote za Skandinavia, wanaamini jogoo anapoona hatari huwika. Kama mko vitani jogoo akawika inabidi mjipange vizuri, akiwika usiku hata saa mbili usiku, kaa chonjo, kuna jambo linakuja, anawataarifu mjiandae namna ya kukabiliana nalo!

Wajapani wanamuona jogoo kama mjumbe wa Mungu. Akipita mchawi nyuma ya nyumba yako, Jogoo anakwambia, kwa sauti ya chini kama anaunguruma hivi. Siku hizi maovu ni mengi ndo maana jogoo wanawika bila kufuata muda. Hata kuchati chati na hawala zako umelala na ndoa yako usiku jogoo hapendi. Akiwika kagua simu ya mume wako ili mdundane. Unaposikia sauti ya jogoo ndotoni jua kuna mambo hujayatekeleza amka ukayafanye.

**Saba: Jogoo huzuia moto**

Nchi nyingi za Ulaya, Marekani na Asia wanaamini jogoo anauwezo wa kuzuia moto ndo maana kwenye milango ya nyumba zao huchora picha ya jogoo mwekundu. Huku kwetu jogoo mwekundu ni mzuri kwa kurogea watu. Lakini pia wanachora picha ya jogoo mweupe mlangoni kuilinda nyumba yako na nguvu chafu.

**Nane: Jogoo ni ishara ya haki, ukweli na usawa**

Kuna hadithi moja huko Ureno, bwana mmoja alisingiziwa kaiba hivyo akauhukumiwa kunyongwa. Jamaa akamwambia jaji aliyekuwa anajiandaa kula jogoo mezani kwake mkinifunga kitanzi shingoni mniue kwa kosa ambalo sijafanya, huyo jogoo atasimama na kuwika. Jaji akasema kwenda zako mbuzi wewe. Jamaa akasema haya, ninyongeni! Walivyofunga kamba ile wanataka kuvuta yule jogoo akasimama kwenye sinia na kuwika. Jaji akakimbia! Kifo kikaahirishwa, jamaa akaondoka zake! Hadi leo Wareno wanamtumia jogoo kama alama ya haki na usawa katika jamii.

**Tisa: Jogoo hutibu nguvu za kiume**

Jogoo ni dawa ya nguvu za kiume. Chukua korodani za jogoo, zichome vizuri kisha na kausha juani, saga halafu anza kulamba, utaniambia kama mama yoyo hajakukimbia! Korodani za jogoo ziko ndani, eneo kati ya upaja na mbavu za mwisho upande wa juu wa uti wa mgongo karibu na figo.

## Kumi: Jogoo ni kinga ya balaa

Wayahudi na Wahindi wanasema unaweza kumtwika jogoo mizigo yako yote. Piga sala Kapparot. Wayahudi walifanya hivyo kabla ya ile vita ya Waisrael na Waraab, Warabu wakaliwa kichwa mapema. Soma Vita ya Yom Kippur. Sala yenyewe iko hivi. Wanasoma Isaya 11:9, Zaburi 107:10, 14, na 17-21, na Ayubu 33:23-24, kisha wanachukua jogoo, halafu anazungushwa kwenye kichwa cha mlengwa mara tatu, kisha wanasema, “This is my exchange, my substitute, my atonement; this rooster shall go to its death, but I shall go to a good, long life, and to peace, " ngoma imekwisha.

# Sura ya 15

# Mambo Kumi Kuhusu Mikopo

Mikopo huamsha akili. Kama hudaiwi akili inalala! Mwanaume bila madeni akili haikai sawa. Naskia ukienda kuoa uchagani lazima wakuulize kama una madeni, ukisema hauna, unakosa mke. Halafu kuwa na madeni ni ishara wewe unaaminika! Lofa hakopesheki! Lakini pia wapo walioapa kutorudia kukopa maana walitendwa na mikopo wakatendeka. Watu wa namna hii wako wengi. Hawajui mambo mengi kuhusu mikopo, ngoja niwape mambo kumi tu!

**Moja** ni hulka ya binadamu kuogopa madeni kuliko mikopo ndiyo maana kukopa harusi kulipa matanga. Mtu yuko tayari hata kudanganya ili tu apate mkopo. Sikiliza swaga za mswahili anavyokopa, “Kaka vipi, shwari? Dah, hatuonani mzee, mishe vipi, mnatunyima nini? Juzi nimekuona kwa mbaaali… mzee shavu dodo, full kipupwe! Sie tupo bwana, shida tu, alafu misiba mingi mingi kweli, wife naye kajifungua ghafla. Sasa, kuna cheque naisubiri haijatoka hadi leo, wanasema itatoka next week, hapa nimekwama kweli. Naweza pata 'Laki Moja' ya karibu hapo nitarudisha mwisho wa mwezi?” Mpe hiyo laki uone sasa! Eti mke kajifungua ghafla. Huyu bwana ukimpatia mkopo lazima urafiki ufe! Hawezi kukulipa!

**Mbili**, watu wengi kurukwa na akili wanapopata mkopo na akili kurudi pesa ikiisha. Hakuna kipindi hatari sana kama kipindi cha

kufuatilia mkopo. Watu watafoji mpaka wazo la biashara, watafoji malengo ya mkopo, watafoji hata namna ya urejeshaji, watafoji utaratibu wa kupata mkopo hata kwa kuahidi ten percent kwa afisa atakayeprocess mkopo utoke mapema. Ni kipindi ambacho mtu anaweza kukopa shilingi laki tano kwa dhamana ya gari au nyumba ya milioni 50. Hapa akili ya kufanya pembuzi yakinifu ili kujua riba kiasi gani, dhamana ni nini, atalipa kwa muda gani, kivipi haipo. Pesa ikitoka atabadilisha hadi ratiba na aina ya chakula kwa hela ya mkopo. Akianza kudaiwa ndipo akili inarudi na kuanza kutukana watoa mikopo na kuwatishia watu wasichukue mikopo. Mkopo siyo mbaya kama unajua sababu ya kuuomba.

**Tatu**, dawa ya deni kulipa na si kuponda. Uzoefu unaonyesha kulipa siyo tabia ya wengi. Siku moja Mwalimu akawauliza wanafunzi wake, “Baba yako akikopa shilingi 5,000 kwenye duka la Mangi halafu akaenda kukopa tena shilingi 5,000 kwenye duka la Masawa. Je! Atarudisha shilingi ngapi kwa pamoja?” Mwanafunzi akajibu,“Harudishi kitu.” Mwalimu akajua mwanafunzi hakulielewa swali, akarudia tena kuuliza, lakini mwanafunzi akajibu vilevile! "Hatarudisha kitu". Mwalimu kwa hasira akasema, “Kaa chini! Hujui kitu”. Mwanafunzi akasema, “Wewe ndo humjui Baba Yangu. Baba akikopa huwa halipi.” Lipa mkopo wa watu uache ukorofi, kumbuka hakuna vitu vya bure duniani.

**Nne**, siyo kila anayetamani kuwa tajiri ana mpango wa kuwa tajiri kwa hiyo usifikiri kila mtu anakopa kwa ajili ya kuzalisha. Mwingine anakopa ili akaoe, mwingine akanunue gari la kutembelea, mwingine anakopa ili akawatunze wenzake siku ya kitchen party, mwingine anakopa ili akahonge, mwingine

anakopa ili aishi kabla hujafa! Labda ni kwambie usipozingatia mambo ya msingi kabla ya kukopa, mkopo hugeuka kero. unaweza kukuvunjia ndoa, undugu, urafiki na kusambaratisha kabisa mahusiano yaliyodumu kwa muda mrefu. Siku hizi wanaume wengi wamejikuta kwenye janga la kulipa madeni ya wake zao, yanaitwa vikoba!

**Tano**, ni vigumu sana kukopa kwa ajili ya kuanza biashara na ukatoka. Kumbuka hakuna biashara inayoanza na kutengeneza faida. Wakati huo kumbuka mara baada ya kuchukua mkopo inabidi uanze kulipa, labda kama unategemea kulipa kwa kutumia mshahara na siyo biashara sawa. Kopa ili ukaendeleze biashara na si kukopa ukaanzishe biashara! Hayati Reginald Mengi anakwambia ukitaka kuanzisha biashara tumia nguvu ulizonazo kama mtaji. Hata benki hazikopeshi mtu anayeanza biashara, ndiyo maana lazima waangalie hali ya biashara yako. Sasa we wadanganye benki wakupe mkopo ukuue! Mtu mmoja alijaza mchanga na takataka kwenye duka la dawa muhimu ili apate mkopo, bahari nzuri wakamgundua mapema. Sasa huyu angepewa mkopo siangekuwa mboga benki? Wangemla kichwa bila ugali!

**Sita,** mkopo ni kama mimba, unaanza kwa siri na kuishia hadharani pale utakapozingua kulipa. Wakati mtu anapata mimba hakuna anayeweza kuuliza lakini ikikuua utaskia, “Yesu na Maria, yaani hadi yule dada mpole kapata mimba!” Utadhani mimba wanapata watukutu tu! Unapokuwa katika harakati za kupata mkopo, kufoji nyaraka na kutoa maji kwa maafisa mikopo huwa ni siri yako, ukishindwa kulipa inakuwa siri ya wote!

**Saba**, uzoefu wangu unaonyesha ili ufanikiwe kibiashara lazima uwe na akili kwanza halafu fedha inafuata. Ni vigumu kuanza na fedha ukatoka, ingekuwa hivyo nchi ingejaa matajiri kwa sababu kuna watumishi walichukua mikopo sana wafungue biashara lakini wamepotea. Hawa walianza kupata pesa kabla ya kupata akili. Akili ni kuwa na mipango.

Jamaa mmoja anasimulia, "Niliwahi kumdhamini binti mmoja kupata mkopo baada ya kumuona ana akili ya biashara na ni mpishi mzuri sana, alikuwa anapika mama ntilie, chakula chenye hadhi huku akiuza na pombe kwa pembeni. Nikamdhamini apanue na kuboresha biashara yake hiyo. Baada tu ya mkopo kutoka akahama chumba kimoja na kupanga vyumba viwili, akamuongezea mchumba wake pesa ili anunue pikipiki ya kutembelea siyo ya biashara, ndani akanunua subwoofer na Tv. Kule katika biashara sanasana alinunua feni moja na viti sita. Huyo mchumba wake akawa anakula bure kutwa mara tatu lakini ile pikipiki akawa anatanua nayo mitaani akibeba mademu wengine.Migogoro ikaanza, biashara ikasambaratika, akashindwa kumaliza kulipa mkopo wake, kesi ikanigeukia mimi mdhamini wake."

Huyo binti hakuwa na akili! Akili ni pamoja na kujua ni biashara gani unayotaka kuifanya. Je, unaifahamu vizuri? Unachukua mkopo kwenda kufungua duka la kuuza masweta mazito kariakoo. Hapo ndo utajua kumbe ujinga na umaskini ni watoto mapacha na uzao wa kwanza wa shetani.

Lakini akili pia ni usimamizi wa biashara. Unakopa hiyo biashara anasimamia nani? Unakopa halafu unaweka mtu asimamie biashara yako wakati wewe upo ofisini? Hapo lazima nyumba

yako ipigwe mnada. Hakuna mtu atakayesimamia biashara yako wakati wewe unapita jioni tu kuchukua mauzo. Kufanya hivyo ni kuonyesha kwamba huna mpango na utajiri ingawa unaupenda. Chagua kukaa ofisini au kufanya biashara kwa sababu mshika mbili moja humponyoka.

**Nane**, ni vigumu kufanya biashara kubwa kwa kutumia fedha yako. Hata kama unayo unashauriwa utumie hela za wengine kuleta faida. Maskini hujiwekea akiba benki imfae kwa dhiki, tajiri anakwenda kuzikopa hizo hela za maskini ili zimfae katika utajiri. Tajiri ananunua daladala kwa pesa ya maskini iliyoko benki, ili aendelee kutajirika kupitia nauli za maskini. Hii inaitwa benefiting from poverty. Jamani twendeni tukakopeee. Kuwa na madeni ni ishara ya kuwa raia mwema alisema Ella Davide. It takes money to make money.

**Tisa**, usiogope kukopa kwa kutegemea miujiza, hukuna fedha inayopatikana kimiujiza. Haijawahi kutokea mtu akapata fedha bila kutumia akili, nguvu na maarifa. Kanuni mojawapo ya kibiashara inasema hivi, "Kwa kadri iwezekanavyo jitahidi uwe na deni na uchelewe kulilipa wakati huohuo uhakikishe unayemdai anakulipa mapema iwezekanavyo! Wenye pesa zao wanakopa, sio kwa vile hawana pesa, la hasha, wana malengo ya kibiashara zaidi.

**Kumi**, siku zote ishi kulingana na kipato chako na si mkopo wa watu, maana mkopo siyo kipato chako, hilo ni deni. Mkopo ukufanye kustrugle kuulipa kwa faida, "If there is no struggle, there is no progress," alisema Frederick Douglass.

# *Sura ya* 16

# Aina za Tatu Marafiki

Kama samaki anavyohitaji maji aweze kuishi ndivyo na sisi tunavyohitaji marafiki tuishi. Mtumishi wa Mungu T. D. Jakes wa Marekani anasema kuna aina tatu za marafiki; confidants, constituents na comrades.

1. **Confidants**

Hawa ni marafiki wanaokupenda bila masharti. Wako nawe katika kupanda na kushuka kwako, katika taabu na raha zako, katika utajiri na umaskini wako,  katika njaa na shibe yako. Ukifungwa watakuja, hawatapiga simu tu, ukilazwa watafika hawatatuma pesa za juice, ukihitaji dhamana watakuwekea bila kutangaza, ukiharibu kazini hawatakuaibisha mitaani, ukiishiwa hawatakukimbia, ukilia watalia na wewe.

Ni aina ya marafiki wanaokupenda kwa vitendo na shilingi na si kwa maneno na ngojera. Confident ndiye mfariji na mdhamini wako wa kwanza unapopatwa na magumu kaa naye karibu. Unaweza kuwaeleza hadi yako ya moyoni na kamwe hutoyasikia nje. Wanaaminika zaidi ya ndugu wa damu. Ni wastarabu na waelewa. Huhitaji kujipendekeza ili wakupende. Akikusaidia jambo hatangazi kwa mtu.

Hawa ndo akina friends in need are friends indeed. Ni marafiki wa kufa na kuzikana. Ukiwanao unapata peace of mind badala ya

stress of mind. Hutaweza kutimiza maono yako bila hawa watu, jitahidi kuwatafuta katika orodha ya marafiki zako kibao. Watu hawa waliumbwa wakusaidie katika mambo yako kwa maombi, ushauri na kukuonya pia. Hawa ndo Mungu alituagiza kuambatana nao (Mithali 18:24).

### 2. Constituents

Hawa ni marafiki wauaji, marafiki pasua kichwa, marafiki maslahi, marafiki wanafiki na wapuuzi sana, akina kikulacho ki nguoni mwako. Watakupenda kwa sababu ya vitu ulivyonavyo, wakivipata wanakutema kama jojo. Wanaitwa akina baby omba usifirsike nikakumbia, akina firisika tujue tabia ya mkeo, akina hapendwi mtu inapendwa pochi, akina mkono mtupu haulambwi, akina wivu sina ila roho inauma ukipata mume.

Ni marafiki wa ajabu kweli, ukifanikiwa wananuna, ukipata mchumba wanamzengea, ukizubaa wanakuolea kachumba kako, ukipata mume wanahakikisha wanatembea naye. Hawafai. Hawa ukiwaonyesha mali zako wanakuletea wezi, wakikupiga tafu watakutangaza mtaa mzima. Hawana siri. Akina good for nothing. Ni washenzi na ndo wameharibu maana ya urafiki.

Hawa wameumiza watu wengi. Najua hata wewe ni muhanga. Ulifukuzwa kazi kwa sababu ya marafiki hawa, mchumba wako aliolewa na rafiki yako, pengine huyo mume uliyenaye alikuwa wa rafiki yako, ukamzunguka, nenda ukatubu maana vya shetani huliwa kuzimuni, hiyo tenda unayofanya yawezekana ilikuwa ya rafiki yako ukaipiga jukwaju ukajiona mjanja kumbe mpuuzi tu; pengine huo mradi unaofaidi proposal iliandikwa na rafiki yako ukamzunguka. Fanya umrudie myamalize kwani malipo ni hapa hapa duniani.

Wahenga waliposema abiria chunga mzigo wao walimanisha kuwa makini na constitutions. Ukimueleza habari za wazo la biashara unayotaka kuanzisha atakuibia hilo wazo; ukimueleza habari za mpenzi wako atakuibia; ukimueleza siri za ndani atazitoa nje, akija kukutembelea kwenu macho kodo kwa dada zako; ukimkaribisha kwako atammezea mate mumeo utadhani fisi, kumbe shost yako.

Furaha ya constituents ni kuona hufanikiwi. Wanaitwa saddists. Hata ukifanya kosa wanakuunga mkono. Utasikia, "Wamekukamata na vikombe vya ofisini kwenu? Hamna shidaaa, mbona wengi wanaiba tu? Mwanao amefeli form four? Usokonde kufeli shule siyo kufeli maisha! Mwanao si wa kwanza kufeli bana twezetu tukacheki gemu!"

Rafiki wa namna hii anajidai kukupenda anapokuona lakini mnapoachana ndo amekufuta akilini. Wewe ndo wa kumpigia simu kila siku. Ukiona kakupigia jua kuna jambo. Kama siyo mzinga basi kuna shari. Akiona simu yako anasema huyu bwege anapiga huyu. Kapata pesa nini? Halafu anakusengenya na kukushusha hadhi anapokuwa na washikaji zako. Anatangaza mambo kukuharibia. Wanatabia za Kiswahili sana hawa watu!

Ni wazuri katika kukupa changamoto za kimatumizi na siyo utafutaji. Hawaoni fursa,hawajishughulishi, hawana maono wala mipango inayohusu maendeleo. Atapenda mpoteze muda kwenye starehe. Hutaweza kufika unakokwenda usipowadondosha mapema marafiki wa staili hii. Watu wote kwenye meli wangeangamia kama wasingemtupa Yona baharini.

### 3. Comrades

Hawa ni marafiki wanaokuja kwako kukusaidia kutekeleza jambo lako na baadaye huondoka zao. Hawahitaji lolote kutoka kwako. Ni kama ngazi ambayo inahitajika sana wakati nyumba inajengwa, lakini nyumba ikishakamilika itaondolewa ila nyumba itabaki. Simoni Mkirene alikuwa comrade wa Yesu. Alionekana tu wakati wa kumsaidia Yesu msalaba na kuufikisha Golgotha, baada ya hapo alitoweka. Comrades si marafiki wa kudumu.

# *Sura ya* 17

# Mbona Tunazidi Kuwa Wajinga?

Tunaishi na kutenda kana kwamba tuliisha katwa vichwa siku nyingi! Au tumerogwa? Maana Afrika kila ukoo una uchawi anasema Bujibuji wa Instagramu. Unaanza kurogwa kwenu, unapata mchumba anakuroga ili umuoe, mkiachana hakufungui, unapata mwingine naye anakuroga, hadi kuja kuoa umeisharogwa vya kutosha, mama mkwe naye anakuroga, mchepuko unakuroga, kazini unarogwa, mtaani unarogwa, baamedi anakuroga, dada wa kazi naye anakuroga usimuulize chenji, bodaboda naye anakuroga ili uwe unamsubiri yeye hata kama umechelewa unakokwenda, wanasiasa nao wanaturoga ili tuwachague, yaani tunaishi katika cheni ya kurogana, usiporoga basi unarogwa.

Pengine hali hii ya kurogana ndo hupelekea tuzidi kuwa wajinga. Zamani umri ulikwenda sambamba na ukomavu wa akili ndo maana mama mpika gongo na baba mchoma mkaa walizaa maprofesa, siku hizi maprofesa huzaa balaa. Wanaitwa uzao wa nyoka!

Pamoja na usomi wako wote unakubali mwanao kulelewa na house girl unayemnyanyasa. Akidai mshahara unamuita mchawi ili umfukuze. Halafu kwa sababu ya ukorofi kwa mahaouse girl, mwanao hadi anaanza shule ameisha lelewa na mahouse girl kumi na tano wenye dini tofauti, maadili mchanganyiko na itikadi tofauti, muislamu, mkristo, mpagani, mdangaji, mchawi, kibaka,

mwizi, mpaka mwanao haeleweki. Ndo maana nauliza, mbona tunazidi kuwa wajinga?

Sitaki kuamini kabisa kama nchi yenye binadamu timamu tumeshindwa kutatua tatizo la ajira. Halafu tunaendelea kutumia mabilioni ya shilingi kusomesha wasomi tusiowahitaji. Karne hii bado kuna wazazi wanauza mashamba na kuchukua mikopo ili kusomesha watoto watakaorudi nyumbani kula. Miaka 30 bado unakula kwenu na wala hushituki na wakati babu yako katika umri huo alikuwa kwenye mipango ya kuongeza mke wa tatu maana yule wa kwanza tayari anafunga kizazi, watoto wameisha tumboni. Mbona tunazidi kuwa wajinga?

Kuelekea karne ya 22 bado tunaishi kama waajiriwa pamoja na kuzungukwa na utajiri wa kutupa, tunakwama wapi? Kipato kinapoishia kwenye chakula na malazi, kiuhalisia hiyo ajira inakuwa siyo fursa ya maendeleo bali juhudi za kubaki hai ambazo ni fursa ya maendeleo kwa muajiri wako. Hali hii zamani iliitwa utumwa, siku hizi ni sifa. Ndo maana hata kama ni mwaka sasa mwajiri hajakulipa mshahara na likizo hujaenda unaona pouwa tu kwa sababu kwenda kazini kila siku kwa gharama zako unaona ni sifa. Mbona tunadi kuwa wajinga?

Halafu kazi unazofanya ni za kutetea haki za binadamu na wakati haki zako zimefungwa kwenye gunia. Ukiukwaji wa haki za binadamu umezagaa kuanzia nyumbani hadi mitaani na makazini lakini tunaona wife beating tu na wakati kuna wanaume wanatandikwa kila siku, tena hali inazidi kuwa mbaya katika enzi hizi za vipato sawa. Mbona tunazidi kuwa wajinga?

Nchi moja yenye mifumo miwili ya elimu, moja kwa ajili ya kuzalisha viongozi na nyingine wapiga kura zikisimamiwa na

waziri mmoja wa elimu, nchi moja yenye mikoa ambayo sasa barabara za lami zinakwanguliwa ili kuweka lami mpya na wakati mikoa mingine lami kwao ni kama tambiko, halafu cha kushangaza shughuli husimamiwa na waziri mmoja na yeye hashituki kufanya kazi ya kuwabagua walipa kodi sawa. Mbona tunazidi kuwa wajinga?

# Sura ya 18

# Ngoja Niwakeree!

Hoja za maskini zinatisha, halafu zinatia huruma. Maskini wa akili akiongea jambo utabaki kujiuliza hivi na huyu kamkosea nini Mungu? Mbona hana wivu wa kimaendeleo na wakati anayataka? Unadhani tatizo ni nini? Tatizo nikwamba! Sehemu kubwa ya ubongo wake imejaa fikra za "Sizitaki mbichi hizi" huku udenda ukimtoka. Hizi ni akili za Sungura. Paza sauti kuzikemea kwa nguvu zako zote, akili zako zote na moyo wako wote, maana unakera!

Utaskia, "Pesa nyingi za nini na wakati wote tunakwenda chooni? Toba! Eti Hata uwe na magari mengi ya kutembelea, chooni utakwenda kwa miguu". Mtumee! Sina pesa lakini nalala usingizi. Yerewii! Hivi unapataje usingizi kodi ya nyumba imeisha wiki iliyopita? Unaweza sema shetani aliishamnyofoa ubongo huyu jamaa kumbe upo sema umenoki. Kwa mawazo ya namna hii unatokaje kwenye umaskini? Yakatae kwa vitendo na matendo, yakatae kwa sala na maombi. Maana kama ni kuomba, unaomba hadi mbingu zinatakisika kwa kelele zako zisizokuwa na hoja! Kumbuka imeandikwa,leteni hoja zenye nguvu na siyo kelele za nguvu. Wewe unabweka!

Nauchukia umaskini kwa sababu unakula ubongo! Mtu mwenye fikra za kimaskini amebarikiwa maneno mengi ya kumpatia ahueni kwenye hamna. Utasikia, "Simu ni simu tu ilmradi

nawasiliana." Nyumba nzuri kitu gani? Kwani usingizi si ule ule? Unataka uniambie usingizi wa aliyelala kwenye nyumba yenye choo cha shimo ndani na aliyelala kwenye nyumba yenye choo cha maji ni sawa? Labda chizi. Maana kwa chizi jana na leo havitofautiani. Ukiwa na fikra za namna hii zitakufanya ufubae kwa umaskini. Utaitwa bingwa wa shida. Hakuna bingwa wa shida hebu nenda katafute pesa!

Hata lugha za mwanaume mashine huwezi kuzikuta kwa serious guys.Utazikuta kwenye vijiwe vya vijana maskini. Hawana kazi ya kufanya zaidi ya kushindanisha wanawake wenye makalio makubwa wanaopita barabarani.

Maskini bwana. Utaskia Mungu amenibariki watoto saba, lakini anashindwa kuwahudumia. Anasema kila mtoto anakuja na riziki yake. Hivi kweli ni Mungu gani huyu akupe baraka usiyoweza kuitunza? Watoto wanakula msoto hadi wanamuuliza mama, baba atakufa lini? Maskini bwana. Hawa ndo hutuzalia akina born to suffer!

Ukimtembelea maskini na gari kali ataishia kusema aliyekupa wewe ndo kaninyima mimi. Badala na yeye kumuomba huyo aliyemnyima ampe gazi zuri anaishia kujenga hoja dhaifu ili kujustify njaa zake. Kauli kama hizi hukujengea matumaini ya kuendelea kuwa maskini. Huwezi kushindana kama una kirusi cha namna hii kichwani. Unahitaji kuformat kichwa!

Maskini kwa vijembe sasa. Loh! Utaskia, "Jino lenyewe moja, mswaki wa nini? Maskini bwana. Ni wazuri katika kujenga hoja za kuvunjana moyo. Hawana lolote. “Utaskia Mungu atatenda. Bwana ndiye Mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu.” Anayesema hatapungukiwa sasa, jana amelala njaa na leo hajui

kama utakula. Huu nao ni upungufu wa akili ujue. Kazi hufanyi, halafu unamsingizia Mungu ati kakunyima. Haya ni majungu!

Eti Mungu hamtupi mja wake na wakati aliishakutupa kitambo. Kanisani huendi, msikitini hukanyagi, sadaka hutoi, kwa nini asikutupe? Ndo maana ukiingia ibadani tu unapigwa na usingizi na usingizi kuisha pale Mtumishi wa Mungu anaposema enendeni kwa imani. Wewe ni pepo.

Hata katika mapenzi maskini anataka mchat muda wote. Utaskia mapenzi ni mawasiliano, ukimya peleka maktaba. Badala ufanye kazi mapenzi yanoge, unataka mkalie kuchat majungu. Unadhani mapenzi yanaboreshwa kwa tafadhali nipigie hadi masaa ya kazi. Eti kama mapenzi ni pesa nenda kaoe benki. Maskini bwana. Hivi wahenga waliposema hapendwi mtu inapendwa pesa maskini walikuwa wapi? Mapenzi yasiyoangalia pesa yako mbinguni siyo hapa duniani.

Maskini akikosa mboga tamu ataishia kujifariji eti mboga maharage, kuku mbwembwe! Zetu dagaa kuku tamaa. Eti ugali unapanda kwa kisamvu, kuku ni kiherehere chako. Maskini wanatisha. Utaskina, "Usiulize maisha yangu, subiri nife historia yangu itasomwa." Kaa!

Eti kila kitu kinapangwa na Mungu. Mungu mwenyewe humjui. Anapangaje sasa vitu vyako? Yaani ukiwa na fikra za kimaskini huishiwi vituko. Eti siwezi kununua gari kwa mkopo mimi. Jamani hivi kuna mtu aliendelea bila kukopa? Haya maisha ya kila mtu atakufa kaburi mjomba hayafai katika jamii zinazotafuta maendeleo!

Maskini kwa majungu sasa. Utasikia huyu bwana wake ni mzee, alifuata pesa tu. Mara siwezi kula chakula cha kwenye friji mimi na wakati hana friji. Anajifanya amesoma sasa mbona haolewi, utadhani kaambiwa kusoma ni kuolewa. Mwingine utaskia "Kuolewa ni stress tu bora nikae single." Kumbe kakosa wa kumuoa. Hiyo kazi aliipata kwa sababu alitembea na bosi. Hata kama anadegree maisha yake sawa na yetu. Siwezi kununua gari na wakati sina nyumba! Anasura nzuri tatizo miguu.

Tatizo ukiwa na fikra za kimaskini lazima uupore ubongo kazi yake ya kufikiri. Unakuwa mtu wa hisia na mihemuko tu. Utaskia usione amenenepa hivyo, anatumia ARV. Ukinenepa unaitwa mgonjwa, ukikonda umeishiwa. Hao ndo maskini wa fikra. Wanakera!

Meneno mengiii utadhani chiriku. Maskini wa akili anajua kuponda tu. Haonagi mazuri ya wenzake. Utaskia eti kasomea nje, nje kitu gani bana? Maisha ni hapahapa bongo, halafu ukimuangalia umri umekwenda, yuko mbongo na maisha hana. Ati kufeli shule siyo kufeli maisha bana. Ukimuangalia anayesema sasa, kafeli vyote. Shule alifeli, na maisha amefeli.

Maskini wana maneno mengi yasiyokuwa na umuhimu. "Ati kila mtoto anakuja na riziki yake. Silaha pesa, rungu mzigo. Utamaliza gesi kwa kupika mifupa. Raha ya kinu mtwangio. Hapa kazi tu unalala mchana ili uchati usiku, mguuni umevaa yeboyebo." Duniani simama nishuke! Mambo yasiyokuwa na umuhimu huzungumzwa kwa muda mrefu kwani wazungumzaji wanayafamu kuliko mambo muhimu.

Acha kuchezea wakati ewe maskini mwema. Kumbuka wakati ni kama upanga usipo ukata utakukata. Usiwe kama inzi kutua juu ya vidonda.

# Sura ya 19

# Tunaishi Katika Dunia ya Namna Gani?

Tunaishi katika dunia ambayo halali huitwa haramu, wazinzi huitwa wapenzi, kamali huitwa kubet, mshirikina huitwa mtaalam, anayetembea uchi huitwa mrembo, anayechukia ulevi, ngono na mapenzi kabla ya ndoa anaitwa mshamba, mafisadi na wezi wanaotoa sana sadaka hupewa viti vya mbele, ndoa takatifu zinaitwa ndoano, starehe ni ngono na ngono ni starehe, matokeo yake balaa na majanga yanazidi kutuandama zaidi na dua hazipokelewi.

Tunaishi katika dunia ambayo maskini anatembea umbali mrefu kutafuta chakula, tajiri anatembea umbali mrefu kuunguza chakula. Halafu ukirudi vitabuni tunaambiwa binadamu wote ni sawa. Usawa katika nini? Labda usawa katika kufa ingawa hata kufa tuna kufa tofauti. Wapo wanaokufa kwa kukosa lishe na wengine wanakufa kwa kuzidisha lishe!

Tunaishi katika dunia ambayo ndoa za mitaala zinaitwa dhambi, ushoga ni haki za binadamu na michepuko dili! Hapo kuna mtu yuko salama? Sidhani! Huwa najiuliza, wazungu waliwezaje kutushawishi kwamba ndoa za wake wengi ni dhambi lakini ndoa za mwanaume kulalana na mwanaume mwenzake ni haki za binadamu? Kaza mwendo usiombe kushukia njiani! Giza ni nene, na masaa yamekwenda sana!

Tunaishi katika dunia ambayo watoto na wazee wanashindana kukosa adabu, babu mwenye pesa anaitwa baby na asiye na pesa anaitwa muhenga na wakati muhenga ni mzee mwenye akili. Kwa nini tunapoteza maana? Eti uzee Chalinze. Babu tulia nyumbani, ota moto ufe salama, usije kufa kifo cha aibu uzeeni. Hiyo pensheni isikuzuzue! Ungekuwa na meno ningesema ponda mali kufa kwaja. Sasa meno hayapo tena!

Tunaishi katika dunia ambayo kundi la Waafrika wakienda Ulaya wanaitwa wakimbizi na wakati kundi la Wazungu wakija Afrika wanaitwa watalii. Ukimkuta mwafrika kwenye mapori ya asili anaitwa jangiri, mzungu anaitwa mtafiti. Kwa style hii tunaachaje kuporwa? Ujinga unaweza usikuue lakini ukakuhenyesha kwelikweli. Afrika mambo mengi yanayotuhenyesha ni ya kitoto kweli.

Tunaishi katika dunia ambayo kosa moja linatosha kufuta uzuri wote aliokutendea rafiki yako na wakati wahenga walisema kosa moja haliachi mke. Siku zote kabla hujafanya jambo lolote ukiwa na hasira hesabu moja hadi kumi. Hadi uje kufika kumi utagundua mazuri mengi aliyokutendea unayetaka kumuua.

Tunaishi katika dunia ambayo wanandoa wanaishi kwa kuzengeana na kukomoana badala ya kusaidiana na kushirikiana. Wanawake wanafundishwa kama humpendi mumeo muombe pesa kila siku atakimbia mwenyewe, wanaume nao wanafundishwa mkeo akifanya kosa usimpige, mpe pesa feki akapigwe sokoni. Tobaaa! Sasa hapo kuna ndoa, au mawindo?

Tunaishi katika dunia ambayo wakosoaji wanaitwa wachochezi na watukanaji tunawaita wakosoaji. Matokeo yake tumeharibu maana ya kutukana na kukosoa. Ajabu kweli! Unakuta mke wako

ameunguza nyama halafu unasema ..SINILISEMA, HILO NDO TATIZO LA WANAWAKE WAFUPI…Sasa mambo ya ufupi na nyama kuungua yanatoka wapi? Hapo hujakosoa, umetukana!

Tunaishi katika dunia ambayo mwenye nacho huongezewa na asiyenacho huibiwa. Dean Griffiths anasema "We live in a world where we give our pounds to those who have too much and our pennies to those who have too little." Katika hilo ndo maana maskini hafilisiki. Afilisike ana nini?

Siku moja Mangi alisema "Dalili moja wapo ya kuwa maskini ni kulala mchana. Zee la Vyeti akajibu, "Futa hii Mangi, wengine sisi ni walinzi tulale saa ngapi?" Hansy Copper akadakia, " Usifute sababu hakuna mlinzi tajiri. Loh!

Tunaishi katika dunia ambayo walalahoi wanachagua viongozi walalahai kwa jina la demokrasia halafu wanaambiwa hii ni serikali yao. Eti serikali ya watu. Unajua ukiwa maskini halafu mjinga ni rahisi sana kudanganyika. Na ukiishadanganyika huchomoki!

Tunaishi katika dunia ambayo ukimpa chakula maskini utaitwa Mtakatifu, ukiuliza kwa nini maskini hana chakula utaitwa mchochezi. Ili uwe salama pambana na hali yako! Lakini kupambana na hali yako si ndo ubinafsi wenyewe? Ndiyo ni ubinafsi lakini kumbuka, hakuna mapambano yanayozidi uhai wako.

Tunaishi katika dunia ambayo uongo unatukuzwa kwa sababu unasemwa na watu wengi na ukweli unapuuzwa kwa sababu unasemwa na watu wachache. Katika dunia ya wengi wape, wajinga ndo waliwao. "Wrong does not cease to be wrong

because the majority share in it,"alisema Leo Tolstoy. Tunaishi katika dunia ambayo ukimaliza kusema ukweli kimbia, ukimaliza kusema uongo nenda kavishwe taji. Jamaniii! Lakini hata huo uongo si mpaka uwe na fursa ya pa kupeleka?

Tunaishi katika jamii ambayo maskini anafundisha mbinu za kuwa tajiri, mzinzi anafundisha mbinu za kuacha uzinzi, aliyekimbia ndoa anafundisha namna ya kuwa na ndoa nzuri, aliyefeli mtihani anafundisha mbinu za kufaulu mtihani, aliyefeli maisha anafundisha mbinu za kufanikiwa maishani na mwenye tabia mbaya anafundisha jinsi ya kuwa na tabia nzuri. Kweli mwisho wa mawindo mbwa hana chake. Hata wewe?

Tunaishi katika dunia ambayo wazazi wenye tabia chafu wanawachukia watoto wao wenye tabia chafu na wakati imeandikwa kenge huzaa kengi, siyo tumbili. Wakati mwingine tupunguze kutafutana ubaya.

Tunaishi katika dunia ambayo waliosoma sayansi wanawaponda waliosoma masomo ya sanaa hata kama wamesoma sayansi ya kurepair viraka! Dunia simama nishuke! Unasoma sayansi bila kukokotoa halafu ukakokotoe ghorofa? Thubutu! Labda kama unataka kuishia jela kwa kujenga ghorofa litakaloua watu.

Tunaisha katika dunia ambayo tunasifiana, kupongeza na kutiana moyo baada ya kufa. Hatuna  lugha ya pongezi na kusifu na wakati ndo lugha ambayo kipofu anaweza kuisoma na kiziwi kuisikia. Brother, najua una mengi mazuri lakini hadi ufe ndo tutayasema.

Tunaishi katika dunia ambayo waliotakiwa kuishi jela wako mtaani na waliotakiwa kuishi mtaani wako jela, hata waliotakiwa

kuishi Milembe kwa vichaa wako mtaani wanatesa kwa zamu. Ajabu. Soma hivi visa viwili halafu uniambie nani mgonjwa wa akili hapa alitakiwa afungiwe Milembe.

Wagonjwa wa akili walipanga jinsi ya kutoroka hospitali. Wakaamua wampige mlinzi, wamnyang'anye funguo, wafungue mlango, wakimbie. Walipofika mlangoni hawakukuta mlinzi na mlango ulikuwa wazi. Wakasema, "duh! mpango wetu wa kutoroka ushafeli!" basi wakaghairi. Watu wa namna hii wapo mtaani pia!

Tunaishi katika dunia ambayo biashara haramu zinalipa kuliko biashara halali. Piga tamasha la Kumsifu Mungu kwa kiingilio hata cha buku jero uone kama utajaza uwanja, lakini piga show za mahaba niue uone. Uwanja utajaa hadi vibaka watapita madirishani kweda kufa kwa mahaba.

Tunaishi katika dunia ambayo watu wachache wanaelewa kabla ya mtihani, wengine wanaelewa wakati wa mtihani na wengi sana wanaelewa baada ya mtihani. Hawa wa mwisho wanaitwa wajinga! Hawa wakiwa wengi katika jamii ni janga la taifa.

Tunaishi katika dunia ambayo wenzako wanawaza swala kabla ya kulala, wewe unawaza hawala anayekumalizia hela. Tunza familia yako blaza, hawala hana shukurani.

Tunaishi katika dunia ya heshima pesa, shikamoo kelele! Huna pesa hakuna anayehitaji hata salamu yako! Heshima na pesa ni kama maji na mkondo wake! Tunaishi katika dunia ambayo ukiwa na pesa watu wataheshimu mpaka kaburi lako!

Tunaishi katika dunia yenye wajenga hoja wengi kuliko wajenga nchi. Zamani tuliimba chama cha jenga nchi, siku hizi tunaimba vyama vyatafuna nchi! Majanga!

## Sura ya 20

# Ukishukuru Mungu Anatenda, Usiposhukuru Shetani Anatenda

Shukrani ni dawa ya mwili na akili wanasema watafiti wa mambo ya kisaikolojia ndiyo maana vitabu vitakatifu vinasisitiza kushukuru kwa kila jambo. Kushukuru maana yake ni kuomba tena, kutoshukuru maana yake usinipe tena. Neno asante linahamasisha mtu kutoa tena. Ukiijua siri ya kusema asante utafaidi mengi, usipoijua utakosa vingi. Wekeza katika shukrani ule maisha.

Siyo kwamba watu wanashindwa kutoa shukrani kwa makusudi, hapana ni kwa sababu hawajui nguvu ya kushukuru.Tuko katika jamii ambayo ukisubiri shukrani utakufa kwa manung'uniko. Unamfadhili mtu anakula, akishiba anakutukana kwa sababu shukrani ya punda ni mateke.

Yaani tunazidiwa kushukuru na mchepuko. Mchepuko akipewa hata elfu tano atakushukuru kwa maneno, meseji na mabusu utadhani umempa milioni moja na wakati kuna mwingine ukimpa hata milioni moja bado atakuangalia kama choo cha shimo.

Hata wale kumi walioponywa ukoma na Yesu ni mmoja tu ndo alirudi kushukuru. Heri kumfadhili mbuzi utakunywa supu, kuliko binadamu mwenye maudhi.

Mungu anajua madhara ya kutoshukuru ndio maana maneno, "Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, kwa maana fadhili zake ni za milele," yamejirudiarudia katika Biblia kupitia Zaburi 107:1, Zaburi 118:1, Zaburi 136:1, 1: Nyakati 16:34, Zaburi 118:29 na Zaburi 106:1.

Adam alipokea mke, hakushukuru, wakatimuliwa Eden. Sasa na wewe shukuru haraka katika maeneo haya kumi

**Moja: Shukuru kwa ajili ya mke uliyenaye yasikukute ya Adam:** Usiposhukuru kwa ajili ya mkeo ndoa utaiona chungu; dada zako watakusumbua, mama yako atakusumbua, mke wako atakusumbua, watoto wako watakusumbua, shemeji zako watakusumbua, mama mkwe atakusumbua, baba mkwe atakusumbua. Utaambiwa unampenda mkeo kuliko wao na wakati mke ni mwili wako. Utaambiwa mkeo anaringa hata kama haring, Ukimsikiliza mkeo utaambiwa unampendelea yeye kuliko ndugu zako, ukiwasikiliza ndugu zako mke atasema humpendi. Mambo yakikuzidia unakwenda kutafuta ahueni Tanga. Hapo ujue umeishatimuliwa Eden kama Adam.

**Mbili: Shukuru kwa ajili ya mumeo uepuke kumroga.** Dada yangu usiposhukuru kwa huyo handsome wako utajikuta umekuwa mshirikina, maana ataanza kutoka nje na kutembea na kila kitu, pesa ya matumizi lazima umkunje. Ukichoka lazima utakwenda kutafuta ulozi umtulize. Utajikuta ukimlisha mumeo uchafu na kumuua bila kujua. Siku hizi wanawake wanaweka nyama sehemu za siri wakati wa siku zao za hedhi halafu inapikwa vizuri na kumlisha mume! Haya ni matendo ya kishetani yatokanayo na kutoshukuru. Shukuru mama usije kufanya haya kwa mumeo.

**Tatu: Shukuru kwa ajili ya watoto wako wasiwe kero kwa jamii.** Kuna watoto ni wasumbufu kanisani, wasumbufu mtaani, wasumbufu shuleni, wasumbufu kila sehemu, yaani utulivu sifuri kabisa, halafu wakienda ugenini muda wote mama anafoka, Junia hebu tulia, mbona husikii. Siku moja Junia na mama yake wameenda kwenye harusi, mama akamwambia Junia, acha kuweka nyama kwenye mfuko kunguru wewe, unaniaibisha!!! Junia akamnong'oneza mama yake , "Mama ongea polepole watu wasisikie ulivyonilea vibaya! Unadhani hawa vibaka walizaliwa na mbuzi? Hapana! Walizaliwa na wazazi wazuri walioshindwa kushukuru kwa kuzaa. Zawadi ya mtoto inaweza kugeuka adhabu kwako kwa sababu hata shetani alikuwa malaika.

**Nne: Shukuru kwa ajili ya mali zako kabla hazijakuua.** Usiposhukuru kwa ajili ya gari lako litakuwa ni la kugongwa kila siku, kuibiwa taa, mara kioo, mara site mirror, mara breki kukatika, mara kula sana mafuta utadhani lina midomo. Shukuru kwa ajili ya pikipiki yako kabla haijakuvunja miguu, shukuru kwa ajili ya baiskeli yako kabla haijaua watoto wako, shukuru kwa ajili ya nyumba yako mpya kabla hamjaungulia humo, shukuru kwa ajili bastola yako kabla haijakufyatukia. Kumbuka kutoshukuru baraka zako zaweza kugeuka balaa.

**Tano: Shukuru kwa ajili ya akili na elimu uliyonayo kabla haijakushangaza.** Umepewa akili nzuri hujashukuru, umesoma vizuri hujashukuru, umepata nafasi nzuri hujashukuru, unapiga pesa za umma kwa jina la cheo chako, wanakukamata, unakimbia kujinyonga kwa sababu shetani amekushinda.

**Sita: Shukuru kwa ajili ya kipaji ulichopewa usije ukajuta maishani.** Usiposhukuru kwa ajili ya kipaji chako unaweza kufa kifo cha aibu. Unapewa sauti nzuri, unaimba vizuri, unapata pesa

nzuri, unaingia kwenye starehe za Sodoma na Gomora, unazoa magonjwa yasiyotibika unaenda kutibikia kaburini ukiacha watoto wako wakiuana kwa mali ulizoacha.

**Saba: Shukuru kwa ajili ya cheo ulichonacho kabla hujamkumbuka aliyesema cheo ni dhamana.** Umepata cheo, shetani anakuvaa, unapata kiburi na kuwa mtukanaji, unatukana mpaka baba zako na wengine unawazaba vibao kabisa, hapo ujue siku zako haziwezi kuwa na heri hapa dunuani.

**Nane: Shukuru kwa ajili ya afya uliyonayo ili uzima wako usikuelekeze kutenda yaliyochukizo mbele za Bwana ukapata hasara.** Kumbuka hata majambazi wamejaaliwa afya njema inayotumika kuwamaliza wao wenyewe. Usiposhukuru kwa zawadi ya maisha, maisha yako yatakuwa kero kwako, kwa familia yako na kwa jamii nzima. Usiposhukuru kwa afya njema uliyonayo uzima wako utakuwa anguko lako.

**Tisa: Shukuru kwa ajili ya mchumba wako kabla hajakutenda ukatendeka.** Siku hizi watoto wadogo wanakufa kwa msongo wa mawazo kwa sababu walipokea wachumba bila kushukuru. Kutoshukuru kwa ajili ya mchumba uliyenaye kutafungua milango ya kuwa na wachumba wengi ambao watakuchanganya na kukunyoosha mpaka uzeekebila kufunga ndoa.

**Kumi: Shukuru kwa ajili ya pesa zako kabla hazijanuka.** Kumbuka pesa inaweza kuhamisha milima sasa ukicheza itakuhamishia milimani. Watu wengi huamini pesa ni chanzo cha mabaya yote, mimi naamini pesa siyo issue, issue ni kuwa na pesa bila shukrani.

Vya kushukuru viko vingi, ndiyo maana tumeambiwa tushukuru kwa kila jambo (1: Wathesalonike 5:18.) Unaweza kusema huna cha kushukuru na wakati ukiangalia nyuma ulikotoka ulitakiwa kuwa umekwisha kufa kitambo, lakini leo bado unadunda.

Shukuru kwa kidogo ulichonacho ili uongezewe. Yesu alipoletewa mikate michache alishukuru na wala hakunung'unika kwamba chakula ni kidogo (Mathayo 15: 32 – 38). Jifunze kumshukuru Mungu kwa ulichonacho hata kama unadhani hakitoshi ili kuruhusu nguvu ya ongezeko itende kazi. Unapokuwa mtu wa shukrani, unafungua baraka juu yako.

Basi twende mbele za bwana kwa shukrani maana imeandikwa atoaye dhabihu za kushukuru, ndiye anayenitukuza. Hapa napo kuna hoja. Usiende kushukuru mikono mitupu hii ni kanuni ya Mungu.

Unapokuwa mtu wa shukrani lazima utakuwa na kitu cha ziada kwa sababu kushukuru ni kuomba tena. Orodhesha mambo mazuri aliyokutendea Mungu ukashukuru. Mara nyingi tunaweka mkazo sana juu ya kile ambacho hatuna na kusahau kushukuru kwa kile tulicho nacho. Usishangae ukawa hujawahi hata kumshukuru Mungu kwa kuzaliwa pengine ndiyo maana unajuta kila siku. Kumbuka usiposhukuru kuzaliwa utajuta kuzaliwa.

Shukrani humfanya achukiwaye kupendwa, akataliwaye kukubalika, vurugu kuwa amani, kuchanganyikiwa kuwa furaha, makazi kuwa nyumbani na adui kuwa rafiki. Ubora wa maisha yako unategemeana na jinsi unavyomshukuru Mungu wako. Shukrani ni kipimo cha kujua maisha yako yanaelekea kwenye neema au balaa. Kama unataka kutafuta furaha, tafuta kwanza kushukuru. Yule anayeshukuru hata kwa madogo huwa na furaha

sana. Haijalishi unapitia magumu kiasi gani, ukianza kushukuru tu magumu huwa yanakuwa mepesi. Kumbuka moyo wa shukurani ni ufunguo wa milango ya duniani na mbinguni.

# Sura ya 21

# Mambo Haya Yanakugharimu

Mwanangu, kuna vijimambo vidogovidogo ambavyo umekuwa ukivitenda bila kuelewa vinakugharimu kiasi gani! Mimi nakwambia kwa sababu wewe ni wangu, wengine hawatakwambia, watakuteta unapoondoka, watakuteta unapopita ndo maana ukipita utasikia vicheko, ukigeuka wanaocheka huwaoni! Naomba nikukumbushe vijimambo hivyo mwanangu ili uviache upate heshima kila uingiapo na utokapo!

**Jambo la Kwanza ni Ulaji Wako**

Mwanangu, namna yako ya kula inatosha kuonyesha wewe ni mstaarabu au mshenzi tu. Unatafuna na kuongea wakati mmoja tena kwa sauti ya juu utadhani umeambiwa ukisubiri kumeza ndo uzungumze utaishiwa maneno.

Mwanangu unakula kwa kudondosha chakula tena ugenini utadhani mikono haina nguvu, mtu akiangalia ulipokaa wakati wa kula pamechafuka utadhani unajifunza kula.

Mwanangu unakula chungwa na kutema mezani kuwatia kinyaa wenzako, unatafuna ugali huku umeshikilia paja la kuku mkononi na wakati umepewa kisosi cha kupumzisha nyama. Halafu mwanangu ukimaliza mnofu wako mifupa unachanganya na mate yako na wakati mifupa hiyo kuna wanaoikusanya na kutengeneza

supu wakauze kwa sababu nao ni washenzi, yaani mwanangu unatutia aibu utadhani mtoto wa nguruwe.

Mwanangu tabia yako ya kuchokonoa meno na kijiti mpaka kijiti nacho unakitafuna baada ya kumaliza kula inakufedhehesha sana. Unashinda na kijiti mdomoni siku nzima ukijichokonoa nyama ya supu ya ofa, unaingia na kijiti hicho hadi ofisini na darasani kabisa.

Unapewa chupa ya maji, unaivuta kwa nguvu hadi mdomoni huku ukiifinya na kutoa kelele utadhani unamwaka mzima hujanywa maji, kwa nini unafanya hivyo na wakati umepewa glasi?

Mwanangu ukila ndizi utupa maganda barabarani na wakati kuna dust bin, ukitafuna karanga unarusha maganda hovyo, tafasiri yake ni kwamba wewe si mstaarabu hivyo hufai kukaa meza moja na wastaarabu.  Acha!

**Jambo la Pili ni Uandishi Wako**

Namna unavyoandika inatosha kukuchora ulivyo, yaani mtu rafu au mtu makini. Unaanza kuandika jina la mtu kwa herufi ndogo, unaandika sentensi haina kituo, unaanza sentensi kwa herufi ndogo halafu unategemea watu makini watakuchukuliaje? Unaandika barua haina kituo, tarehe wala sahihi halafu unategemea ujibiwe. Hapo utawapa shida wafagia ofisi kuichoma tu. Ukiandika Kiswahili hakieleweki, kizungu ndo balaa tupu yaani unakuwa kama popo,hajulikani ni mnyama au ndege. Mtu akitembelea ukurasa wako anakuta matusi tu! Tafasiri yake ni kwamba wewe si mtu makini hivyo hufai kukaa meza moja na watu makini.

## Jambo la Tatu ni Uvaaji Wako

Mwanangu vaa yako ni mazingaombwe matupu. Sasa unapovaa vazi la kuogelea kanisani unategemea nini? Unakwenda kwenye usaili huku kila kiungo kimepuliziwa aina yake ya pafyumu halafu unategemea kupewa kazi kabisa? Hivi unafahamu kama ulivyoingia kwenye chumba cha usaili kuna watu waliishiwa pumzi sababu ya mchanganyo wako wa pafyumu? Haya ni mambo madogo sana lakini athari zake ni kubwa. Kila baada ya siku mbili unataka uingie ofisini na aina tofauti za visuko tena vya gharama. Sawa najua mwanamke nywele lakini kumbuka kabla hawajakupandisha cheo na kukupa majukumu makubwa watahofia kama utapata muda wa kupiga kazi ukaacha kwenda kusuka. Ondoka usemwe!

## Jambo la Nne ni Uzungumzaji

Hapa napo wengi ni chenga tu. Unataka uzungumze wewe tu. Kila kitu hata kama hujui unataka uchangie. Unapokea mpaka simu na kuongea kwa sauti ukiwa kwenye ofisi ya watu. Wanakuchora tu. Unakata mazungumzo na boss wako, au mchumba wako, au baba yako, au mtu wako wa karibu ili ujibu chattings zinazoendelea kwenye Group lako la Primary. Yaani boss wako anaongea wewe unabaki kuitikia tu mmhhh, eheee, hata pasipohitaji jibu hilo. Hapa lazima upishane na watu makini. Kama ni ofisini hutopanda cheo ng'oo kwa sababu tabia mbaya ni sawa na tairi lenye pancha, haliwezi kwenda popote mpaka libadilishwe!

## Jambo la Tano ni Muda

Hapa napo wagonjwa ni wengi. Vikao vyote kuanzia vile vya harusi mpaka vya ofisini na mabosi wako unachelewa. Yaani unachelewa mpaka appointments ulizopanga mwenyewe. Kwa tabia za namna hii mwanangu utaishia kuwa chini ya mtu mpaka unastaafu. Unachelewa mpaka mazishi halafu unategemea watu wakuheshimu. Thubutu. Yaani kila unayemwambia utampigia simu baadaye hupigi. Yaani unatupiga sound hadi sisi wazazi wako tuliokuzaa!

Sasa mwanangu naomba nikuachie amri hizi kumi zitakusaidia kuwa muungwana!

1. Ukichukua kitu toka mahali fulani kinapotakiwa kukaa jaribu kurudisha sehemu ulipokitoa baada ya kutimiza hitaji lako. Hata kama ni kitana, kikombe, au dekio lweke sehemu ulipokitoa. Jizoeze hivi inajenga tabia ya kuwa makini.
2. Ukikopa pesa rudisha kwa wakati ulioahidi, endapo umekwama basi jaribu kuwa muungwana mwanangu, jieleze kwa mhusika kama ulivyojieleza wakati unakopa. Kukaa kimya huku unajua umeahidi kitu mpaka ukumbushwe ni utapeli.
3. Ukiazima kitu kama kitabu, kiatu, gari, pikipiki, nguo, computer au redio kitunze na ukirudishe katika hali ileile kama kilivyokuwa wakati unapewa. Kirudishe mara umalizapo hitaji lako. Kujisahaulisha ni tabia ya ovyo sana mwanangu, unamkwaza mwenye mali hata kama mmezoeana vipi. Hata kwambia tabia yako mbaya, atawaambia wengine, yakufikie, unune, urafiki ufe!

4. Usichukue kitu cha mtu bila kuomba hata kama mna ukaribu wa bega na kidevu. Omba, toa taarifa hata kama ni peni, jizoeze hivyo ni rahisi na inapendeza mwanangu!
5. Usinunie watu bila kuwaambia walipokukwaza ukitarajia wataona yaliyokununisha. Kwanza utaonekana kituko mwanangu, pili ni kujinyima raha ya maisha. Maisha ni mafupi sana, unapata wapi muda wa kununanuna hovyo?
6. Unapotoa ahadi ya kukutana na mtu, hakikisha unamjulisha mhusika endapo utachelewa au hautofika. Fanya hivi mapema na endapo utashindwa kutoa taarifa, hakikisha baadaye unamjulisha mhusika sababu za kutotimiza ahadi, au kutotokea.
7. Ukitumwa kitu na chenji ikabaki, rudisha kwa mhusika. Kukausha na chenji ya watu si tabia nzuri hujui bajeti ya mtu aliyekutuma.
8. Unaposemeshwa na mtu weka simu pembeni umsikilize. Kujifanya unamsikiliza huku mikono na macho viko busy na simu ni ishara ya dharau. Ni bora uombe samahani umalizane na simu kisha umsikilize kiuungwana.
9. Unapokuwa kwenye mazungumzo na simu ikaita, omba radhi hata kwa ishara, ama mjulishe mhusika kuwa unapokea simu. Ni kitu kidogo sana lakini chenye maana kubwa mbele ya uliyenaye hapo.
10. Mwanangu kamwe usile bila kuomba ukaja kula na shetani, mwanangu kamwe usilale bila kuomba ukalala na popo bawa, mwanangu usitoke kitandani na kwenda uendapo bila kuomba siku yako ikajaa balaa!

# *Sura ya* 22

# Tukosoane, Tusitetane

Watu wenye fikra pevu wanaamini hakuna mafanikio pasipo ukosoaji na wakati watumwa wa fikra wanaamini kukosolewa ni uonevu, kuaibishana na kuoneana wivu. Wao kutetana ndiyo bora. Lakini ukweli ni kwamba, ni kupitia ukosoaji watu wenye fikra pevu wamevunja rekodi katika utendaji na watumwa wa fikra kuvunja rekodi katika kushindwa. Watu wanapojua hupendi kukosolewa, basi watakukosoa kupitia kwa wenzako na hapo watakuteta. Hata Nyerere kupitia chapisho lake la Tujisahihishe anasema, "Wengine humwona mwenzao anafanya kosa. Badala ya kumwambia pale pale kijamaa kwamba atendalo ni kosa, watanyamaza kimya. Lakini hawanyamazi kabisa! Watakwenda kumteta katika vikundi vya sirisiri. Mateto haya siyo ya kumsaidia mwenzao, ni ya kumdhuru".

Kuyaona madhaifu ya mwenzako na kumweleza yeye mwenyewe ni kumkosoa, lakini kwenda kuyaeleza madhaifu hayo kwa wengine ni kumteta, kumdunisha, kumdhalilisha na kumdhuru. Kumdunisha mwingine ni kujidunisha. Kumdhalilisha mwingine ni kujidhalilisha. Kumteta mwenzako ni unafiki. Jamaa mmoja alimgeukia mwanaume aliyekuwa karibu naye na kuanza kumponda mwimbaji aliyekuwa anaperfoma "Ana sauti mbaya sana! Unamjua ni nani?" Mwanaume akaiibu, "Ndiyo namjua ni mke wangu." Jamaa kikamshuka, "Samahani, sisemi juu ya sauti yake bali maneno anayoimba si mazuri. Nashangaa nani alitunga

wimbo huo mbaya." Mwanaume akajibu, "Ni mimi niliyetunga wimbo huo." Mpondaji huyo alijidhalilisha na kujidunisha. Kumbe angekuwa muungwana, baada ya kumaliza angemfuata mwimbaji yule na kumweleza alikosea wapi ili pengine aboreshe zaidi.

Kumbe tukosoane, turekebishane, tuwajibishane ndipo tusameheane alisema Regia Mtema. "Tishio kubwa katika uhuru ni kukosekana kwa ukosoaji" alisema Wole Soyinka. Kukosoa siyo dhambi. Kwa kuwa hakuna mkamilifu duniani basi lazima tukubali kukosolewa.

Tuwe kama mchezaji wa mpira, kukosolewa kutusaidie kucheza vizuri. Winston Churchill aliwahi kusema, "Ukosoaji unaweza usikubalike, lakini ni wa muhimu. Unatekeleza jukumu sawa na maumivu katika mwili. Huleta umakini katika mambo ambayo hayaendi vizuri".

Leo hii ukionekana kukosoa mienendo mibaya ya upinzani kwa mustakabali wa demokrasia watakutukania mpaka bibi yako aliyetangulia mbele za haki. Kadhalika ukijaribu kukosoa mienendo ya chama tawala jiandae kuitwa mpinzani hata kama unaongea kama mtanzania wa kawaida tu. Yaani upuuzi uonekane na usikemewe kisa tu utaitwa mpinzani. Anakosolewa Mungu sembuse binadamu?

Tuheshimiane na tupingane kwa hoja na mwisho wa siku ukweli utajibainisha. Tuwe na subira kwa sababu ukweli unapanda ghorofa kwa ngazi na wakati jazba hupanda kwa lift. Madhara ya kuupuzia ukweli ni makubwa kwa sababu ukweli unatabia ya kulipiza kisasi.

# *Sura ya* 23

# Hasara Katika Biashara ni Giza la Kukusaidia Kuona Nyota

Pamoja na kwamba hasara katika biashara ni kitu cha kawaida ni wafanyabiashara wachache sana wanaoweza kukivumilia. Wengi wakipata hasara wanaachana na biashara, wengine wanabadili biashara na wachache sana wanajiua. Labda nikwambie tu, hasara ni changamoto zinazokuja katika biashara kwa sababu maalumu. Kumbe hasara ndio hufanya biashara yoyote ile ivutie kuzishinda hufanya biashara iwe na maana. Twenda pamoja na mambo kumi muhimu ili kukabiliana na hasara ili kuifanya biashara yako iwe na maana!

Moja, chukulia hasara katika biashara yako kama **ujumbe wa kukutaka ujaribu mbinu mpya za kufanya biashara yako.** Hasara ikusaidie kuona mbinu nzuri za kufanya biashara zilizojificha. **Kama uliruhusu ukoo mzima kuuza duka lako basi kauze mwenyewe. Kama ulikuwa na kauli mbaya kwa wateja badili. Kama ulikuwa unachelewa kufungua biashara na kuwahi kufunga acha mara moja.**

**Mbili, h**asara uliyoipata katika biashara yako inaweza kuwa mtaji unaoweza kukupa heshima hapo baadaye. Kumbuka kukosa njia ndio kujua njia. Njaa ndio hukipa chakula ladha yake. Kiu ndio hufanya maji yawe matamu. Upweke ndio huupatia urafiki thamani yake. Ndio maana wahenga walisema, **kuna mambo**

**ambayo unajifunza vizuri sana wakati kuna dhoruba.** Tumia hasara kujifunza. Bila kupata hasara huwezi kuwa na nidhamu katika biashara. Mabepari wanasema chezea biashara yako uadhibiwe na wateja wako.

**Tatu, chukulia kupata hasara katika biashara yako kama kukanyaga kaa la moto maana lazima utaondoa mguu haraka bila kupoteza muda**. Yaani unapopata hasara mara moja elekeza nguvu zako katika kutatua na si kunung'unika. Manung'uniko huchosha akili, manung'uniko husononesha moyo, manung'uniko huuguza moyo, manung'uniko huleta vidonda vya tumbo, manung'uniko huleta makunyanzi usoni, manung'uniko ni sumu inayoua biashara yako taratibu, kamwe usiyape nafasi katika biashara yako. Hasara haikwepeki. **Ukiona mbele kuna ukuta usirudi nyuma, we uruke tu**. Kumbuka hasara ni yako. **Hasara inapokupa sababu mia za kulia, ionyeshe sababu elfu za kutabasamu.**

**Nne, hasara ni mtazamo tu, hivyo relax. Kuna watu mvua inaponyesha wanaona tope, wengine wanaona mazao.** Mtazamo ni jambo dogo sana linalofanya tofauti kubwa maishani. **Haijalishi hasara yako ni kubwa kiasi gani, cha msingi kuwa na mtazamo chanya halafu pambana kama Daudi. Daudi alipoona ukubwa wa Goliath, alijipa moyo na kusema walau jiwe langu halitakosa pa kupiga.** Harry Truman aliwahi kusema, **"Mtu mwenye mtazamo chanya hufanya matatizo yake yawe fursa."**

**Tano**, jaribu kuona mazuri katika kila hasara unayoipata na biashara utaiona nyepesi. **Kuna mtu alimwambia mvuvi, wewe huogopi kwenda baharini kuvua samaki? Mjomba wako, baba yako na kaka yako walifia baharini, wewe mbona**

**huogopi? Mvuvi alijibu hivi, "Watu wengi wanakufa wakiwa vitandani lakini watu hawaachi kulala vitandani."** Mvuvi aliona uzuri katika shughuli ya uvuvi. Hata wakati mwingine **uyoga mtamu huota kwenye kinyesi kilichokauka**. Ukiona ubaya wa kinyesi hutokula uyoga. Ukiona hasara tu hutofanya biashara.

**Sita**, k**wa kuwa huwezi kukwepa hasara katika biashara basi ifanye hasara kuwa sehemu ya vitu unavyoweza kuvitawala.** Wakati mwingine hasara inatokea ili uweze kutumia akili alizokupa Mungu. Wenye akili huona fursa kwenye kila tatizo. **Uzuri hakuna hasara inayotugandamiza kwenda chini, badala yeke hutuachia fursa ya kwenda mbele au nyuma.** Songa mbele, usikate tamaa.

**Saba**, ichukulie hasara kama dhiki kuelekea kwenye mafanikio. **Maisha yanapokupa limao, tengeneza juice ya limao badala ya kusema limao ni chachu, maadui wanapokutupia mawe, yakusanye ujenge msingi wa nyumba.** Chukulia hasara kama msalaba unalotakiwa kuubeba ili likubebe.

**Nane, chukulia hasara katika biashara kama weusi ulioko nyuma, mbele ni kweupe**, usikubali kurudi gizani (nyuma). Nyuma siyo pazuri, ndiyo maana mke wa Luthu alivyogeuka nyuma akawa jiwe la chumvi. Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo ni methali ya Kiswahili. **Kukumbuka yaliyopita yatakuondolea furaha yako na kushindwa kufikiria mambo makubwa na mazuri yaliyoko mbele.**

**Tisa, chukulia hasara katika biashara yako kama mawe ya kuvukia kwenda kwenye wazo jipya ambalo usingeligundua bila kupata hasara.** Hasara ni matuta katika barabara kuu ya biashara. Chukulia hasara kama **mapumziko katika shughuli**

**zako za biashara. Hasara ni kituo siyo alama ya nukta.** Mfanyabiashara mmoja aliweka maneno yafuatayo kwenye fremu ya duka lake:

> **"Alishindwa katika biashara mwaka 1831.**
> **Alishindwa tena katika biashara mwaka 1833.**
> **Alichaguliwa kuwa mmoja wa watunga sheria mwaka 1834. Mpendwa wake wa moyo, yaani mke wake aliaga dunia mwaka 1835.**
> **Alishindwa nafasi ya uspika 1838.**
> **Alishindwa kuingia kwenye Congress mwaka 1848.**
> **Alishindwa kuchaguliwa kuwa Elector mwaka 1840.**
> **Alishindwa kuingia kwenye Congress mwaka 1843.**
> **Alishindwa kuingia kwenye Congress Mwaka 1848.**
> **Alichaguliwa kuwa Rais wa Marekani mwaka 1860.**
> **Naye ni Abraham Lincoln."**

**Kumi, hasara katika biashara yako ikukomaze kama maji yanavyokomaza zege. Hata jani la chai linapata nguvu ya kugeuza rangi ya maji likiwa kwenye maji ya moto.** Matatizo yanaongeza nguvu.

Kuanzia leo unatakiwa kufahamu kwamba, "hasara ni alama ya mkato na siyo kituo, hasara ni giza la kukusaidia kuona nyota, hasara ni mawe ya kuvukia, hasara ni mawimbi katika bahari, hasara ni mtazamo, hasara ni ujumbe, hasara ni mwisho wa sura si mwisho wa kitabu, hasara ni weusi ulioko nyuma mbele kweupe, hasara ni sumaku inayokuvuta uwe karibu na Mungu, hasara ni matuta katika barabara kuu ya maisha, hasara ni somo, hasara ni masahihisho, hasara ni ishara ya uhai, hasara ni fursa,"

**Sura ya 24**

# Amri Kumi za Kunasa Wateja

Kwa ujumla ipo shida kubwa katika suala zima la kuwahudumia wateja. Ukianzia madukani mpaka kwenye nyumba za wageni, groceries, baa, maofisini na kwenye nyumba za ibada kwa kiasi kikubwa ***customer care*** ina shida. Mteja hana tofauti na ombaomba tu. Hata baadhi ya maandishi kwenye kuta za biashara ni ya kumdhalilisha mteja. Unakwenda kutafuta huduma unapokelewa na maneno, MWAMBIE MKEO HII BAJAJI SIYO YANGU. Hapa unadhani nani atapanda. Mteja unapokelewa na maneno **LIPA BILA KULAZIMISHWA** utadhani umekwenda kuiba! **USILETE UNDUGU, BIASHARA YANGU HAIKUJUI**.

Mahali pengine unalipia chumba cha kulala unakuta ndala zote ni za mguu mmoja ili usiibe. Mahatma Ghandi aliwahi kusema, “Mteja ni mgeni muhimu katika biashara yetu. Yeye siyo tegemezi kwetu, ila sisi ndiyo tunamtegemea yeye. Tusimuone mteja kama mtu wa kuja tu, ila tumuone kama sehemu ya biashara yetu. Siyo kwamba tunampa favour. No! Yeye ndiyo anatupa favour kwa kukubali tumhudumie.”Katika hili nalo tunahitaji ukombozi wa fikra ili kufahamu nafasi ya mteja katika ujasiriamali watu.

Tunatumia nguvu na gharama kubwa kutafuta wateja lakini tukiwapata tunashindwa kubaki nao. Hatuna tofauti na kondakta wa daladala. Kondakta atakubembeleza upande gari lake, ukiishapanda thamani yako inaishia mlangani. Huko ndani anaweza hata kukwambia kaa chini tupite mizani. Shida ni kwamba hatujui thamani ya HUDUMA KWA WATEJA katika biashara zetu. Bado tunaamini katika fikra za **kizuri cha jiuza**.

Sikiliza, l**engo la huduma kwa wateja ni kumnasa mteja ili na kesho arudi tena.** Ni injini ya biashara yako, ikitetereka hutoona faida ya biashara yako. Badala yake utakuwa ukilia kwamba kuna mkono wa mtu. Huduma nzuri kwa wateja ni tangazo linalotembea kuitangaza biashara yako vizuri bila malipo yoyote. Ukishindwa kuimudu, utamudu kwenda kutafuta wateja kwa washirikina na wakati huduma kwa wateja inahitaji kucheza na saikolojia ya wateja na siyo ushirikina. Lengo la huduma kwa wateja ni kumhudumia mteja ili akalete wateja wengine wengi zaidi.

Sasa hebu tuangalie amri tano sasa za kunasa wateja!

**Amri ya Kwanza: Mteja ni mfalme, mpe heshima yake!**

Tunapokuja katika suala la biashara tunatakiwa kuelewa kwamba bosi ni mmoja tu yaani mteja. Mteja **anauwezo wa kumfukuza kazi kila mtu yoyote yule katika kampuni pale anapoacha kuja kununua.** Bila wateja hakuna biashara inayoweza kufanyika. Sasa kama mabosi na wafalme wanavyopenda kunyenyekewa, ndivyo hivyo wateja wanapenda kunyenyekewa kwa kauli nzuri na za kuvutia.

**Amri ya Pili : Jifunze kusikiliza kwa umakini,**

Mungu amekupa maskio mawili na mdomo mmoja ili vikusaidie kusikiliza sana na kusema kidogo unapokuwa katika ujasiriamali. Kabla hujamjibu mteja wako, msikilize kwa umakini. Wafanyabishara wengi wanamajibu ya hovyo kwa sababu huwa hawasilizi ili kuelewa, wanasikiliza ili kujibu. Kutomsikiliza mteja wako ni ishara kwamba wewe ni mbinafsi hivyo lazima upoteze mteja. Kumbuka **mteja hafokewi, anabembelezwa kwa maneno matamu.**

**Amri ya Tatu: Mpe kipaumbele mteja wako ili kuteka hisia zake!**

Siku zote wateja wanaongozwa na hisia badala ya mantiki, wanapofanya manunuzi ya kununua, ndiyo maana shati la Sh 10,000 anaweza kwenda kulinunua kwa Sh 50,000 kwa muuzaji anayegusa hisia zake. Sasa ili kuziteka hisia za mteja wako, wewe mpe kipaumbele tu. **Mhudumie kama vile yuko peke yake!** Jim Rohn, Mwandishi na Motivational Speaker aliwahi kusema, "One of the greatest gifts you can give to anyone is the gift of attention." Hii husaidia mtu ajisikie vizuri na wa muhimu sana. Ikiwezekana mtaje hata kwa jina lake, au muaddress kwa majina ya kumuinua juu kama wanavyoitana vijana huko mitaani, **chief, mkuu, bosi, mkurugenzi na wakati hakuna lolote**.

Ukifanikiwa kuziteka hisia za wateja wako utashangaa kuona wanavyopanga foleni kutafuta huduma kwako na wakati mnaotoa huduma kama hiyo mko wengi. Washindani wako katika biashara wataogopa kushindana na wewe wakiamini unatumia ushirikina. **Wakati mwingine ujinga ni fursa kwa wenye akili.**

## Amri ya Nne: Karibisha mteja kwa tabasamu na umuage kwa shukurani

Tabasamu humvuta mteja katika biashara yako na kumfanya afungue waleti yake kununua pasipo kulialia punguzo la bei kwa sababu tabasamu ni lugha yenye nguvu kuliko lugha zote duniani. Haijalishi una sura nzuri kiasi gani usipotabasamu sura yako itafukuza wateja. Uzuri wa mtu ni tabasamu na si sura! Kuna methali ya wachina inasema kama huwezi kutabasamu usifungue duka. Atoaye tabasamu hupokea wateja wengi na hii ndiyo ile maana ya kila **atoaye hupokea**. Lakini msindikize mteja wako kwa shukurani kwa sababu ku**shukuru ni kuomba tena walisema wahenga!** Usiposhukuru ni dhahiri haujaona thamani ya mteja wako hivyo usishangae kumpoteza.

## Amri ya Tano! Mteja hakosei

Unapokuwa unafanya biashara ni wazi utakutana na maudhi ya kila aina kutoka kwa wateja. Kuna watakaokuja kwa lengo la kufanya ***window shopping*** na maswali mengi mengi ya kuudhi. Hutakiwa kuchukia hata kidogo kwa sababu kanuni ya kwanza katika biashara inasema hivi, mteja hakosei na kanuni ya pili inasema , akikosea rejea kanuni ya kwanza. Ili kufanikiwa katika biashara tembea na kanuni ya **kusamehe saba mara sabini.**

Sasa kama unasimamia biashara yako mwenyewe zingatia haya na kama umeajiri mtu msisitize azingatie haya na matokeo yake yatakushangaza.

# Sura ya 25

# Dhambi Saba Takatifu

Nimeziita dhambi takatifu kwa sababu tunazifanya pasipokujua kama ni dhambi ndo maana uzitendapo hakuna atakayekukemea na wala siku ya toba hakuna anayezitubu!

**Dhambi ya Kwanza!**

Tunatumia muda mwingi katika kumuomba Mungu vitu ambavyo hatuna badala ya kushukuru kwa vitu tulivyonavyo. Hapa lazima Mungu akuone punguani. Yaani ni sawa na wewe hapo umejinyima kweli ukamsongeshea girlfriend wako vijisent halafu anakwambia hela gani hii sasa? Hebu niambie utajisikiaje hapo? Wewe jamaa yako amejikamua kakutumia 50 unasema ni vijisenti na wakati kuna mwanamke mwenzako kupata buku tano tu lazima ainue vyuma. Shakespeare aliwahi kusema, "Nililia wakati sina viatu, ila niliacha kulia baada ya kumwona mtu hana miguu." Unatumiwa pesa unalalamika kwamba hajakutumia na ya kutolea. Kuna mwenzako kupata buku tano tu lazima ebebe zege!

Unamlilia Mungu akupe gari badala ya kushukuru kwanza kwa pikipiki uliyonayo! Unaomba tu na wakati una vitu kibao hujashuhuru. Sikiliza kabla hujaomba lolote kwa Mungu hebu hesabu baraka ulizonazo uone kama haijakuchukua mwaka mzima ukishukuru tu. Kushukuru ni kuomba tena walisema wahenga. Usiposhukuru shetani atatenda, ukishukuru Mungu atatenda! Maisha yamejaa baraka tele lakini tumeshindwa kuzithamini.

Kuna mwingine analia kwa sababu hana kazi, mwingine analia kwa sababu kazi ni nyingi, mwingine analia hana watoto mwingine analia watoto wanamsumbua, mwingine analia ndoa inamtoa jasho mwingine analilia ndoa mwaka wa 38 hajachumbiwa. Shukuru kwanza kwa ulivyonavyo!

**Dhambi ya Pili**

Tunampa sifa na utukufu shetani kwa mafanikio ya watu na kumlaumu Mungu kwa balaa zinazotupata. Akipata mtu ajali akakatika kichwa tunasema ni kazi ya Mungu, mtu huyo akinunua magari mengi kwa mkupuo tunasema ni Freemason! Ukinusurika ajali unasema machale yalikucheza, ukipata ajali unasema alipanga Mungu! Mtu akipanda cheo kutokana na juhudi zake tunasema ametambikia, akifukuzwa kazi kutokana na uzembe wake tunasema ni mapenzi ya Mungu atapata kazi nyingine. Dhambi hii ya kumdhalilisha Mungu kiasi hiki haiwezi kutuacha salama. Tubu ndugu yangu!

**Dhambi ya Tatu**

Yaani linapokuja suala la kumtafuta Mungu tunakuwa paka na panya, full kupondana. Muislam anamuita Mkristo kafiri, Mkristo anamuita Muislam mtu wa Mataifa, Mpagani anawaita wote Machizi lakini wanapokuwa kwenye pombe wanagonga cheers. Yaani huwezi amini kama hawa ndo walikuwa wanaitana makafiri. Acha pombe, njoo kwenye mapenzi ndo utashangaa. Unakuta penzi limekolea kati ya mpagani na mkristo hadi Mungu anasema hawa jamaa vipi?

Hata wakiwa safarini, mpagani, muislamu na mkristo wanapanda basi moja na wanapiga stori kuifanya safari kuwa fupi lakini huwezi kuwakuta katika nyumba moja wakimsifu Mungu! Hata kwenye mazishi ni jambo la kawaida kaburi la mkristo kuchimbwa na mpagani na mambo yanakwenda fresh. Watu

walioajiriwa na mtu mmoja hawawezi kuajiriwa na Mungu! Ndo maana kuna mambo tunatakiwa kutafakari kwa kina. Hivi Mungu kweli ndo anaweza kuwa chanzo cha kuwatenganisha watu?

**Dhambi ya Nne**

Kila mtu anategemea kuvuna alikopanda badala ya kutegemea kuvuna alichopanda. Utasikia kweli shukrani ya punda ni mateke, heri kumfadhili mbuzi utakunywa supu kuliko kumfadhili binadamu akaishia kukujambia. Halafu mbaya zaidi unakuta anayelalamika ni Mkristo anayesoma Biblia kila siku pasipokuielewa. Bora hata Wahenga waliposema tenda wema uende zako walionyesha kuielewa Biblia. Galileo Galilee aliposema Biblia haikuandikwa kwa watu wote, bali kwa watu wenye akili alimaanisha hivyo!

Kuna watu wameisoma Biblia ikawabinua! Wengine wameisoma Biblia wakaishia kufanya mambo ya ajabu hadi madhabahuni, jamii ikawaita vichaa! Kumbe kazi yako wewe ni kutenda wema, na kusubiri kulipwa mema. Ndo maana unaweza kusomesha watoto 12 wakashindwa kukutunza, ukaja kutunzwa na watu baki kabisa! Hapo usiwalaani watoto wako, badala yake shukuru kwa wema uliotenda kwa watoto wako. Leo utamtendea mwenzako mabaya ukashangaa watoto wako nao wanatendewa mabaya na watu wengine kabisa. Pengine hata wewe balaa unazopitia ni matendo mabaya ya babu zako kwa watu wa Mungu. Lakini pia pengine Baraka unazokula leo ni matunda ya wema waliofanya wazazi wako kwa watu baki!

**Dhambi ya Tano**

Tumelifanya somo la Kingereza ambalo halitulishi kuwa somo la lazima kwa kila mwanafunzi na somo la Kilimo linalotulisha kuwa somo la ziada kwa kila mwanafunzi. Halafu bado tunasema kilimo ni uti wa mgongo wa taifa. Huoni kama hiyo ni dhambi

takatifu? Ndiyo maana hatuishiwi njaa pamoja na kuwa na ardhi nzuri, hali ya hewa safi tunaishia kulishwa mchele wa maplastiki kutoka China. Ukijitambulisha ni mkulima jamii inakuonea huruma lakini ukizungumza Kingereza kizuri watu wanakumezea mate. Hii nayo ni dhambi takatifu tunayotakiwa kuitubu! Kumbuka dhambi haikupi muda, ukikosea inakulamba pale pale. Dhambi inayotutoa jasho kwa kudharau kilimo ni kubwa.

**Dhambi ya Sita**

Tunahamasishana kufanya kazi kwa bidii badala ya kufanya kazi kwa akili. Dunia siku zote inaongozwa na watu wanaotumia akili vizuri! Kuna kisa cha Mchina na Mapaka kutoka mitandaoni. Anakuja Mchina anasema anahitaji paka, ananunua mmoja kwa 20,000/=, basi wanakijiji wanahaha kusaka paka, wanawaleta, Mchina ananunua wote anaondoka nao. Anarudi tena anasema, "vipi, naona wameadimika, sasa ntanunua kwa bei ya 35,000 paka mmoja." Wanakijiji wanaenda msituni, kamata Paka, leta kwa mchina, mchina anasepa nao, wiki inayofuatia Mchina anasema "bado anataka paka, saivi nitanunua kwa laki moja moja." Wanakijiji macho yamewatoka, hawana tena paka. Mchina anasema "basi nitafutieni kwa laki na nusu." Kesho yake inasikika kuwa kuna Mchagga anauza paka kijiji cha pili, anauza kwa laki moja, wanakijiji wanawahi kijijini kununua paka wote wa kijiji cha pili. Wanarudi kijijini hawana pesa ila wana mapaka wakijua watamuuzia mchina kwa laki na nusu, Mchina hatokei Ng'oooo! Kumbe yule Mchina alikuwa anawakusanya tu na kuwahifadhi kule kijiji cha pili akijua atakuja wauza kwa laki moja moja kwa hawa hawa wa kijiji hiki. Bila shaka unaona kazi ya akili. Sifurahii Mchina alivyowaumiza wanakijiji, nafurahia namna alivyowaingiza mtegoni. Ndivyo dunia inavyoendeshwa. Sasa kuendelea kuhimizana ati tufanye kazi kwa bidii ni kutenda dhambi takatifu. Hard workers die poor, smart workers die rich. Smart workers employ hard workers alisema Pasta Mensah Otabili.

**Dhambi ya Saba**

Kila mtu anayekuja kwako anavitania vitoto vyako vya kike, mchumba umependeza, mchumba ntakuoa, mchumba sijui nini! Hili ni kosa kubwa sana kwa usalama wa watoto wako. Kakizaliwa katoto ka kike hata hakajaanza kukaa kanabebeshwa misuko ya kila aina, mara rasta, mara wigi, mara dawa kichwani halafu baada ya kusukwa kanakutana na mibabu inakatania...mchumbaaa wangu...mke wangu...ntakuoa, katoto kadogo kichwani kanajazwa akili za mawigi na mapenzi, haka hata kakipelekwa shule hakawezi kuwa na akili ya kuvumbua vitu zaidi ya kuwaza mawigi na mapenzi halafu kakiolewa kakawa kakunguru tunasema wanawake wa siku hizi ni hovyo! Kumbe hovyo ni sisi wazazi na walezi! Hii ni dhambi takatifu. Huyu mtoto atakua akijua maisha ni kujipodoa na kuolewa basi. Kanatobolewa masikio hadi mapua. Mtoto mdogo anashinda saluni kusukwa badala katulie nyumbani kalale.